

**SUALA LA UHAMAJI NA UHAMIAJI KAMA  
LINA VYOENDELEZWA KATIKA RIWAYA YA *MBALI* NA  
*NYUMBANI* YA ADAM SHAFI.**

**NA**

**KAROKI EMAITTA**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA IDARA YA  
KISWAHILI.**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

**NOVEMBA 2014.**

## **IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

.....

.....

KAROKI EMAITTA

TAREHE

(MWANAFUNZI)

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu cha Nairobi

.....

.....

DR. ZAJA OMBOGA

TAREHE

(MSIMAMIZI)

.....

.....

DR. MWANGANGI WA MUSYOKA

TAREHE

# **TABARUKU**

Tasnifu hii naitabaruku kwa familia yangu ninayoipenda sana kwa kunitia moyo na kujitolea

kwao kwa njia mbalimbali nikisoma. Hawa ni:

**Bwanangu, Patrick Murugu na watoto wangu; Mugambi, Naitore, Kimathi na Karambu.**

## SHUKRANI

Kwanza ningependa kumshukuru Mwenyezii Mungu kwa kuniwezesha kufika hapa. Bila Yeye, singeweza kumaliza masomo yangu. Nimepitia changamoto nyingi lakini kwa sababu ya neema, uwezo na wema Wake, nimefika mwisho wa safari hii ndefu.

Shukrani zangu maalum kwa wasimamizi wangu wawili: Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Mwangangi wa Musyoka. Licha ya kuwa wahadhiri wangu, wamenifaa na kunisaidia sana kwa kunielekeza katika kazi yangu. Bila uelekezi wao singefanikiwa katika kazi hii.

Pia natoa shukrani kwa wahadhiri wote katika idara ya Isimu na Lugha – Chuo Kikuu cha Nairobi. Mchango wao wa kimafunzo na kimawaidha umenifaa sana na ndio ulionifikisha hapa. Hawa ni pamoja na: Profesa M.H. Abdulaziz, Profesa John Habwe, Profesa Kithaka wa Mberia, Profesa Mwenda Mbatiah, Dkt. Ayub Mukhwana, Dkt. Tom Olali, Dkt. Amiri Swaleh, Profesa Kinene Wamutiso, Profesa Wamitila, Bwana Mungania na Dkt. Alfred Buregeya.

Wenzangu tuliosoma nao pamoja, nawashukuru kwa msaada wa aina yoyote hasa kuhimizana na kushauriana. Hawa ni: Ann Njoroge, Ann Raitania ( aliyenipa msaada wa kipekee), Millicent Auko, Rose Mirianga, Benjamin Kilanga, Mary King'ora na James Mburu.

Shukrani nyingi pia zimwendee rafiki yangu mpendwa Lina Akaka kwa usaidizi mwingi alionipa wa aina mbalimbali. Mungu akubariki. Mwisho kabisa, ningependa kuwashukuru wengine wote walionihimiza na kunitia moyo wakati wa masomo yangu. Juhudi zenu na kuhusika kwenu ndivyo vilivyochangia kukamilika kwa kazi hii.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu suala la uhamaji na uhamiaji kama linavyoendelezwa katika riwaya ya kitawasifu ya *Mbali na Nyumbani* iliyoandikwa na Adam Shafi. Suala la uhamaji na uhamiaji ndilo lililotawala riwaya nzima kutoka mwanzo hadi mwisho. Mwandishi wa riwaya hii ameathiriwa na suala hili la uhamaji na uhamiaji kwani ameyapitia hayo yote. Hii ndiyo sababu riwaya yenyewe inaitwa ya kitawasifu. Uhakiki wetu umeongozwa na nadharia ya uhalisia ambayo hujikita katika utoaji wa picha halisi ya maisha ya binadamu. Nadharia hii ina vipengele vingi lakini sisi tumetumia vipengele vitatu. Hivi ni: Kipengele cha kihistoria, kisiasa na kitamaduni. Kazi hii imelenga kushughulikia tatizo la utafiti ambalo linahusu uhamaji na uhamiaji. Matatizo yanayowakumba wanajamii katika sehemu mbalimbali za ulimwengu hasa mataifa ya ulimwengu wa tatu ndiyo yaliyotusukuma kufanya utafiti huu. Matatizo haya yanazidi kuangaziwa kila uchao kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, tumechambua maudhui yanayoingiliana na suala la uhamaji na uhamiaji katika riwaya husika. Sababu yenyewe ni kwamba, maudhui hayo yanachangia katika kuboresha au kufanya maisha ya wahusika kuwa magumu wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji. Si hayo tu bali tumefafanua aina za uhamaji na uhamiaji zinazopatikana katika riwaya yenyewe. Vilevile, tumeangalia sababu zinazochangia hali hiyo na manufaa ya uhamaji na uhamiaji. Zaidi ya hayo, tumeeleza kwa kina matatizo yanayowakumba wahusika katika riwaya hii na jinsi wanavyojaribu kuyatatua. Katika utafiti huu, tumegundua kuwa matatizo yanayowakumba wahusika katika riwaya hii ni yaleyale yanayowakumba watu wengine wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji popote pale. Baada ya kupata hayo, tunapendekeza kwamba, serikali na mataifa yaliyokumbwa na tatizo hili yajaribu kuweka mikakati ya kuchunguza kiini chake na kutafuta njia za kulitatua kabla halijaharibu mishikamano ya wanajamii.

# YALIYOMO

Mada.....	i
Ikirari.....	ii
Tabaruku.....	iii
Shukrani.....	iv
Ikisiri.....	v
Yaliyomo.....	vi
Alama Zilizotumika.....	xi
<b>SURA YA KWANZA.....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi.....	1
1.1 Tatizo La Utafiti.....	10
1.2 Madhumuni Ya Utafiti.....	11
1.3 Nadharia Tete.....	11
1.4 Sababu Za Kuichagua Mada hii.....	12
1.5 Upeo Na Mipaka.....	12
1.6 Msingi Wa Kinadharia.....	13
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii.....	18
1.8 Njia Za Utafiti.....	24
1.9 Hitimisho.....	24

**SURA YA PILI.....25**

2.0 Utangulizi.....25

2.1 Dhana Ya Uhamaji Na Uhamiaji.....25

2.2 Ukarimu.....27

2.3 Kutokuwa na Roho Ya Kusaidiana.....36

2.4 Tamaa Ya Pesa.....39

2.5 Ufisadi.....41

2.6 Ukoloni na Siasa.....43

2.7 Maamuzi Mabaya.....48

2.8 Azma.....52

2.9 Hitimisho.....55

**SURA YA TATU.....56**

3.0 Utangulizi.....56

3.1.0 Aina Za Uhamaji Na Uhamiaji.....56

3.1.1 Uhamaji Na Uhamiaji Wa Hiari.....57

3.1.1.1 Uhamaji Zanzibar.....58

3.1.1.2 Uhamaji Mombasa.....58

3.1.1.3 Uhamiaji Bungoma Na Nakuru.....59

3.1.1.4 Uhamiaji Misri.....59

3.1.1.5 Uhamiaji Ujerumani.....60

3.1.1.6 Uhamiaji Zanzibar.....	60
3.1.1.7 Uhamaji Na Uhamiaji Wa Abdalla Juma Bulushi Na Shabaan Salim.....	61
3.1.1.8 Uhamaji Na Uhamiaji Wa Nduguye Shafi.....	61
3.1.2.0 Uhamaji na Uhamiaji Wa Kulazimishwa Na Hali Ya Mambo.....	61
3.1.2.1 Uhamiaji Mombasa Na Eldoret.....	62
3.1.2.2 Uhamiaji Kampala Na Khartoum.....	62
3.1.2.3 Uhamiaji Katika Kambi Ya Kijeshi Na Zanzibar.....	63
3.2.0 Sababu Za Uhamaji Na Uhamiaji.....	64
3.2.1 Kupata Elimu.....	64
3.2.2 Ukosefu Wa Pesa.....	69
3.2.3 Uhitaji Wa Kazi.....	71
3.2.4 Kutafuta Viza.....	72
3.2.5 Kupata Mafunzo Ya Kijeshi.....	73
3.2.6 Kukomboa Nchi Zao.....	74
3.2.7 Kuanza Maisha Mapya.....	75
3.3.0 Kutathmini Manufaa Ya Uhamaji na Uhamiaji.....	75
3.3.1 Manufaa Ya Kiuchumi.....	76

3.3.2 Manufaa ya Kisiasa.....	77
3.3.3 Manufaa Ya Kijamii.....	81
3.4.0 Hitimisho.....	84
<b>SURA YA NNE.....</b>	<b>85</b>
4.0 Utangulizi.....	85
4.1.0 Matatizo Ya Uhamaji Na Uhamiaji.....	86
4.1.1 Matatizo Ya Kijamii.....	87
4.1.1.1 Matatizo Ya Safari.....	87
4.1.1.2 Shida Za Chakula.....	93
4.1.1.3 Shida Za Malazi.....	94
4.1.1.4 Shida Za Lugha.....	98
4.1.1.5 Mateso Ya Kisaikolojia.....	102
4.1.2 Matatizo Ya Kiuchumi.....	103
4.1.2.1 Mawazo Ya Kisaikolojia Yanayohusiana Na Ukosefu Wa Pesa.....	103
4.1.2.2 Shida Za Pesa.....	105
4.1.2.3 Ukosefu Wa Ajira.....	107
4.1.2.4 Changamoto Za Kikazi.....	108

4.1.3 Matatizo Ya Kisiasa.....	110
4.1.3.1 Sheria Za Uhamiaji.....	110
4.1.3.2 Changamoto Za Kijeshi.....	115
4.2.0 Suluhisho La Matatizo Ya Uhamaji na Uhamiaji.....	117
4.2.1 Utatuzi Wa Masuala Ya Kisiasa.....	117
4.2.2 Utatuzi Wa Masuala Ya Kijamii.....	119
4.2.3 Utatuzi Wa Masuala Ya Kiuchumi.....	121
4.3.0 Hitimisho.....	122
<b>SURA YA TANO.....</b>	<b>123</b>
5.0 Utangulizi.....	123
5.1 Muhtasari Wa Matokeo Ya Utafiti.....	123
5.2 Mapendekezo.....	126
<b>MAREJELEO.....</b>	<b>127</b>

## **ALAMA ZILIZOTUMIKA**

1. A.N.C. - African National Congress.
2. K.D.F. - Kenya Defence Forces.
3. k.h.j. – Kama hapo juu
4. T.U.K.I. – Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili
5. uk. – Ukurasa
6. U.N.H.C.R. – United Nations High Commission for Refugees.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Kabla ya kujadili swala la uhamaji na uhamiaji, tumeanza kwa kuangalia baadhi ya kazi za Adam Shafi. Huyu ndiye mwandishi wa riwaya ya kitawasifu ya *Mbali na Nyumbani* na alizaliwa mjini Zanzibar mwaka wa 1940. Ni mwandishi aliyekomaa katika maandishi ya kifasihi hasa uandishi wa riwaya. Ameandika vitabu kama vile: *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978), *Kuli* (1979), *Vuta N'kuvute* (1999), *Haini* (2003) na *Mbali na Nyumbani* (2013) ambacho ndicho tunachoshughulikia.

Kitabu cha kwanza alichokiandika Adam Shafi ni *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978). Hiki ni kitabu kinachosawiri mvutano baina ya ubwana na umwinyi kwa upande mmoja na unyonge na utwana kwa upande mwingine. Mamwinyi hawa ambao wamemiliki mashamba makubwa makubwa wanaishi maisha ya ukwasi na starehe ilhali watumishi wao wanaishi maisha ya kudhulumiwa na kufukarishwa kwingi.

Kitabu kingine alichokiandika kinaitwa *Kuli* (1979). Hiki kinaongea juu ya maisha ya Kuli ambaye kazi yake ni ya kijungu-jiko na iliyojaa hatari na ajali nyingi. Anafanya kazi za sulubu za kubeba mizigo kwa rukwama, kupakia na kupakua mizigo bandarini na nyinginezo, lakini malipo ni kidogo sana yakilinganishwa na kazi ngumu anayoifanya. Hatari ya kazi ya ukuli inadhihirika wakati Majaliwa babake mhusika mkuu, Rashid anaaga dunia kwa sababu ya ugonjwa uliotokana na kazi hiyo. Wafanyakazi wengine hukatika viungo vya mwili na wengine hugongwa na kreni na kufa. Migomo ya wafanyikazi kwa ajili ya ujira mdogo na hali duni ya maisha hupelekea wengi kufutwa kazi. Sababu ii hii ndiyo inayomfanya Rashid kuhukumiwa kifungo cha miaka mitatu na kazi ngumu gerezani.

Pia ameandika riwaya inayoitwa *Haini (2003)*. Riwaya hii inahusu kukamatwa kwa Hamsa, kijana mwandishi wa habari (mhusika mkuu) na watu wengine wengi kwa kutuhumiwa kuwa mahaini waliohusika katika kuuawa kwa kiongozi wa nchi moja barani Afrika. Sehemu kubwa ya riwaya hii inasimuliwa gerezani ambako mhusika mkuu na watu wengine wanateswa, wanadhalilishwa na kutendewa unyama wa kila namna. Walakini, mwishowe Hamsa na wengine wanaachiliwa huru kwa kutopatikana na hatia ya mauaji ya kiongozi huyo. Vitabu hivi vya kwanza vitatu vinaangazia dhuluma na unyonyaji unaotendewa wanyonge na wenye nguvu.

Hizo ni baadhi ya riwaya alizozindika Adam Shafi pamoja na *Mbali na Nyumbani (2013)* ambayo ndiyo tunayoishughulikia katika kazi yetu. Kazi hizi zinaonyesha kuwa, Adam Shafi ni mwandishi aliyekomaa katika uandishi wa kifasihi. Kwa kifupi, tunaweza kusema kwamba kazi hizo zake zote ni za kihalisia. Hii ni kwa kuwa, mambo yote aliyoshughulikia katika kazi hizo zake yamewahi kutendeka au yanaweza kutendeka katika maisha ya kawaida ya binadamu.

*Mbali na Nyumbani* ni riwaya ya kitawasifu. Maoni yetu kuhusu maana ya tawasifu ni kwamba, mwandishi wa kazi hii hueleza juu ya maisha yake kinyume na kazi ya wasifu. Madumulla, (2009:61) anasema kuwa, riwaya ya kitawasifu huhusu maisha ya mtu binafsi akieleza mambo yake mwenywe. Anaendelea kusema kuwa mwandishi hueleza maisha yake yaliyopita na hata matarajio yake.

Tuki, (2010:44) nayo pia ina maoni yayo hayo kwamba tawasifu ni habari za maisha ya mtu zilizoandikwa na yeye mwenyewe. Katika fasihi ya Kiswahili, diwani ya Shaaban Robert inayoitwa, *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini (1966)*, *Siku Njema (1996)* iliyoandikwa na Ken Walibora na *Mbali na Nyumbani (2013)* ya Adam Shafi ni baadhi ya tawasifu chache zilizoandikwa.

Tukijaribu kueleza maana ya riwaya tunaona kuwa, riwaya ni utungo mrefu wa kifasihi ulioandikwa kwa lugha ya nadhari. Pia una maudhui mengi na wahusika wengi. Senkoro (1982:73-74) anasema, “Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana, maisha ya jamii.” Msokile (1992:207-208) anasema, “Riwaya ni kazi ya sanaa ya kubuni. Ni maandishi ya nathari yanayosimulia hadithi ambayo kwa kawaida ina uzito, upana na urefu wa kutosha. Ina wahusika mbalimbali wenye tabia za aina nyingi.”

Wamitila (2002:5) anasema, “Riwaya ni kazi iliyoandikwa kwa mtindo wa kinathari ambayo ina urefu wa kiasi fulani, ni pana, ina uchangamano wa kimitindo na kidhamira na inashughulikia masuala kadhaa katika mtazamo mpana wa wakati.” (Khj:2010:278) anasema kuwa riwaya huwa ndefu na huweza kuchukua muda mrefu kusomwa. Kulingana na maoni yetu na maelezo ya maandishi hao, tunaweza kusema kuwa kitabu hiki cha *Mbali na Nyumbani* licha ya kuwa tawasifu, pia ni riwaya. Hii ni kwa sababu ni ndefu kwani ina kurasa mia nne themanini na mbili, ina wahusika wengi na ina visa vingi kwani ina maudhui mengi.

Swala la uhamaji na uhamiaji limejitokeza sana katika riwaya ya kitawasifu ya *Mbali na Nyumbani* ya Adam Shafi. Uhamaji unaweza kufafanuliwa kuwa ni hali ya mtu kutoka mahali alipokuwa akiishi na kwenda kuishi mahali pengine. Uhamiaji nao ni kule kwa mtu, watu au jamii ya watu kuingia mahali na kuanza kuishi hapo. Tunaweza kutoa mfano wa uhamiaji wa jamii mahali kama vile jamii ya Wasomali iliyoingia Kenya na kuhamia mtaa wa Eastleigh. Istilahi hizi mbili huandamana pamoja kwa sababu hatua ya kwanza ambayo ni uhamaji lazima ifanyike ili hatua ya pili ambayo ni uhamiaji nayo itekelezwe. Kwa mfano, ili jamii hii ihamie Eastleigh, iliwabidi kwanza wahame kutoka kwao Somalia.

Suala la uhamaji na uhamiaji limekuweco tangu historia ya mwanadamu, lingaliko na litaendelea kuweco. Hii ni kwa sababu hali hizi huchochewa na mambo mbalimbali. Mambo haya ni pamoja na masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hata tukirejekea historia ya makabila mbalimbali nchini Kenya na kwingineko, tunaona kuwa uhamaji na uhamiaji wao ulizungukwa na masuala yayo hayo matatu. Utafiti wetu unadhamiria kujibu maswali kama vile, ni nani au ni akina nani wanaohama na wanahamia wapi? Kuna aina gani za uhamaji na uhamiaji? Ni nini husababisha uhamaji na uhamiaji huu? Kuna manufaa yoyote yanayotokana na uhamaji na uhamiaji? Kuna matatizo yanayoambatana na uhamaji na uhamiaji huu? Swali la mwisho kabisa ni, ni vipi wahusika wanavyojaribu kuyatatua matatizo hayo?

Kwa kifupi, riwaya tunayoihakiki inahusu mambo halisi kwani ni ya kitawasifu na kazi tunayoishughulikia pia inaangazia matukio halisi. Tunasema ni matukio halisi kwa sababu masuala ya uhamaji na uhamiaji yanaendelea kushuhudiwa kila siku katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kwa mfano, ukisikiliza masimulizi ya watu mbalimbali, utagundua kwamba ni vigumu kupata mtu ambaye ameishi mahali pamoja maisha yake yote. Wengi huongea juu ya kuhama mara mbili au zaidi. Walakini, uhamaji na uhamiaji huu hutofautiana kutegemea umbali na muda watu hukaa mahali pamoja kabla ya kuhama tena. Sababu za uhamaji ndizo huamua aina za uhamaji zinazohusika. Kwa mfano, ikiwa uhamaji na uhamiaji huo ni wa hiari, ni wa kulazimishwa na vile hali ya mambo ilivyo au ni wa lazima (kuhamishwa). Uhamaji na uhamiaji unaojitokeza katika kazi yetu ni wa aina za kwanza mbili. Hii ni kwa sababu, mwandishi wa riwaya tunayoishughulikia amepitia uhamaji na uhamiaji wa hiari na wa kulazimishwa na hali ya mambo ilivyo kule aendako.

Uhamaji wa pili pia hutokea mara nyingi wakati wa vita ambapo watu wakiona mambo yamechacha na maisha yao yamo hatarini, hujiamulia wenyewe kuhama huko na kwenda

kutafuta hifadhi kwingine. Wakati mwingine serikali ya nchi husika yaweza kujitolea kuwahamisha raia wake kutoka eneo lenye vita na kuwapeleka mahali kwenye usalama. Hivyo ndivyo mambo yalivyotokea nchini Kenya baada ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi wa mwaka wa 2007 Disemba. Uhamaji huu ndio sana sana husababisha hali ya ukimbizi mahali kwingi ulimwenguni. Nchini Kenya, watu waliotoroka makwao wakati huo wa vita vya kikabila vya baada ya uchaguzi tulioutaja hapo juu ni wale tunaowaita wakimbizi wa ndani kwa ndani kwani ni wakimbizi isipokuwa wako katika nchi yao. Lakini wakimbizi wengi ni wale wanaohama kwao kwa sababu ya vita na ukosefu wa usalama. Hawa hutafutiwa hifadhi na Shirika la Umoja wa Mataifa (UNHCR) linaloshughulikia masuala ya wakimbizi ulimwenguni. Kenya kwa mfano imewapa hifadhi wakimbizi wengi kutoka nchi mbalimbali kama vile: Somalia, Rwanda, Congo na sasa Sudan ya Kusini. Hawa wote wamekuwa wahamiaji nchini Kenya. Si Kenya tu bali kuna nchi nyingine nyingi ambazo zimehamiwa na wakimbizi kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu. Marekani kwa mfano inapambana na tatizo la uhamiaji.

Aina nyingine ya uhamaji ni ule wa lazima. Hapa mhusika hana uhuru wa kujiamulia ikiwa anataka kuhama ama hataki. Anajipata tu akihamishwa bila kupenda kwake. Huu ndio ule uhamaji ambao Malwyn (1960:4) na Cernea (1993) wanaouita uhamishwaji wa ghafla unaosababishwa na majanga ya kawaida kama vile; mafuriko, mitetemeko ya ardhi na mengineyo. Hata huu pia hupelekea watu kuwa wakimbizi wanakoenda.

Jambo jingine ambalo linazingira suala la uhamaji na uhamiaji linahusu sababu zake. Sababu za uhamaji na uhamiaji zinatokana na mambo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Sababu za kijamii ni kama vile: ndoa, mizozo ya kifamilia, ongezeko la watu, elimu na mengineyo. Kuhusu ndoa, kwa mfano mwanamke anapolewa hutoka kwao na kwenda kujiunga na bwanake. Katika tukio kama hilo, mwanamke huwa amehama kwao na kuhamia kwa bwanake. Wakati mwingine

wanaume wanapooa, huamua kuhama pale kwa wazazi wao na kwenda kuishi pahala pengine. Inaweza kuwa ni katika shamba lile lile lakini sasa anahamia mahali pengine kando na pale alipokuwa akiishi kabla ya kuo. Wengine hata huhama kwao na kwenda kukodi nyumba nje au mijini. Wengine pia huamua kununua nyumba mijini, kiwanja ama shamba ambamo hujenga na kuhamia huko.

Mizozo ya kifamilia pia ni kichocheo kingine cha uhamaji na uhamiaji. Mizozo hii hutokana na mambo mbalimbali kama vile, fitina zinazotokana na wivu kati ya ndugu na mwingine au kati ya wanawake waliiolewa na ndugu katika familia moja. Hawa hupigania mashamba na mengineyo. Mapigano ya aina hii huwalazimu wale wasiopenda mizozo kuhama hapo na kwenda kutafuta hifadhi mahali pengine penye amani na utulivu.

Ongezeko la watu vilevile huchochea uhamaji na uhamiaji. Idadi ya watu ikizidi kiasi kinachotakikana mahali popote, baadhi ya watu hulazimika kuhama hapo na kwenda kutafuta mahali kwingine kwenye nafasi nzuri na ya kutosha. Hapa tunamaanisha mahali penye utoshelezi wa mahitaji yao yote ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Hii ndiyo sababu iliyopelekea kuhama kwa baadhi ya watu kutoka sehemu moja ya Bonde la Ufa. Hawa walienda na kuhamia katika msitu wa Mau ambapo watolewa na serikali ili kuzuia uharibifu wa misitu.

Elimu ni kichocheo kingine cha uhamaji na uhamiaji. Hii ni kwa sababu, ikiwa elimu unayotaka haipatikani kwenu, itakubidi utoke kwenu uende kule utakapopata elimu hiyo. Kwa mfano, kama mtu aenda ng'ambo kwa masomo zaidi, atakuwa amehama kwao na kuhamia huko kwa kipindi hicho chote atakachokuwa akisoma. Huu ndio uhamaji ule unaojitokeza katika safari ile ya mwandishi wa riwaya ya *Mbali na Nyumbani*.

Sababu za kiuchumi ni pamoja na: uendelezaji wa kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara na mengineyo. Wakulima hupenda kuishi mahali kunakopata mvua ya kutosha na kwenye ardhi iliyo na rutuba. Kwa vile kilimo ni uti wa mgongo kwa uchumi wao, mvua ikikosekana kwa muda mrefu mfululizo, huwa hawana jingine la kufanya ila kuhama huko. Wanapohama, hutafuta mahali kwingine kunakopata mvua ya kutosha ili waendeleo na ukulima wao. Jamii za wafugaji nazo huishi maisha ya kuhamahama kwani hupenda kuhamia mahali mifugo wao watapata lishe ya kutosha na maji. Kwa hivyo uhamaji wao husukumwa na mahitaji ya mifugo wao.

Biashara ni kichocheo kingine cha uhamaji na uhamiaji. Biashara ni za aina nyingi na hufanywa kote ulimwenguni. Kuna wafanyibiashara ambao hufanya biashara zao wakienda na kurudi mahali wanapoishi na kuna wengine wanaopenda kuhamia kule wanakofanyia biashara zao. Mtu akiona biashara yake haiendi vizuri mahali anapoifanyia, anaweza kuhama hapo na kuhamia kule anaona biashara yake itanawiri vizuri. Tunaweza kutoa mfano wa biashara za makampuni ya kimataifa ambazo baadhi yao huendelezwa na watu kutoka nchi mbalimbali wakiwa wahamiaji katika nchi wanazofanyia biashara. Kwa hivyo, ili biashara hizo zifaulu, ni lazima wahame kwao na wahamie nchi hizo. Kwa mfano, tuna wageni wengi waliohamia Kenya kwa lengo lilo hilo.

Wavuvi nao hupendelea kuishi karibu na mito na maziwa ili waendeleze maisha yao ya uvuvi. Mito ikikauka, huenda kutafuta mahali pengine ambapo watapata maziwa na mito mingine wahamie karibu nayo.

Sababu za kisiasa ni kama vile, uvamizi wa jamii moja na nyingine ili kupanua mipaka ya kiutawala. Katika tukio kama hilo, jamii ile dhaifu iliyoshindwa hulazimika kuhama hapo na kuhamia kwingine. Jamii ile iliyoshinda nayo huhamia hapo. Wakati mwingine si lazima walioshindwa wahame. Wanaweza kukubali kusimilishwa kwa kuungana na wageni na kukubali

matakwa yao na wazingatie sheria zao. Mfano huu unaingiliana vizuri na ule wa wakoloni ambao walivamia nchi nyingine na kuanza kuzitawala kimabavu. Huu ni uhalisia wa kihistoria na kisiasa kwani mambo ya ukoloni ni historia sasa. Nayo mambo ya utawala yanahusina na siasa. Ili utawala wa kikoloni ufanikiwe, iliwapasa baadhi ya wazungu hao wahame kwao na wahamie katika nchi walizozitawala. Hiyo ni baadhi ya mifano ya mambo yanayosababisha uhamaji na uhamiaji.

Uhamaji na uhamiaji huandamana na matatizo mbalimbali. Haya ni pamoja na matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Matatizo ya kijamii ni kama vile: shida za usafiri, chakula, malazi, ukosefu wa lugha ya mawasiliano ikiwa mhamiaji haelewi lugha ya huko na shida nyingine nyingi zinazowakabili watu wakiwa katika hali ya ugenini.

Matatizo ya kiuchumi ni kama vile, ukosefu wa pesa za kugharamia mahitaji yote ya kibinadamu, ukosefu wa ajira kwa sababu mtu anahitaji kazi ya kumwezesha kuendeleza maisha yake na mengineyo. Shida ya pesa ndiyo iliyokuwa imewasukuma wakimbizi hivi majuzi. Wakimbizi hawa walikuwa wametoka kambi zao na kuanza kuzurura jijini Nairobi wakitafuta vibarua. Msako ulipoanzishwa na serikali, wahamiaji ambao hawakuwa na stakabadhi zifaazo walikabiliwa na changamoto maridhawa. Waliopatikana bila vyeti vifaavyo, walikamatwa na kupelekwa katika uwanja wa michezo wa Kasarani na baadaye walirudishwa makwao.

Matatizo ya kisiasa sana sana huhusiana na sheria za uhamiaji. Hizi humhitaji mhamiaji awe na pasi ya kusafiria, viza ya kuingia nchi anayotaka kwenda na kitambulisho cha nchi anayohamia kama amenunua uraia wa nchi hiyo. Katika nchi nyingi, mtu hata hutakiwa kujaza fomu inayokuhitaji useme sababu ya kwenda nchi hiyo, mahali maalum unakoenda na muda utakaokaa huko. Sheria nyingine za uhamiaji hutegemea mahitaji ya nchi mbalimbali.

Uhamaji na uhamiaji nao una manufaa yake. Manufaa hayo hutokana pia na mambo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Ikiwa mhamiaji amefanikiwa katika mambo yaliyompeleka kule alikohamia, yawe ni ya kijamii, kiuchumi au ni ya kisiasa, atakuwa amepata manufaa ya uhamiaji. Hayo ni baadhi ya mambo yanayojitokeza katika suala la uhamaji na uhamiaji.

Suala hili limeshughulikiwa kwa undani na waandishi wengi lakini halijashughulikiwa katika fasihi ya Kiswahili. Kwa hivyo, linapojitokeza katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, tunapata nafasi ya kulihakiki kifasihi. Mambo ya uhamaji na uhamiaji ndiyo yaliyoitawala riwaya nzima. Haya yanatokea kupitia kwa mwandishi mwenyewe na kwa hivyo huleta uhalisia wa mambo. Mambo anayoyapitia ni ya kweli na ni mambo ambayo watu hupitia wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji. Hivyo basi, uhakiki wa kazi hii utaziba pengo lililoko kuhusiana na suala la uhamaji na uhamiaji kwani haya ni maudhui mapya katika uhakiki wa kifasihi.

Suala la uhamaji na uhamiaji limejitokeza sana katika tawasifu hii ya *Mbali na Nyumbani*. Mhusika mkuu ambaye ndiye mwandishi wa riwaya hii, amenuia kukisaka ikipendacho roho ambacho ni elimu. Adam Shafi anatoka nyumbani kwao Zanzibar akiwa amesukumwa na kiu ya kupata elimu zaidi. Anatoroka nyumbani bila ya kuwaaga au kuwaarifu wazazi wake na hata walimu wake wa Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa.

Mwandishi anaandika kisa hiki baada ya miaka arubaini na mitatu lakini safari hii ndefu anayoifanya anapotoroka kwao nyumbani anaifanya akiwa kijana wa miaka ishirini tu. Akiwa katika safari yake ndefu ya kwenda kutafuta elimu, anapata visingiti vingi njiani. Ukosefu wa pesa na shida nyingine anazokumbana nazo, vinafanya maisha yake yawe ya uhamaji bila ya yeye kukusudia. Kwa mfano, anapotoka kwao Zanzibar, haendi moja kwa moja mpaka huko ng'ambo anakouia kupata elimu zaidi lakini anahamia Bungoma, Kampala, Khartoum, Kairo na

hata baada ya kurudi nyumbani Zanzibar, hakai bali anajipata Ujerumani kwa ufadhili wa kisiasa. Huko Ujerumani, anasoma, anahitimu na kurudi nyumbani kuendelea na maisha yake. Kwa hivyo maisha yake yanakuwa ya mtu asiyetulia mahali pamoja bali ni ya kuhamahama.

Kwa kifupi, kazi yetu inaangalia mambo yafuatayo katika riwaya ya kitawasifu ya *Mbali na Nyumbani*. Mambo yenyewe ni: aina za uhamaji na uhamiaji, sababu zake, manufaa ya uhamaji na uhamiaji na matatizo yanayoandamana na wahusika na jinsi wanavyojaribu kuyatatua.

### **1.1 TATIZO LA UTAFITI**

Uhamaji na uhamiaji ni suala ambalo limekumba nchi nyingi ulimwenguni hasa nchi za bara la Afrika kutokana na shida za kisiasa. Uongozi mbaya, mashindano ya uongozi, mizozo ya kikabila na ya kidini huzusha mapigano katika nchi husika. Mapigano haya ndiyo husababisha uhamaji wa raia wanaotoroka makwao na kuwa wakimbizi waliohamia nchi jirani wakitafuta hifadhi. Mfano mzuri wa uongozi mbaya ni wa nchi ya Somalia. Kushindwa kwa viongozi wake kuudhibiti uongozi wa nchi hiyo kulisababisha ukosefu wa amani na usalama nchini humo. Hii ilipelekea wananchi wake kuhama na kuhamia nchi jirani kama vile, Uganda, Tanzania, Kenya na nyinginezo. Hali hii ya uhamaji na uhamiaji imewasababishia matatizo wahamaji na nchi zinazowapa hifadhi. Kenya kwa mfano imekumbwa na ukosefu wa usalama kwa ajili ya suala hilo. Wakimbizi kutoka Somalia wamekuwa tishio kubwa kwa usalama wa nchi kwa sababu kundi la wanaojiita Al-Shabaab kutoka Somalia hujiingiza nchini kwa kujifanya wakimbizi na kisha kuanza kuendeleza ugaidi.

Matatizo yanayowakumba wahamaji na nchi wanazohamia ndiyo yaliyotufanya tufikirie kushughulikia suala hili tata la uhamaji na uhamiaji. Kwa hivyo utafiti wetu pia unanua kuangalia maudhui yanayohusiana na suala hili la uhamaji na uhamiaji, kujadili aina za uhamaji

na uhamiaji katika riwaya ya kitawasifu ya *Mbali na Nyumbani*, kuchunguza sababu za uhamaji na uhamiaji, kutathmini manufaa yanayotokana nao na kueleza kwa kina matatizo yanayowakumba wahusika katika riwaya hii na jinsi wanavyoyatatua.

## **1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza suala la uhamaji na uhamiaji katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* kwa mtazamo wa nadharia ya uhalisia kwa madhumuni yafuatayo:

- i. Kujadili aina za uhamaji na uhamiaji.
- ii. Kufafanua sababu za uhamaji na uhamiaji.
- iii. Kuchunguza manufaa yanayotokana na uhamaji na uhamiaji.
- iv. Kueleza kwa kina matatizo yanayowakumba wahusika katika riwaya hii.
- v. Kutathmini jinsi wahusika wanavyojaribu kusuluhisha matatizo yanayowakumba.

## **1.3 NADHARIA TETE**

1. Kuna aina mbili za uhamaji na uhamiaji: Uhamaji na uhamiaji wa hiari na wa lazima.
2. Uhamaji na uhamiaji huchochewa na ari ya kutaka kujienedeleza kimaisha.
3. Uhamaji na uhamiaji una manufaa.
4. Uhamaji na uhamiaji huandamana na matatizo mbalimbali.
5. Wahusika hujaribu kusuluhisha matatizo yanayowakumba.

#### **1.4 SABABU ZA KUICHAGUA MADA HII**

Sababu ya kwanza iliyotufanya tuchague mada hii ni kuwa, hakuna mtu mwingine aliyeishughulikia katika lugha na fasihi ya Kiswahili. Maandishi yaliyoandikwa kuhusu mambo ya uhamaji na uhamiaji yamefanywa katika nyanja nyingine na kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hivyo, kazi yetu itawafaidi sana wasomaji wa lugha ya Kiswahili.

Sababu ya pili ni kwamba, kitabu hiki cha Adam Shafi, *Mbali na Nyumbani* ni kitabu ambacho hakijafanyiwa uhakiki mwingine wowote.

Sababu ya tatu ni kuwa unaposoma kitabu hiki, unapata kwamba suala linalokitawala kitabu kizima ni mwendo unaosababisha uhamaji na uhamiaji hata kama kipindi cha kufanya hivyo si kirefu. Hali hii inazua matatizo mengi kwa mhusika mkuu na wenzake na matatizo hayo ni yale yale yanayomkumba mtu yeyote akiwa ugenini.

Sababu ya nne inatokana na upekee wa kimaudhui kwa maana kwamba, maudhui yanayoshughulikiwa hapa ni ya kihalisia. Pia kuna upekee wa utungo kwani ni tawasifu inayotokana na ushuhudiaji, ushiriki, uwepo na uhusika wa mhusika mkuu ambaye ni mwandishi mwenyewe.

#### **1.5 UPEO NA MIPAKA**

Utafiti huu umeangazia suala la uhamaji na uhamiaji katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Hii ni kwa sababu, suala hili limejitokeza vizuri sana katika riwaya hii. Ni suala ambalo halijawahi kujadiliwa katika kazi za kifasihi. Kwa hivyo tumepata nafasi nzuri ya kulihakiki. Pia, tumeangalia maudhui mengine yanayohusiana na kazi yetu. Tunayaita maudhui mengine kwa sababu hata uhamaji na uhamiaji hujadiliwa katika sehemu ya maudhui. Walakini,

hatutajishughulisha na uchambuzi wa maudhui yote katika kitabu hiki. Pia hatutajishughulisha na masuala ya uchambuzi wa wahusika na fani kama vile lugha.

## **1.6 MSINGI WA KINADHARIA**

Utafiti huu umefanywa kwa msingi wa nadharia ya uhalisia. Nadharia hii hujikita katika utoaji wa picha halisi ya maisha ya binadamu. Kwa hivyo, mwandishi wa kazi ya kihalisia hujaribu kuandika juu ya mambo ambayo yalitendeka, yanatendeka au yanaweza kutendeka katika maisha halisi ya binadamu bali si udhanifu. Kazi ya kihalisia ni kinyume cha kazi za kilimbwende ambazo hazichori picha halisi ya maisha ya binadamu. Baadhi ya kazi zilizo na mawazo ya kilimbwende ni kama vile: *Kusadikika* (1966), *Babu Alipofufuka* (2001), *Mafamba* (2008), *Walenisi* (2003) na vinginevyo. Kazi hizi zinaongea juu ya mambo ambayo hayawezi kufanyika katika maisha ya kawaida. Yafuatayo ni maelezo ya waandishi mbalimbali kuhusu uhalisia.

Lukács (1972:13) ameeleza jinsi waandishi wa nyakati hizo walijaribu kushughulikia masuala yaliyozikumba jamii zao wakati huo. Anasema kwamba, mwana-uhalisia wa kweli ni yule aliyepata suluhisho tofauti la tatizo la kimsingi kulingana na wakati wake. Lakini wana-uhalisia wote walikuwa na kitu kimoja kilichokuwa sawa kwao wote. Hiki kilikuwa ni kuingia ndani kabisa katika shida kubwa za ulimwengu wa wakati wao na kuonyesha kwa dhati umuhimu wa uhalisia kama walivyoona.

Boyle na Swales (1986:83) wanasema kuwa fasihi inatusaidia kuelewa wazo kuwa, uhalisia ni jinsi vitu kweli vilivyo. Kwa hivyo, mwandishi wa kazi ya uhalisia akizingatia wazo hilo, inampasa azungumzie vitu au mambo jinsi yalivyo katika jamii yake. Waandishi hawa (khj:107) wanasema kuwa mwandishi Proust, wanayemrejelea alitaka kuandika juu ya kile kingeonyesha umuhimu wa nafsi na aliyoyapitia. Maoni haya yanaingiliana na tawasifu ya *Mbali na Nyumbani*

kwani inaongea juu ya mwandishi na aliyoyapitia katika safari yake ndefu iliyosababisha maisha ya kuhamahama. Wananendelea kusema (khj:110) kwamba, uhalisia umenuiwa kuwa kama thibitisho la ukweli.

Mbatiah (2001:92) anasema kuwa, uhalisia ni mkondo wa uandishi unaohusishwa hasa na utanzu wa riwaya. Anasema kuwa ni tapo la uandishi uliozuka Ulaya katika karne ya kumi na nane na kusambaa katika mataifa mengine ya ulimwengu. Anaendelea kusema kuwa wasanii wa kiuhalisia walijishughulisha kuutafuta na kuubainisha ukweli wa maisha. Waliamini kuwa ukweli huo uliweza kupatikana katika maisha ya kila siku ya mwanadamu. Hivyo basi, walijikita katika mazingira halisi ya kijamii na kujaribu kuyasawiri kama yalivyo bila kupotosha wala kutia chumvi.

Wamitilia (2002:114) anasema kwamba, uhalisia una historia ndefu na kama Wafula na Njogu walivyosema, hata yeye anasema kuwa uhalisia ulizuka kama vuguvugu la kupinga mtazamo wa ulimbwende. Anakubaliana na Mbatiah kuwa, uhalisia kama tapo la uandishi unasisitiza usawiri wa mambo au maisha katika fasihi kama yalivyo kila siku. Anasema kuwa George Lukács, mfuasi wa Karl Marx ni mmoja wa wataalamu wanaohusishwa na nadharia hii na mchango wao umekuwa na faida nyingi sana katika mkondo huu. Wanaosisitiza mkondo huu huamini kwamba, yale yanayozungumziwa katika maandishi fulani sharti yaweze kuthibitika katika jamii ya kweli.

Wamitila anaendelea kusema kuwa, Hegel ni mwanafalsafa ambaye pia anachukuliwa kama mhimili wa tapo la uhalisia. Anasema kwamba Hegel katika kitabu chake *Aesthetik* ametumia msamiati uhalisia kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inawakilisha jamii ambayo wahusika waliomo wanafanya mambo kulingana na wanavyosukumwa na hali iliyomo. Wamitila

anasisitiza ushabihikweli katika tapo la uhalisia unaomaanisha kuwa, kazi yoyote inayoandikwa katika misingi ya uhalisia ni lazima ikaribiane na kuelezea ukweli katika jamii inayohusika.

Pia uhalisia hutofautiana kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mfano, kwa maoni yetu, hii ina maana kuwa, mambo yale yaliyochukuliwa kuwa ya kweli zamani yanaweza kutokuwa ya ukweli sasa. Jambo jingine kuhusu uhalisia ni kwamba, uhalisia hutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Hii pia ni kweli kwetu kwani mambo yale yanayoweza kuwa ya kweli hapa, yaweza kutoaminika kwingine. Mbali na hayo, fasihi ya mkondo wa uhalisia yafaa kuaminika na kusema ukweli kwa kuonyesha mazingira halisi. Maelezo hayo yanaoana na wazo kwamba, fasihi ni kioo cha jamii.

Wafula na Njogu (2007:61) wanasema kuwa, uhalisia ulianzia nchi za Ulaya katika karne ya kumi na tisa na kuenea katika nchi nyingine za ulimwengu kutokana na mapinduzi ya kiviwanda. Mapinduzi haya yalisababisha kuzuka kwa mambo mapya katika nyanja mbalimbali za maisha. Mojawapo ya mambo hayo ni upanuzi wa miji. Matatizo yaliyotokana na mambo hayo ndiyo yaliyowafanya waandishi wengi kuudhihaki ulimbwende na kuanza kuandika juu ya hali halisi ya maisha ya jamii. Kwa hivyo, wasanii hawa walianza kuangazia matatizo yaliyozikumba jamii zao hivyo basi kuendeleza tapo la uhalisia.

Waandishi hawa, Wafula na Njogu wanaendelea kusema kuwa, uhalisia wa kifasihi unaashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uhakika wa maisha. Maana hii ndiyo iliyotumiwa huko Ufaransa na waandishi kama vile Flaubert mwaka wa 1850 kuelezea kazi ya sanaa inayoonyesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo.

TUKI (2010:724) inasema kuwa uhalisia ni kitu chenye uhalisi, kuwezekana na cha kweli. Tunaunga mkono kauli hii kwa sababu, ikiwa kazi ya fasihi itachukuliwa kuwa ya uhalisia,

lazima yanayosimuliwa yawe ni mambo yanayoweza kupatikana katika jamii ya kweli. Kwa hivyo, kwetu uhalisia ni tapo la kifasihi linalosisitiza kwamba, yanayozungumziwa katika maandishi yoyote sharti yakubalike katika maisha ya jamii ya kweli.

*Microsoft Encarta Online Encyclopedia (2000)* inasema kuwa, uhalisia hujishughulisha moja kwa moja na kile kinachotekwa na akili. Inaendelea kusema kuwa, fasihi ya uhalisia ilibuniwa Ulaya na Marekani mnamo mwaka wa 1840 na kuendelea. Inaendelea kusema kuwa, uhalisia ulianza Ufaransa katika riwaya za Gustave Flaubert na hadithi fupi za Guy de Maupassaut. Katika Urusi, inawakilishwa katika tamthilia na hadithi fupi za Anton Chekhov. Mwandishi wa riwaya, George Eliot alianzisha uhalisia Uingereza nao Mark Twain na William Dean Howells wakawa waasisi wa uhalisia Marekani. Pia inasema kuwa mwandishi Mwingereza –Mmarekani, Henry James alikuwa mmoja wa wana-uhalisia maarufu sana na alipata mvuto wake kutoka kwa washauri wake, Eliot na Howells.

Josh Rahn, katika *Online Literature (2011)* naye anasema kuwa, mwanzo wa kutumia mtindo wa uandishi wa kiuhalisia ulitokana na Honore`de Balzac, mwandishi wa riwaya na tamthilia kutoka Ufaransa (1799-1850). Anaendelea kusema kwamba, uhalisia katika fasihi sana sana unahusishwa na mwamko wa kimaandishi uliotokea Ufaransa katika karne ya 19. Aina hii ya uandishi inahusishwa mno na mwandishi wa riwaya, Flaubert Gustave (1821-1880) kutoka Ufaransa. Anachukuliwa kuwa mmoja wa mihimili ya uhalisia. Josh pia anasema kuwa Howells William Dean (1837-1920) ndiye mwasisi wa uhalisia Marekani. Vile vile ana maoni sawa na *Online Encyclopedia* kuhusu mihimili ya uhalisia katika Ulaya na Marekani. Ametaja waasisi wengine kama vile, Eliot George (1819-1880), Dostoyevsky Fyodor ( 1821-1881), James Henry (1843-1916) na Twain Mark (1835-1910). Kwa kifupi, waasisi hawa ndio mihimili ya uhalisia.

Nadharia hii ina vipengele vingi lakini sisi tumetumia vipengele vifuatavyo: kipengele cha kitamaduni, kihistoria na kisiasa. Tukirejelea kipengele cha kitamaduni, Margolis (2001) anaeleza kwamba, maoni kuwa utamaduni ni wanadamu wenyewe na walivyoviumba (kama vile: lugha, historia, kitendo na sanaa) ni halisi kama maumbile ya asili. Kwetu kipengele cha utamaduni hugusia mambo yote yanayoitambulisha jamii yoyote ile yakiwemo: mila, lugha na mengineyo.

*Wikipedia, the free encyclopedia* inasema kuwa, uhalisia wa kihistoria humhitaji mhakiki kuwa na maarifa juu ya mwana-historia aliye na fasiri ya matukio ya kihistoria. Pia inaendelea kusema kuwa historia imekuwa na manufaa sana kwa fasihi na waandishi wengi walijishughulisha na mambo ya kihistoria. Sisi tunasema kwamba, uhalisia wa kihistoria hurejelea matukio halisi katika historia ya jamii. Kuhusu uhalisia wa kisiasa, Moseley katika *Wikipedia* anasema kwamba, uhalisia wa kisiasa ni nadharia ya falsafa ya kisiasa inayojaribu kueleza na kuelekeza mahusiano ya kisiasa. Huchukulia kwamba, mamlaka ndio ama yanafaa kuwa msingi wa vitendo vya kisiasa, iwe ni katika nchi au ni katika uwanja wa kimataifa. Katika nchi, nadharia hii husisitiza kwamba, wanasiasa ndio wanaofaa kuongeza mamlaka ilhali katika uwanja wa kimataifa, nchi ndizo zinazofaa kuongeza mamlaka. Sisi tunaonelea kwamba, uhalisia wa kisiasa huongea juu ya utawala katika nchi yoyote ile na jinsi nchi mbalimbali huhusiana kisiasa. Hapa ndipo suala la ukoloni linapoingilia kwani ukoloni ni ile hali ya nchi moja kuivamia nchi nyingine na kuanza kuitawala. Kihistoria, mambo haya yote yamewahi kutokea.

Huo ndio muhtasari wa nadharia ya uhalisia na vipengele vyake tunavyotumia. Kutokana na maelezo hayo, tumeamua kutumia nadharia hii ya uhalisia kama msingi wa uhakiki wa kazi yetu. Hii ni kwa sababu masuala yaliyojitokeza katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ni ya kweli na hata mwandishi mwenyewe, Adam Shafi anasema hivyo. Kwamba anatoka nyumbani kwao

Zanzibar katika maisha ya kiuhalisia. Matatizo anayokumbana nayo katika safari yake ndefu ni ya kweli na pia huwakumba watu wengine katika jamii mbalimbali wakiwa ugenini au katika hali ya uhamiaji. Yote Adam Shafi anayoyaelezea ni ukweli mtupu kwani ameyapitia mwenyewe pamoja na wenzake.

## **1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII**

Kuna mengi yaliyoandikwa juu ya mada hii ya uhamaji na uhamiaji lakini ni katika lugha ya Kiingereza. Hakuna uhakiki wowote uliofanywa kuhusu mada hii katika lugha ya Kiswahili. Walioandika kuhusu mada hii ni pamoja na Malwyn (1960: 4) ambaye, katika tasnifu yake ya M.A ameandika juu ya *American Immigration*. Amesema kuwa kuna aina mbili za uhamiaji. Aina ya kwanza inahusu uhamiaji wa lazima. Huu unashirikisha wahamiaji kama vile wakimbizi wanaotoroka nchi zao za asili ama wanaofukuzwa nchi zao na kwenda nchi nyingine kutafuta hifadhi. Anaendelea kusema kuwa, uhamaji huu husababishwa na majanga ya kiasili kama vile mafuriko, ukame unaoendelea, mitetemeko ya ardhi na mengineyo. Pia anasema kuwa uhamaji na uhamiaji wa pili ni wa hiari. Huu nao ni ule unaohusu wahamiaji wa hiari au wanaohama makwao kwa kujiamulia wenyewe. Hawa ni pamoja na: watalii, wale wanaotafuta vivutio vya kiuchumi kama vile: wanaviwanda, wachimba madini, wafanyibiashara, wataalamu mbalimbali na wengineo. Kazi yake imeshughulikia sababu za uhamaji na uhamiaji. Kazi hii itatusaidia katika kulinganisha ikiwa sababu za uhamiaji katika kazi yake ni sawa na za uhamiaji katika kazi yetu.

Caldwell (1969:94) anaongea juu ya anasa za mijini. Anasema kuwa maisha ya mjini bila shaka huvutia mhamaji. Anavitaja vivutio vya mijini kama vile; nafasi za kazi, maisha ya mjini kubadilika na wakati, usafiri kuwa rahisi ukilinganishwa na ule wa mashambani, kupatikana kwa

umeme, matibabu na elimu. Anaendelea kusema kuwa, mji pia ni mahali pa kutoroka maingiliano na majukumu ya kijamii na mengineyo.

Hance (1970:164) katika kitabu chake, ameanisha uhamaji kwa njia mbalimbali akitumia vigezo kama vile: njia ya mwendo inayotumia vifaa (gari, treni, meli na ndege): wakati gani katika mwaka na kipindi (kuhama kwa muda au kabisa): aina ya wanaohama ikiwa ni kabila, jamii husika, na njia nyinginezo. Kazi hii itatusaidia kwa sababu hata yetu inaangalia baadhi ya masuala hayo. Kwa mfano, katika kitabu cha *Mbali na Nyumbani*, tunaona kuwa, anayehama ni mwandishi mwenyewe na wakati mwingine anahama na marafiki zake wachache. Maswali mengine ni kama vile, mhamaji anahama kutoka wapi, anahamia wapi na anatumia mwendo gani (ni meli, treni au ni nini?) na mengineyo.

Scott (1972:3) katika kitabu chake, ameeleza maana ya uhamiaji na kuangazia uhamiaji wa watu mbalimbali Marekani hasa kutoka Ulaya. Yaani vile Marekani ilihamiwa na watu kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu. Kitabu hiki kimetusaidia kupata maana ya uhamiaji na hali ya uhamiaji Marekani. Marekani kama nchi nyingi za ulimwengu, imekumbwa na changamoto zinazotokana na kuongezeka kwa idadi ya wahamiaji kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu kama vile, Asia, Uarabuni, Marekani ya Kati, Afrika na kwingineko. Baadhi yao ni wakimbizi wanaotoroka nchi zao kwa sababu ya vita na ukosefu wa usalama hasa ikikumbukwa kwamba kumekuwa na vita katika baadhi ya nchi za Uarabuni.

Amin (1974:67) katika kitabu chake pia anajadili suala la uhamaji kwa vigezo karibu sawa na Hance, isipokuwa vigezo vya Amin ni vinne ilhali vya Hance ni sita. Hii inamaanisha kuwa kuna tofauti kuhusiana na jinsi walivyovianisha vigezo hivyo. Walakini, hakuna tofauti kubwa. Kwa

hivyo, kama tulivyosema kuhusu manufaa ya kazi ya Hance, hata ya Amin itatusaidia kuelewa na kulinganisha uhamaji huu na wa kazi yetu.

Harris na Levey, (1975:137) wametoa maelezo kuhusu uhamiaji. Wamesema kuwa, uhamiaji ni kuingia kwa mtu katika nchi ngeni kwa madhumuni ya kuanzisha makazi ya kudumu. Kwa hivyo wametupa mwangaza juu ya maana ya uhamiaji.

Barnum na Sabot (1976:7) wanasema kwamba, uhamaji wa kutoka mashambani kuelekea mijini umeingiliana sana na maendeleo ya kiuchumi na ukosefu wa kazi mijini. Hali hii imeendelea kuwa hivi tangu kuisha kwa vita katika nchi zinazoendelea. Hii ni kweli kwa sababu hata katika riwaya tunayoishughulikia, suala hili la ukosefu wa kazi limejitokeza sana. Hii inadhihirika Shafi anapoongea juu ya vile wanavyopata mabango mengi yakiwa yametundikwa sehemu mbalimbali yakisema “Hakuna kazi.” Maandishi haya yamenuiwa kuwatahadharisha watu dhidi ya kuingia huko kuulizia kazi. Nchi nyingi hasa mataifa yanayoendelea yamekumbwa na changamoto hii. Ni kweli kuwa ukosefu wa kazi katika mataifa mengi umechangia pakubwa uhamaji wa watu hasa vijana kutoka maeneo ya mashambani wakihamia mijini wanakoamini kuna nafasi za kazi. Hii ni kwa sababu biashara na viwanda vingi ambavyo hutoa kazi kwa wengi hupatikana mijini.

McNeill na Adams (1978:337) katika kitabu chao, wameeleza maana ya uhamaji, shida na hasara za uhamiaji na manufaa yake. Mengi waliyojadili yametusaidia sana kwa sababu kazi yetu inahusiana sana na maelezo yao isipokuwa yetu ni ya kifasihi. Maelezo yao yanaingiliana na kazi yetu kwa njia sawa na vile maelezo ya Skeldon yanavyohusiana na kazi yetu.

White na Woods (1980) katika kitabu chao, wameeleza maana ya uhamaji na sababu zake. Wanasema kuwa uhamaji ni badiliko katika mahali pa kuishi na badiliko kama hilo hulazimisha mwendo ingawa kwa kiwango tofauti. Maandishi yao yanaingiliana sana na kazi yetu kwa

sababu yanaongea juu ya uhamaji kuwa badiliko la mahali pa kuishi linalolazimisha mwendo ingawa kwa kiasi tofauti. Mwendo huu wanaozungumzia ni sawa na ule tunaoshuhudia katika safari ndefu ya Shafi. Safari ambayo ndiyo iliyosababisha maisha ya kuhamahama kwa Shafi. Kazi hii imetusaidia kwa sababu tunajishughulisha na masuala yayo hayo.

Cernea (1993:10) katika kazi yake, ameeleza juu ya sababu za uhamaji na uhamishwaji wa ghafla usiotazamiwa. Amegusia kidogo tu kuhusu uhamaji wa mtu kujiamulia mwenyewe na kusema kuwa watu huhama mjini polepole. Kwa hivyo kazi yake nyingi ni juu ya uhamishwaji wa kighafla. Ametoa sababu za aina tatu za uhamishwaji kama vile, majanga ya kawaida kwa mfano, mafuriko, mitetemeko ya ardhi na mengineyo. Sababu ya pili amehusisha na matukio ya kisiasa kama vile, vita, mapinduzi na nyinginezo. Sababu ya tatu inahusiana na mipango ya maendeleo ya miji kwa mfano, ustawishaji wa uchumi unaosababisha ujenzi wa viwanda. Pia ameongea juu ya madhara yanayotokana na mambo hayo.

Kazi hii ya Cernea pia imetusaidia kwa sababu, ingawa kazi yetu inasisitiza sana uhamaji na uhamiaji wa hiari ambao Cernea hashughulikii, ina aina nyingine ya uhamaji na uhamiaji. Huu ni ule wa kulazimishwa na vile hali ya mambo ilivyo. Kuna wakati mwingi akina Shafi wanapojikuta wakihama lakini si kwa kupenda kwao bali ni kulazimishwa na vile hali ya mambo inavyokuwa. Cernea naye amezungumzia hali ya wahusika kuhamishwa kutokana na majanga ya kiasili. Hata hivyo, hakuna tofauti kati ya aina yetu ya pili ya uhamaji na uhamiaji na ile ya Cernea kwa sababu katika hali zote mbili, mhusika hana hiari kuhusiana na uhamaji huo.

Walibora (1996) katika tawasifu yake ameonyesha jinsi alivyohama mara mbili akiwa katika harakati za kumtafuta babake. Mara ya kwanza alihama kutoka kwao Tanga na kuhamia Mombasa alikoishi na marafiki zake kwa muda. Baadaye alihama tena akaenda Kitale alikokuwa

akiishi babake lakini alimpata akiwa ameaga dunia. Kazi hii imetusaidia kuisitiza wazo la Scott (1972) kuwa, historia ya mwanadamu ni mwendo wa daima usiotulia kama inavyojitokeza katika maisha ya Kongowea Mswahili. Lengo lake la kumtafuta babake ndilo limesababisha hali hiyo ya maisha. Ingawa amehama mara mbili, suala hili halijajitokeza sana kama lilivyo katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* kwani ndilo limetawala riwaya nzima.

Skeldon, (1997:1), ameeandika juu ya uhamaji na maendeleo. Ameeleza maana ya uhamaji na faida zinazotokana na uhamaji huo. Kuhusu uhamaji, anasema kuwa unaashiria kuhama katika mahali pa kuishi kutoka eneo moja hadi jingine. Kazi hii imetusaidia kupata sio tu maana ya uhamaji bali pia sababu zinazochangia uhamaji na uhamiaji, maendeleo yakiwa mojawapo. Vile vile, amezungumzia manufaa ya uhamaji na uhamiaji ambayo pia tunashughulikia. Maendeleo kama dhana, inaweza kuangaliwa kwa mikabala mbalimbali. Kwa mfano, maendeleo ya kujiendeleza kibinafsi hatimaye huchangia maendeleo ya nchi na jamii kwa jumla. Maandishi ya Skeldon ni muhimu katika kazi yetu kwa vile yanatuwezesha kuangalia sababu zilizomchochea Shafi kuhama ambayo ni maendeleo ya kibinafsi. Haya ni maendeleo yanayofungamana na maendeleo ya taifa lake hasa ikikumbukwa kwamba alikuja kuwa mwandishi maarufu sio nchini mwake tu, bali kote Afrika Mashariki.

Odhiambo, (2003:1), ameeandika tasnifu ya M.A. juu ya *African Immigration Policies: The case of Kenya, 1906 – 2000*. Katika tasnifu hii amejaribu kuonyesha hali ambazo zimeelekeza sera za Kenya za uhamiaji baada ya uhuru, lakini msisitizo wake wote uko kwa wakati wa baada ya 1963. Kazi hii imetusaidia kuelewa sababu zinazomfanya Shafi na wengine kupata shida za kuingia nchi ngeni. Sababu hizo zinahusiana na sheria za uhamiaji ambazo zinasisitiza umuhimu wa mhamiaji kuwa na pasi ya kusafiria na viza ya kumruhusu kuingia nchi anayotaka kwenda.

Kiruthu, Kapiyo na Kimori (2011:153) wameelezea jinsi wazalendo wengi barani Afrika walivyolazimika kutoroka nchi zao kwa kuhofia maisha yao. Walienda kutafuta hifadhi Afrika kote hasa katika nchi kama vile: Zimbabwe, Zambia, Angola, Kenya na Tanzania. Hii ilitokana na hali ya hatari ilivyokuwa nchini mwao. Hali ilikuwa mbaya kiasi kwamba, waliotiwa mbaroni waliwekwa kizuizini kwa muda mrefu kama vile Nelson Mandela wa Afrika Kusini. Baadhi ya waliowekwa kizuizini nchini Kenya ni pamoja na hayati mzee Jomo Kenyatta na mashujaa wenzake waliokuwa wamefungiwa Kapenguria. Wazalendo wengine hata waliuawa. Mifano ya wazalendo waliouawa ni, Steve Biko kutoka Afrika Kusini, Dedan Kimathi kutoka Kenya na wengineo. Maelezo haya yanaoana vizuri na hamasa za kisiasa ambazo Shafi anahusisha na Mtaa wa Zamalek huko Kairo. Ni maelezo muhimu kwani yanazungumzia shida wazalendo walizopitia walipokuwa wakipigania uhuru wa nchi zao kiasi cha kuwa wakimbizi na pia wahamiaji katika nchi nyingine. Huu wote ni uhalisia wa kihistoria na kisiasa.

*Wikipedia, the free encyclopedia* imetoa maana ya uhamaji na kusema kuwa, uhamaji wa binadamu ni mwendo wa watu kutoka mahali pamoja na kwenda mahali pengine kwa nia ya kukaa huko. Mwendo ni wa masafa marefu na kutoka nchi moja hadi nyingine, lakini hata uhamaji wa ndani ya nchi unawezekana. Inasema kuwa uhamaji waweza kuwa wa mtu binafsi, familia au wa makundi makubwa. Uhamaji wa hiari na wa lazima umekuwa ukiendelea nchini na nje. Uhamaji wa lazima hutokana na biashara ya utumwa na chuki ya kikabila inayosababisha mauaji. Kuhusu sababu za uhamaji, imetaja elimu kama kichocheo kikubwa kwa wengi. Kingine ni kustaafu kwa watu katika mataifa tajiri wakihamia katika mataifa yasio tajiri bora hali ya anga huko ni nzuri. Imetoa mfano wa raia wa Uingereza waliostaafu wakihamia Uhispania ama Italia nk. Vichocheo visivyo vya kiuchumi ni kama vile, mateso ya kidini, ukandamizaji, mauaji ya kikabila na hatari za vita. Uhamaji mwingine ni wa kibinafsi unaosababishwa na haja ya

kuungana kwa familia zilizokuwa zimetengana ama kuoana kwa watu kutoka mataifa tofauti. Pia imeongea juu ya uhamaji unaotokana na sababu za kiuchumi hasa kupata ajira, bora gharama isiwe kubwa. Haya ni baadhi ya maelezo ya waandishi mbalimbali kuhusu suala la uhamaji na uhamiaji.

## **1.8 NJIA ZA UTAFITI**

Tumefanya utafiti wetu kwa kusoma tasnifu na vitabu vilivyoandikwa na waandishi mbalimbali maktabani kuhusu mada yetu juu ya uhamaji na uhamiaji. Vingine vimetusaidia kufafanulia nadharia ya uhalisia ambayo ndiyo tumetumia katika kazi yetu. Hii ni kwa sababu, ukweli wa mambo ambao unasisitizwa na nadharia hii ndio umejitokeza katika tawasifu ya *Mbali na Nyumbani*. Ujumbe mwingine tumepata kutokana na matangazo ya runinga kuhusu vita hasa vya wenyewe kwa wenyewe na matokeo yake. Vita vimetokea katika nchi mbalimbali hasa za Uarabuni na hivi majuzi katika Sudan ya Kusini. Mojawapo ya matokeo ya vita hivyo ikiwa ni uhamaji na uhamiaji wa raia wanaotoroka nchi hizo na kwenda kuhamia nchi jirani kama wakimbizi. Pia, tumetumia mtandao kutupa mwangaza kuhusu dhana ya uhamaji na uhamiaji na nadharia ya uhalisia na tumefaidika sana.

## **1.9 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumeshughulikia masuala ya kimsingi yanayohusiana na utafiti huu. Haya ni pamoja na utangulizi wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada hii, upeo na mipaka, msingi wa nadharia, yaliyoandikwa juu ya mada hii na mbinu za utafiti.

## **SURA YA PILI**

### **MAUDHUI YANAYOHUSIANA NA SUALA LA UHAMAJI NA UHAMIAJI KATIKA RIWAYA YA *MBALI NA NYUMBANI*.**

#### **2.0 UTANGULIZI**

Katika sehemu hii, tumejaribu kuonyesha ufafanuzi wa waandishi wengine kuhusu dhana ya uhamaji na uhamiaji. Pia tumeshughulikia maudhui ambayo yanahusiana na suala la uhamaji na uhamiaji katika riwaya husika. Hii ni kwa sababu, maudhui hayo yanachangia katika kuboresha au kufanya maisha ya wahusika kuwa magumu wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji.

#### **2.1 DHANA YA UHAMAJI NA UHAMIAJI**

Uhamaji na uhamiaji unahusu mambo halisi yanayofanyika katika nchi mbalimbali ulimwenguni. Nadharia ya uhalisia tunayoitumia katika kazi hii inaoana vizuri na suala la uhamaji na uhamiaji. Ufuatao ni ufafanuzi zaidi kuhusu uhamaji na uhamiaji kulingana na maoni ya waandishi mbalimbali. Kwa mfano, Scott (1972:3) anasema kuwa, historia ya binadamu ni hadithi ya mwendo wa daima usiotulia akijitahidi kupata kitu bora zaidi. Mwendo huu anaouzungumzia unaweza kulinganishwa na ule wa Shafi unaomtoa nyumbani kwao akinuia kupata elimu Ulaya. Elimu anayoisaka ndiyo kile Scott anachozungumzia kama historia ya mwendo wa binadamu wa daima akijitahidi kupata kitu bora zaidi. Hii ni kweli kwa sababu, ingawa Shafi anasomea mafunzo ya ualimu katika Chuo kimoja huko kwao, haridhiki nayo bali anajitahidi apate elimu zaidi. Anaamini kuwa ataipata elimu hiyo Ulaya.

Harris na Levey (1975:137) wanasema kuwa, uhamiaji ni kuingia kwa mtu katika nchi ngeni kwa madhumuni ya kuanzisha makao ya kudumu. Sisi hatukubaliani na maelezo hayo kwa sababu si lazima mtu ambaye anahamia mahali au nchi nyingine aishi huko maisha yake yote. Tunasema hivyo kwa sababu kuna watu wengi ambao huhamia nchi nyingine kwa madhumuni mbalimbali lakini hawaisi huko milele. Wanaweza kuwa wamehamia huko kwa ajili ya kufanya biashara, kueneza injili, kusoma kama vile Shafi na wengine. Walakini, baada ya kutimiza malengo yao, mwishowe hurudi kwao nyumbani kama vile Shafi anavyofanya baada ya kumaliza masomo yake huko Ujerumani.

White na Woods, (1980:3) wanasema kuwa uhamiaji ni badiliko katika mahali pa kuishi. Wanaendelea kusema kwamba, badiliko kama hilo hulazimisha mwendo ingawa kwa kiwango tofauti. Kwetu, tofauti za kiwango cha mwendo ni ule umbali kutoka mahali mhusika anahama mpaka mahali anapohamia. Viwango au umbali huu hutegemea ikiwa uhamaji na uhamiaji ni kutoka sehemu moja hadi nyingine katika nchi hiyo hiyo, ikiwa ni kutoka nchi moja hadi nyingine katika bara lilo hilo au ni kutoka bara moja hadi nyingine.

Kwanza kabla ya kujadili maudhui hayo yanayohusiana na uhamaji na uhamiaji katika riwaya hii, tumeangalia maana ya neno maudhui. Njogu na Chimerah (1999:21) wanasema kuwa, “maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi, iwe riwaya, tamthilia, shairi au hata wimbo. Maudhui ni sehemu ya maana na huingiliana na mada.” Mbatiah (2001:43) naye anasema kuwa, maudhui ni jumla ya mawazo, fikira, dhamira na hisia zinazowasilishwa na kazi ya kifasihi. Anaendelea kusema kwamba, maudhui yanajibu swala la “nini” kazi ya fasihi inazungumzia.

Wamitila (2008:521) anasema kuwa, maudhui ni jumla ya masuala au mambo yanayoshughulikiwa katika kazi ya kifasihi. Madumulla (2009:120) naye anasema kwamba, maudhui ni mawazo, fikra na ujumbe uliomo katika kazi ya fasihi. Maoni yetu ni kwamba, maudhui ni mambo muhimu ambayo mwandishi anasisitiza katika kazi yake ya fasihi. Kazi kama za riwaya huwa na maudhui mengi au masuala muhimu ambayo mwandishi anataka kuisitiza katika kitabu chake.

Hatua yetu ya pili ni kujaribu kuchunguza maudhui mbalimbali ambayo yanahusiana na suala la uhamaji na uhamiaji kama linavyojitokeza katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* ya Adam Shafi. Maudhui hayo ni kama vile: ukarimu, watu kuwa na roho mbaya, ufisadi, tamaa ya pesa, azma, maamuzi mabaya, ukoloni na siasa. Maudhui haya yote yanazungumzia uhalisia wa mambo katika jamii zetu. Tumeyachambua kama ifuatavyo:

## **2.2 UKARIMU**

Ukarimu au mtu kuwa na roho nzuri ni jambo linalohimizwa hata na vitabu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu. Wahusika kama vile Utubora Mkulima katika Diwani ya Shaaban Robert ya *Utubora Mkulima* (1968), hujaribu kuishi vyema na watu wengine. Kulingana na matendo yake, yeye ana roho nzuri na ni kielelezo cha kuigwa na wengine. Kwa mfano, tunamwona akiamua kwenda kunadhifisha bustani ya Bimkubwa kwa sababu anamtakia furaha ambayo aliipoteza alipofiwa na jamaa zake wote. Katika ulimwengu wa sasa, watu kama Utubora ni wachache sana. Hii ni kwa sababu ya ubinafsi uliowaingia watu mpaka hakuna anayemjali mwingine. Upweke uliomkumba nyanya huyu ni mfano wa maisha wanayoishi wazee wengi siku hizi kutokana na kuachiliwa na watoto wao waliohama mashambani na kuhamia mijini ili kutafuta

kazi. Hii ni hali ya kusikitisha sana na jamii yafaa kutafuta njia za kuwatunza wazee hawa waliotufikisha pale tulipo. Tunaambiwa,

Nia ya Utubora ilikuwa si kutafuta ijara kwa Bimkubwa huyu ila alitaka kumrudisha katika hali njema na kumfariji...Utubora alikuwa na wazo kuwa wakati wote mtu anapokuwa hai lazima ajiweke tayari kwa kuhama dunia lakini wakati ule ule lazima ajali maisha yake vile vile kama kwamba ataishi duniani milele. Kwa hivi, alikuwa anajaribu kumwamsha Bimkubwa huyu ili ajali maisha yake tena. uk 48

Hata Utubora anatukumbusha mambo ya uhamaji ingawa uhamaji anaourejelea ni ule wa mtu kuhama ulimwenguni kabisa kwa njia ya kifo. Anaongea juu ya mtu kujaribu kufurahia maisha wakati yuko hai na ndiyo sababu anafanya juu chini kurejesha furaha katika maisha ya Bimkubwa huyu. Tangu afikwe na msiba huo, hajui furaha ni nini na amekataa kuhusiana na watu kwa kuwa haoni maana ya maisha.

Tukirejea tena katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, tumeanza kwa kujadili maudhui ya ukarimu. Katika riwaya hii, wahusika mbalimbali wamedhihirisha ukarimu kwa wengine na hasa kwa mwandishi na wenzake wakiwa katika hali ya uhamiaji. Ukarimu ni hulka muhimu sana katika maisha ya mwanadamu kwani huwafaidi wengine. Ukarimu ambao mwandishi na wenzake wanatendewa na watu mbalimbali umewafanya kufurahia maisha na kuwapunguzia matatizo kule wanakohamia. Mwandishi ambaye ni Adam Shafi, anapata msaada wake wa kwanza kutoka kwa rafiki yake Mohammed Nura ambaye tayari yuko London. Nura alikuwa mwanafunzi mwenzake katika Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa walichokuwa wakisomea. Msaada huo ulikuwa wa pesa kwa ajili ya safari yake ndefu ya kwenda Ulaya kupata elimu. Ni vizuri kukumbuka kwamba, safari hii ndefu ndiyo inayosababisha uhamaji na uhamiaji tunaouzungumzia. Mwingine anayemfanyia ukarimu ni Abdalla Mwinyi aliyekuwa rafiki yake

wa dhati. Huyu ndiye aliyekuwa mwandalizi mkubwa wa safari ya Shafi na ndiye aliyemwachia jukumu la kuwasaidia wadogo zake baada ya yeye kuondoka. Shafi anasema,

Urafiki wetu mimi na yeye umepindukia ile daraja ya urafiki wa kawaida na tumekuwa kama ndugu wa baba mmoja, mama mmoja. uk 11

Kwa hivyo, ukarimu huu unarahisisha safari ya Shafi kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, pesa anazotumiwa na rafiki yake Nura aliyetangulia kufika London zinaongeza akiba aliyokuwa ameweka kwa ajili ya safari yake. Msaada wa Mwinyi nao wa maandalizi ya safari unamfaa sana. Kule kwa rafiki yake Mwinyi kukubali kuachiwa jukumu la kuwasaidia wadogo zake kunampunguzia mawazo ya kisaikolojia ambayo yangemsumbua na kumnyima amani katika safari yake. Hii ingetokana na mawazo ya kukumbuka kuwa, alikuwa na jukumu la kuwasaidia wazazi wake kwani ndiye aliyekuwa kifunguamimba kwao. Mambo ya kifunguamimba kusaidia wazazi wake kwa majukumu ya nyumbani akiwa mkubwa yanaingiliana na uhalisia wa kitamaduni. Utamaduni ndio unaompa jukumu hilo.

Ukarimu mwingine anatendewa na marafiki zake wengine wawili ambao ni, Abdalla Juma Bulushi na Abdalla Juma Maharuki waliokuwa wakisoma naye skuli moja. Hawa marafiki zake wanaonyesha ukarimu wao wanapomwalika Shafi kuandamana nao katika safari yao ya kwenda Kairo kwa ufadhili wao. Shafi anasema,

Nilifurahi, moyo wangu ulichanua kama ua lililopata umande wa alfajiri. Nilijihisi kama niliyekwishafika huko Kairo. Niliona huku n'do kulala maskini ukaamka tajiri. uk 37

Wema huu anaotendewa wa kufadhiliwa safari unafufua safari iliyokuwa imekwama baada ya kurudishwa Mombasa kutoka Aden. Huko Aden, alikuwa amezuiliwa kuendelea na safari yake kwa kukosa kutoa shilingi mia sita kama dhamana ya kuingia humo. Hii ni kulingana na sheria

za mambo ya uhamiaji ya nchi hiyo. Kama marafiki hawa zake hawangefadhili safari hii, hatujui angekaa Mombasa kwa muda wa kiasi gani akingojea kupata pesa za kuendelea na safari yake. Hii ni kwa sababu alikuwa amekosa kazi. Hivyo basi, ufadhili huu unamsaidia kuendeleza safari yake kwa vile hakuwa na pesa hata kidogo. Anasema,

Sikuwa na hata senti moja mfukoni mwangu na maisha yangu yote wakati wa safari yetu hiyo yalitegemea takrima ya wenzangu wawili. uk 48

Wanapofika Nairobi kutoka Mombasa, wanaibiwa mizigo yao yote na kijana mwingine wanayesafiri naye bila kujua ni mwizi. Kwa bahati nzuri, mwenzao safarini anayelitwa Ben ndiye anayewahurumia na kuwapa pesa zinazogharamia safari yao ya kwenda Eldoret. Ukarimu huu pia unawawezesha kuendelea na safari yao. Bila msaada huo kutoka kwa Ben, safari yao ingekwama walipofika Nairobi baada ya vitu vyao kuibwa.

Huko Eldoret pia, wanashindwa kuendelea na safari yao kwa ajili ya ukosefu wa pesa uliosababishwa na kule kuibiwa kwao Nairobi. Wakiwa Eldoret, wanatendewa wema na marafiki zake Abdalla Bulushi. Hawa ni vijana wawili wa kisomali wanaowakubalia wahamie kwao kwa siku kadhaa. Shafi anasema,

Vijana hao wawili ambao, kwa muda wote tuliokaa Eldoret walikuwa ndio wenyeji wetu, walikuwa wachangamfu mno. Waliishi na sisi kama kwamba tulikuwa ni masahibu wa muda mrefu. uk 57

Licha ya kupewa malazi na wale vijana, maisha yao Eldoret yanazidi kuwa ya baraka wanapokutana na mzee Abdalla Ngazi ambaye Shafi anasema ni marehemu sasa. Kwa mzee Ngazi, milango ya nyumba yake ilikuwa wazi kwa akina Shafi wakati wowote ule. Walikuwa wakila kwake kadiri ya kutosheleza njaa yao.

Anasema,

Maisha yetu Eldoret yalikuwa na baraka tele kwani pa kula palikuwepo na pa kulala pia. uk 57

Ukarimu wanaotendewa Eldoret kwa muda wa mwezi mmoja, unayafanya maisha yao ya uhamiaji yawe mazuri na ya kufurahia kinyume na vile maisha ya watu wakiwa nchi ngeni huwa. Kama hawakukutana na wenyeji wao, wangetaabika sana kupata chakula na mahali pa kulala. Hivi viwili (chakula na malazi) ndivyo huwapa changamoto wahamiaji mara nyingi.

Kutoka Eldoret, wanaenda Bungoma ambapo wanakirimiwa na shemeji yake Abdalla Bulushi kwa muda wa wiki moja. Hapa pia ukarimu unadhihirika kwani wanapokelewa kama watoto wa nyumbani. Wema huu wa watu mbalimbali unatokana na uwenyeji na uhodari wa Abdalla Bulushi wa kuingiliana na watu. Hii inawawezesha kupewa pesa za kusafiri kwa treni mpaka Kampala.

Wanapofika Kampala, wanakutana na vijana wanaobaini kwamba, walikuwa wakisoma nao “Comorian School” huko Zanzibar. Kwa kujuana nao, muda wote wanaokaa Kampala wanakirimiwa kula na kulala bila shida yoyote. Hii pia inayafanya maisha yao huku kuwa mazuri. Wanazidi kutendewa wema wakati Shafi anapewa shilingi mia tatu na rafikiye baba yake. Msaada huu unawapa motisha ya kuendelea na safari ambayo, kwa mara nyingine ilikuwa imekwama kwa sababu ya ukosefu wa pesa. Ukarimu huu vilevile umewapa matumaini ya kuendelea na safari yao. Bila msaada huo, hawangekuwa na namna ya kuondoka Kampala ili wasonge mbele.

Wema mwingine unashuhudiwa huko mji wa Gulu ulio mpakani mwa Uganda na Sudan Kusini. Wanapozuiliwa huko kwa wiki mbili kwa sababu hawana viza ya kuingia Sudan, mzungu mmoja ambaye ni mkuu wa polisi anafadhili kukaa kwao hotelini. Kila mmoja anapewa chumba chake

cha kulala na chakula. Huu pia ni wema wa hali ya juu kwani angetaka, angeagiza warudishwe walikotoka bila mipango yoyote. Ukarimu huu pia unapunguza matatizo yao ya uhamiaji kwani hawana wasiwasi kuhusu, watakula nini au watalala wapi.

Ukarimu wa Sheikh Noor nao wadhihirika anapompa Shafi chumba cha msikitini awe akiishi humo akiwa Bungoma. Msaada huu unamsaidia kwani hana wasiwasi ya malazi akiwa katika harakati zake za kutafuta kazi ya kumwezesha kupata pesa za kuendelea na safari yake. Anaufurahia msaada huu kwa sababu hakuwa na hakika kuwa angeruhusiwa kuhamia msikitini. Hii ni kwa vile, msikiti si mahali pa kuishi bali ni mahali pa kuabudia. Kitendo hiki cha Sheikh Noor pia kinaonyesha kuwa, kweli ni mcha Mungu na tena ni mwenye utu kwa kumwonea Shafi huruma.

Shafi kukaribishwa na kijana Abdo waende wakatembe Kisumu vilevile ni ukarimu ambao anaufurahia sana. Hii ni kwa sababu, matembezi hayo yanamwondolea upweke unaoandamana na maisha ya ugenini ambako mtu huwa hajajuana na watu. Anasema kwamba, matembezi hayo yangempa nafasi ya kutoka nje ya Bungoma kwani tangu aingie humo, hakuwa ametoka nje ya mji huo. Kwa hivyo, Shafi anaona kuwa Abdo amemtendea hisani kubwa sana. Anaeleza,

Tokea siku niliyofika Bungoma sikutoka nje ya eneo la mji ule. Matembezi yangu yote yalikuwa baina ya pembe moja na pembe nyingine ya barabara kuu. Kazi yangu ilikuwa ni kuzurura tu...Ikifika usiku, nilirudi kwenye chumba changu cha msikitini nilale...kwani humo chumbani mlikuwa hata taa ya kibitari hamna...Safari ya Kisumu kwa hivyo niliifurahia sana. uk 127

Kwa mara nyingine, Kijana Abdo anamtendea Shafi wema anapomwajiri kazi ya kutayarisha madai kufuatana na hati za maombi ya usafiri zilizotoka serikalini. Asema kuwa, alifanya kazi hiyo kwa bidii na uangalifu mkubwa mpaka Abdo mwenyewe akafurahi. Kazi hiyo ikawa

inampatia pesa kidogokidogo zilizompunguzia ulitima uliokuwa umemwandama alipokuwa akizurura pale mjini bila ya hata senti moja mfukoni. Baadaye, aajiriwa kuwa kondakta wa basi moja la Abdo. Kazi hii inamsaidia kujiwekea akiba ya kuendeleza safari yake ya kwenda kuisaka elimu ng'ambo. Kijana Abdo kuwa na biashara nzuri hivyo kunatia moyo na ni mfano unaofaa kuigwa na vijana wengine hasa wale wazururao mitaani na mijini na wanaojishughulisha na uhalifu wa namna mbalimbali. Wakomeshe tabia hizo na watafute mbinu za kujiajiri wenyewe kama hakuna kazi.

Kama tulivyosema hapo awali, wema na ukarimu ni hulka ambayo mwanadamu yeyote afaa kuwa nayo ili aweze kuishi vyema na wengine. Walakini, si lazima kila wakati wageni wategeme kutendewa mema na wenyeji ilhali wao hawatarajii kurudisha wema huo. Tunasema hivyo kwa sababu, kitendo ambacho Shafi anamfanyia Abdo kinastahili kuigwa na wageni au wahamiaji wengine. Kitendo chenyewe kinatokana na kazi yake ya ukondakta. Shafi anapokutana na Shabaan rafiki yake wa zamani, wanapanga safari ya kwenda kukutana na rafiki yao mwingine huko Nakuru. Huyu rafiki yao anayekaa Nakuru ni Abdalla Bulushi. Wakutanapo Nakuru, wataweza kufanya mipango ya kuendelea na safari yao hadi Misri. Kwa sababu safari ya Shafi na mwenzake ya kwenda Nakuru ni ya ghafla, Shafi hawezi kukaa mpaka jioni ili amkabidhi Abdo, mwajiri wake pesa alizokusanya basini mwake siku hiyo. Kwa hivyo anazichukua pesa zile pamoja na kitabu cha tiketi na mkoba wa pesa na kumkabidhi Kassim, dereva wa basi lile. Shafi anasema,

Ningeliweza kuondoka na pesa zote nilizokusanya siku ile bila ya Wilson na Kassim kujua nilikwenda wapi. Lakini kufanya hivyo kungeniharibia jina. Jina langu lingenuka Bungoma nzima mahali ambapo nilipokelewa kwa huruma na kuonyeshwa ukarimu mkubwa. Sikutaka kuwa mwizi wa fadhila. uk 171

Maneno haya ya mwandishi yanaingiliana vizuri na vile hali halisi ilivyo nchini mwetu Kenya. Kenya ni mojawapo ya nchi barani Afrika ambazo zina wahamiaji wengi hasa wakimbizi. Baadhi ya wageni na wahamiaji hawa wanakuwa wezi wa fadhila kama anavyosema Shafi. Hii ni kwa sababu baadhi yao hawatii sheria za uhamiaji. Wale nao walio na vibali vya kuwaruhusu kuendeleza majukumu yaliyowaleta nchini, hawafanyi hivyo kwa amani bali wanatenda kinyume. Wengine wanaingiliana na kukubali kutumiwa na kundi katili la Al-Shabaab linaloendeleza vitendo vya kigaidi humu nchini na kwingineko. Hivi ni pamoja na: kuvuruga amani nchini, uharibifu wa mali na kusababisha vifo vya raia wasio na hatia. Wanafanya hivi kwa njia ya ulipuaji wa mabomu makanisani, katika vituo vya mabasi, majumba makubwa ya biashara na mahali pengine wanakofikiria kuna watu wengi. Mfano mzuri ni ule uvamizi wa kinyama wa jumba la kibiashara la West Gate uliosababisha vifo vya karibu watu sabini na uharibifu mwingi wa mali. Kwa hivyo, wahamiaji wote wangeiga mfano huu wa Shafi wa kutokuwa wezi wa fadhila, hakuna mwenyeji yeyote angewachukia wahamiaji kama inavyodaiwa na baadhi yao.

Ingawa safari ya kina Shafi imekumbwa na kisirani cha kurudishwa nyuma walipotoka kwa kukosa viza, wanapofika Kampala kwa mara ya pili, wanakaribishwa vizuri. Hii ni kama Shafi anavyosema.

Kwa wiki nzima tulikula fadhila za Maalim Idi. Tulikuwa tukipata huduma iliyojaa taa na unyenyekevu kutoka kwa watoto wake. Tulikodiwa teksi na tulisindikizwa na Maalim Idi mwenyewe na marafiki zake. uk 182

Makaribisho haya yanaonyesha kuwa, wahamiaji wote wangukuwa wakijuana na kukaribishwa na wenyeji wa huko wanakoenda, maisha ya uhamiaji hayangukuwa magumu vile hutokea.

Kwa mara nyingine, akina Shafi wakiwa melini kuelekea Sudan, wanabahatika kukirimiwa mikate na familia moja ya Kisudan kwa siku kadhaa. Wakati huo walikuwa wakiihitaji sana kwani hawakuwa na chakula chochote. Ukarimu huu unawapunguzia njaa ambayo ingewasumbua katika safari yao. Sio Shafi na wenzake tu wanaotendewa wema bali hata wao wanawatendea wema vijana wawili wanaokutana nao. Hawa ni Elly na Amos kutoka Kenya ambao wanawagawia kipande cha mkate. Wanawahurumia wanapogundua kuwa, walikuwa wamekaa kwa siku mbili bila kula chochote. Wafikapo Sudan, wanaonyeshwa ukarimu na mwenyeji anayewasaidia kwa ushauri na kujitolea kuwapeleka mpaka wizara ya Mambo ya Nje kwa gari lake mwenyewe. Wema huo unawaondolea shida ya kuzunguka jijini wakiwa na masanduku yao vichwani na hawajui waendako.

Wakiwa huko huko Khartoum, wakutana na Daniel, Kijana mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Khartoum. Wanapomweleza shida zao, Daniel awahurumia na kuwatendea wema kwa kuwakaribisha kwa chakula cha mchana. Shafi asema,

Tulikula mpaka matumbo yakatujaa chakula tukawa tukikitazama kwa macho tu. Nilitamani niwe na tumbo la mbuzi, nikifutike akiba tumboni ili nitakaposhikwa na njaa nikicheue na kukila tena.

uk 274

Kitendo hiki cha Daniel ni cha kutia moyo kwa sababu, ni adimu kupata watu kama hao wanaowatendea wageni wasiowajua wema. Ukarimu wa Daniel unajitokeza tena anapowatafutia mahali pa kulala hata kama ni nyumba ya udongo. Kwao, nyumba hiyo ni afadhali kuliko kulala nje ya stesheni ya treni. Wema huu unawaondoela shida ya malazi wakati wote wanapokuwa Khartoum. Wakati wa kuondoka Khartoum unapofika, Daniel anakuja kuwaaga, anawanunulia soda ya kwaheri na anawasindikiza mpaka stesheni ya reli.

Wizara ya Mambo ya Nje pia inawatendea wema kwa kuwapa kila mmoja *Gurshi* mia mbili, yaani pesa za huko Sudan. Jambo hili lingehimizwa kwani nchi nyingine zingekuwa zikifanya hivyo, wahamiaji wengi hawangukuwa wakitaabika sana. Hata kama si nyingi, zingewapunguzia mzigo wa mahitaji yao kwa kiasi. Msaada huu kina Shafi wapewa nao unawasaidia kusafiri mpaka Misri.

Ujerumani pia ni mahali ambapo wanatendewa ukarimu na kijana mmoja wa kihindi anayewapa *faranga* tisa ambazo ni pesa za huko. Pesa hizo zinawanusuru wanapohitajika kulipa kodi ya uwanja wa ndege. Kama kijana huyo hangewapa pesa hizo, wangepata shida ya kuabiri ndege katika uwanja wa ndege wa Zurich. Ukarimu na misaada wanayopewa na watu mbalimbali kule wanakopitia na kuhamia vimewawezesha kutimiza malengo yao.

### **2.3 KUTOKUWA NA ROHO YA KUSAIDIANA**

Hapo awali, tulisema kuwa, ukarimu ni hulka nzuri katika maisha ya binadamu lakini kutokuwa na roho ya kusaidiana ni tabia isiyopendeza kamwe. Tabia hii haimsaidii yeyote. Iwe ni mwenyewe au ni yule anayehitaji msaada. Kwa hivyo, si vizuri mtu kukataa kumsaidia binadamu mwenzake ikiwa ana uwezo. Kama huna uwezo, mwambie au umweleze ni kwa nini huwezi kumsaidia.

Kwa mfano, katika riwaya ya *Mwisho wa Kosa*, kuna mhusika anayeitwa Monika ambaye amerudi nyumbani kutoka masomoni Ulaya. Huko Ulaya ameiga tabia za Kizungu kuhusiana na mavazi, mwendo, fikra, kimazungumzo na mengineyo. Tabia hizi zinamfanya akosane na majirani zake. Monika hata anabishana na jirani yake Bi Ketu ambaye anamchapa Monika makofi kwa kumtukana na kumwaga uji wake akisema ni mchafu. Monika hata hawezi kumsaidia mama yake kwa njia yoyote ile. Iwe ni kazi za nyumbani au ni kifedha. Badala ya

mamake Monika kumuomba pesa, anaenda kumuomba msichana wa jirani pesa. Anafanya hivi ingawa Monika ana pesa kwani amejiriwa na hana majukumu yoyote kwao nyumbani. Kwa kifupi, tabia hizi za Monika haziwapendezi wazee wake na mwishowe zinamfanya Monika aamue kuhama nyumbani kwao na kwenda kuishi na marafiki zake.

Tabia za Monika za uchoyo, maringo, ugomvi na kwa jumla kuwa na roho mbaya hazimchori kama msichana aliyepata elimu. Elimu ya kuinufaisha hata jamii kama vile Shafi ambaye mwishowe amekuwa mwandishi wa kuifaidi jamii. Hivyo basi, jamii ingewahimiza watu wenye tabia kama hizo za kina Monika wabadilike na wawe watu wenye roho nzuri za kuwasaidia wengine wenye kuhitaji msaada wao hasa wazazi wake.

Tukirejerea riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, tunaona Shafi akijipata katika hali mbaya ambapo afisa wa uhamiaji huko Aden akatiza safari yake kwa sababu hana pesa za kuweka dhamana kama inavyohitajika. Kwa bahati nzuri, Shafi amwona daktari kutoka kwao Zanzibar na kufurahi akifikiria angemsaidia. Aliyoifikiria ni bahati haiwi bahati kwani daktari huyo hamsaidii hata baada ya Shafi kumwomba msaada. Kukosa kwake msaada wa pesa zilizohitajika kunamlazimu kurudishwa kwao tena. Hapa tunamwona daktari wa kwao akikataa kumsaidia Shafi na hamwambii sababu ya kukataa kumsaidia. Hii ndiyo ile tabia tunayoizungumzia ya baadhi ya watu kuwa na roho mbaya. Daktari huyu angempa Shafi msaada aliokuwa akimwomba, Shafi hangerudishwa kwao bali angeendelea na safari yake. Hivyo basi kitendo hiki kinamwathiri Shafi kwani kinairudisha safari yake nyuma.

Kuna watu wengine ambao huwa na tabia ya kuwazungumzia wengine kwa ukali na dharau. Kwa mfano, kuna afisa wa uhamiaji anayempokonya Shafi pasi yake ya kusafiria anaporudishwa

Mombasa kutoka Aden mpaka ampelekee pesa za kulipia safari hiyo. Shafi anaelezea hivi kumhusu,

Kijana wa Kijerumani kanisimamia mbele yangu utadhani akitaka kunila. Alikuwa kanuna... Alinizungumzia kwa jeuri, huku akinitazama kwa macho yake makali. uk 39

Watu wa aina hii humdhalilisha mtu, humtia wasiwasi na kumwacha akiumia ndani kwa ndani. Tabia kama hii humvunja mtu roho na hata kama mtu anatekeleza sheria, tunapendekeza aifanye kwa njia yenye utu na mtu ataelewa tu. Ikiwa mtu unayeongea naye hajakataa unalomwambia, kwa nini unakuwa mkali kwake kiasi cha kumkondolea macho kama vile afisa huyo anavyomfanyia Shafi?

Katika kituo cha polisi huko Gulu, pia wanakutana na askari wabaya wenye kukunja nyuso zao kama anavyosema Shafi,

Hapo, kumpokea mtu kwa mlahaka mwema ilikuwa mwiko. Lugha ya hapo ilikuwa ni ya ujuzi na vitisho. uk 87

Hii ni tabia inayoendelea kukashifiwa na wengi hata nchini Kenya na huduma ya polisi inahimizwa kuwa na mlahaka mzuri na raia. Tabia hii mbaya ya polisi ndiyo inayochangia kutoaminika kwa polisi na raia. Vilevile, hii ndiyo sababu raia hawataki kujitolea kuwaarifu polisi kuhusu uhalifu unaoedelea miongoni mwao hata kama wanajua. Uhusiano mzuri ambao serikali inahimiza baina ya polisi na raia utapatikana tu wakati polisi watakubali kubadilisha tabia hiyo waliyo nayo ya ukali na ukatili. Hii ni kwa sababu, si kila mtu aingiaye kituoni mwa polisi huwa mhalifu. Yafaa wamsikize mtu kwanza ndipo waamue ikiwa watamkondolea macho au watamzungumzia kwa heshima.

Mwingine asiye kuwa na roho nzuri ni bawabu anayelinda lango la Ubalozi wa Misri huko Khartoum. Licha ya kuukunja uso wake, ana mtazamo wa kutisha na kubabaisha. Kina Shafi wanashangazwa na mlahaka wake uliokosa ushuba kwa wageni asiowajua. Mfano mwingine wa watu wenye tabia kama hiyo ni wa yule mzungu wanayekutana naye Uganda. Mzungu huyu anamlazimisha Shafi kuvua nguo zote hata chupi na anafurahia kuuona uchi wake. Tabia kama hizi zafaa kukomeshwa kwani zinadhalilisha, zinaaibisha na huku ni kumkosea mtu heshima na ni kinyume cha haki za kibinadamu.

## **2.4 TAMAA YA PESA**

Tamaa ya pesa ni tabia inayoleta uhalisia wa kiuchumi. Hii ni tabia iliyowakumba watu wengi sana hasa nchini Kenya. Tabia hii inaweza kusababisha uovu mwingi sana hata kuua ili mtu apate pesa. Vilevile imechangia utengano katika familia. Kwa mfano, kufarakana kwa ndugu na mwingine au mzazi na mtoto wake. Kupenda pesa sana pia kumesababisha kuvunjika kwa ndoa nyingi kwa vile wanawake wengine huwaacha waume zao na kwenda kuolewa na wale walio na uwezo wa kifedha. Tamaa ya pesa katika kitabu hiki imejitokeza kuhusiana na kazi ya usafiri wa mabasi. Shafi ameajiriwa kazi ya ukondakta. Wenye mabasi hayo wanafurahia mabasi yao yakiwa yamejaa kabisa hata watu wamebanana mpaka hakuna nafasi ya kugeuka. Kwao, hiyo ni siku njema iliyo na biashara nzuri na baraka. Wenye mabasi haya na madereva wao hawajui wanahatarisha maisha ya wasafiri wote kama vile Shafi anavyosema,

Nilipata wasiwasi pale basi lilipoanza kupanda kilima. Nililisikia... Likinung'unika kupanda kilima kwa shida utadhani lingerudi nyuma wakati huohuo, litumwage tuliokuwemo ndani. Sote tulikuwa roho mkononi... Utingo na kondakta walimchochea dereva na kumjaza mori azidi kuyakanyaga mafuta, asikubali kupitwa na gari lolote... Na lile lililokuwa mbele lazima alipite na kulitimulia vumbi. uk 102

Maelezo hayo yaonyesha kuwa hata Shafi mwenyewe kama kondakta, anajua maisha yake yamo hatarini lakini hana la kufanya. Hii ni kwa sababu ni lazima afanye kazi hiyo itakayomwezesha kuweka akiba ili kuendelea na safari yake. Baadhi ya wafanyikazi wa mabasi haya hawajali maisha ya abiria wao kwani kama Shafi anavyosema, abiria aliyezubaa kidogo tu wakati wa kushuka au kupanda, alimbeba mzimanzima na kumvurumisha nje au ndani ya basi. Hii ni tabia mbaya na inaendelea kusababisha vifo vya watu wengi kwani abiria anaporushwa nje, aweza kukanyagwa na basi lili hili au gari lililo nyuma yake. Tabia hii inasababishwa na tamaa ya pesa kwani, kadiri hawa wahudumu wa magari ya umma watakavyokusanya pesa nyingi, ndivyo watakavyolipwa vizuri. Mawazo hayo ndiyo yanayochochea tabia hizo.

Tabia nyingine inayoonyesha tamaa ya pesa ni ile ya makondakta kung'ang'ania abiria. Ni tabia wanayoiita kupigia debe basi lao. Hawa huwanyang'anya mizigo abiria wanaoshuka kutoka mabasi mbalimbali. Wanafanya hivi ili wajaze magari yao haraka ndipo waende mara nyingi na mwishowe wapate malipo mazuri. Katika harakati zao za kung'ang'ania abiria, huwashikashika abiria wakijaribu kuwasukuma ili waingie katika magari yao. Baadhi ya abiria hao ni kina mama ambao ni kama mama zao. Huku ni kukosea abiria heshima na hili hutendeka sana nchini Kenya. Ni tabia ambayo huchukiza mno na ni lazima ikomeshwe.

Tamaa nyingine ya pesa inadhihirika wakati Abdo, mwenye basi hilo anapomkaripia Shafi kwa kutomlipisha nauli Mariana, mpenzi wake Abdo. Hili linashangaza kwani ni vigumu mtu kumlipisha mpenzi wake nauli. Abdo amwonya Shafi dhidi ya kumbeba Mariana tena bila kulipa. Abdo amwambia,

Hiyo iwe ndiyo mara yako ya mwanzo na ya mwisho. Ukimchukua tena lazima alipe nauli.

uk.150

Shafi pia, karibu akosane na mwajiri wake kwa kumpelekea pesa zilizopungua kiasi kama cha siku iliyotangulia. Shafi hafurahishwi na jambo hili kwa sababu, aona kuwa Abdo amekosea kwa vile biashara haiwezi kuwa sawa siku zote. Shafi anasema,

Nilijuta, siyo kwa kumchukua Mariana bila ya kumtoza nauli tu bali hata kwa kumpelekea pesa nyingi kwa biashara nzuri ya siku ile. Kwa yote hayo nilidhani nastahili shukrani ...kwa uaminifu wa kumkabidhi kitita cha pesa kwa biashara ya siku moja tu. Lakini shukrani za Abdo zilikuwa za punda, ni mashuzi tu. uk 150

Wangeendelea hivyo, tamaa ya pesa aliyokuwa nayo Abdo ingemharibia Shafi kazi na ni kazi anayoihitaji sana ili kuendelea na safari yake.

## **2.5 UFISADI**

Hii ni tabia ambayo imeenea sana katika mataifa mengi hasa nchini Kenya. Ufisadi ni uovu unaozuia maendeleo katika nchi kwa sababu hushirikisha watu wengi hasa serikalini. Olali (2008:12) katika riwaya yake, *Mafamba* amelichambua sana suala hili la ufisadi ambao anauita mafamba. Amejariibu kuelezea vile sayari ya NUKA ilivyohalalisha ufisadi chini ya uongozi wa Kiongozi Maotad mpaka ukawa sera rasmi. Hii inamaanisha kuwa, afisi za serikali, hospitali, shuleni na kila mahali, watu walihitajika kushiriki mafamba ili wapewe huduma muhimu. Ufisadi unaozungumziwa hapa haujajitokeza sana katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* kwani ufisadi umejitokeza kidogo tu. Kwa mfano, ufisadi umetajwa na Shafi kuhusiana na mtu kuhitajika kutoa hongo anapopatikana akirandaranda mjini bila kitambulisho. Hii hufanyika wakati kuna msako wa vitambulisho. Shafi anasema,

Ukitaka kutoka basi uwe na angalau shilingi ishirini mfukoni ambazo ungelimhonga askari kuukomboa uhuru wako pale atakapokukamata. uk 33

Anaendelea kusema kuwa, bila hongo ungefikishwa mahakamani na hawakutaka hilo kwa sababu lingewapotezea wakati mwingi na faini ingekuwa nyingi kuliko hizo shilingi ishirini walizokuwa wakiwaitisha. Pia mtu angekosa faini hiyo, angetumikia kifungo cha miezi kadhaa. Kwa kifupi, ufisadi huathiri maisha ya raia na sana sana wahamiaji kama Shafi ambao hawana kazi au pesa za kutoa hongo.

Ufisadi unajitokeza tena kupitia kwa Shafi anapotusimulia kuhusu maisha magumu ya makondakta. Makondakta hawa hutaabishwa na askari wa usalama barabarani kila siku kwa kusheheni abiria kuliko idadi inayotakiwa na makosa mengine. Shafi anasema kuwa ilikuwa lazima mgawane kile ulichonacho ndipo wangukuachilia uendelee na safari yako. Anasema,

Hiyo ndiyo lugha pekee waliyokuwa wakiielewa... Bila ya kuwahonga, wewe utakuwa mtu wa kupanda na kushuka kizimbani kila siku ukishitakiwa kwa kosa la kuzidisha abiria... Hata matajiri waliomiliki mabasi hawakupenda kusikia kuwa basi limekamatwa na biashara yao kusimama. Kwa hilo waliwaruhusu makondakta wao kutoa kitu kidogo. uk 139-140

Ufisadi unadhihirika pia katika mazungumzo ya akina Shafi na vijana wenzao kutoka Kenya. Wanapokutana Sudan, vijana hawa, Elly na Amos wanawaeleza jinsi walivyoingia Uganda kwa njia ya magendo. Jambo hili la wageni kuingia nchi ngeni kwa njia za magendo linatukumbusha jinsi nchi yetu imekumbwa na tatizo la wageni kuingia nchini bila kibali. Baadhi ya wageni hawa huja kuwa wahalifu wanaotekeleza vitendo vya kigaidi. Vitendo hivi huyahatarisha maisha ya wenyeji kama inavyoendelea kushuhudiwa katika sehemu mbalimbali za nchi. Haya yameshuhudiwa, Nairobi, Mombasa na sehemu nyingine za Kaskazini Mashariki. Ni vizuri kukumbuka kwamba, si wageni wote huwa wahalifu. Tunaweza kutoa mfano wa Shafi na wenzake ambao wako mbali na nyumbani wakijaribu kujiendeleza kimaisha lakini si kwa njia mbaya. Kwa hivyo, licha ya ufisadi kurudisha maendeleo ya nchi nyuma, ufisadi pia

huwawezesha wahalifu kupenya nchi ngeni na kuendeleza vitendo viovu kama vile, uuzaji wa dawa za kulevya, mauaji ya ndovo na vifaru kwa ajili ya pembe zao na mengineyo. Haya si masimuli au mambo ya kufikiria bali ni uhalisia wa mambo kama yalivyo nchini Kenya na kwingineko.

## **2.6 UKOLONI NA SIASA**

Longman (2005:1266) inasema kuwa, siasa ni mawazo na mambo yanayohusiana na utawala katika nchi. Tunaonelea kwamba, huwezi kutenganisha ukoloni na siasa lakini hatuwezi kusema kuwa siasa yote ni ukoloni. (khj. 2005:295) inasema kuwa, ukoloni ni kuingia kwa nchi ngeni katika nchi nyingine na kuanza kuitawala. Maudhui ya koloni na siasa yanaoana vizuri na vipengele vya nadharia ya historia na siasa. Ukoloni ulianza zamani na nchi nyingi za ulimwengu ikiwemo Marekani zilikuwa zimetawaliwa na nchi za Ulaya kama vile, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Ubelgiji na nyinginezo. Nchi nyingi barani Afrika pia zilikuwa zimetawaliwa na hii ni sababu mojawapo ya nchi hizi kubaki nyuma kimaendeleo. Walakini, nchi hizi zilipata uhuru wao na kuanza kujitawala tena. Baadhi yazo zilipigania uhuru wao na nyingine zilipewa tu bila ya kupigana. Waandishi wengi wa kifasihi wameshughulikia suala hili la ukoloni. Kwa mfano, Hussein (1969) katika tamthilia ya *Kinjeketile* ameelezea jinsi Watanzania walivyopigana vita vya Maji Maji dhidi ya Wajerumani walioivamia nchi yao na kuwatawala kimabavu. Watanzania walikuwa wameahidiwa maji na mganga mmoja aliyekuwa akiitwa Kinjeketile. Kinjeketile aliwapa watu maji ambayo yalikuwa alama ya umoja na ngao ya mauti. Aliyaambia makabila yaungane na yajitayarisha kupigana na Wajerumani.

Anawambia,

Baada ya kuwa kitu kimoja,...Udongo mwekundu atapigwa na atatolewa nchini...Haya ni maji - maji ya maisha. ...Mwenye kunywa na kupaka maji haya hatadhurika na chochote. Risasi itakuwa maji juu ya mwili wa mwenye kutumia dawa hii. ... Lakini kumfukuza Mzungu lazima vita. uk 15

Ingawa Watanzania walishindwa na wengi wao waliuawa kutokana na imani potovu, walikuwa na azimio la kumfukuza mkoloni na walijua kuwa vita ndiyo dawa ya kuuangamiza ukoloni. Hata kama walishindwa, kujitokeza kwao kupigana na Wajerumani kuliufanya utawala huo kulegeza kamba kwa kubadilisha mfumo wa utawala huo ili kuzuia uasi tena.

Saidi (1980:25) naye amegusia suala la ukoloni katika riwaya ya *Utengano*. Ukoloni umejitokeza kwenye kisa cha sanamu ya mashujaa wawili waliokuwa wamekatwa baadhi ya viungo vya mwili. Mwanamume amekatwa mguu na mwanamke matiti. Sanamu hii inathibitisha kuwa kulikuwa na umwagikaji wa damu uliosababishwa na vita baina ya Wakoloni na Wafrika. Hiki ni kitendo cha kikatili na chaonyesha ukosefu wa utu.

Mazrui (1981) pia ameshughulikia suala lilo hilo la ukoloni. Ingawa anayehusika hapa (Delamon) si mtawala mwenyewe bali ni mlowezi, lakini wote washirikiana kuwadhulumu na kuwanyonya Wafrika. Tamthilia hii ya *Kilio cha Haki* ni juu ya mapambano baina ya wafanyakazi watawaliwa na wakoloni walioivamia nchi yao na kuwatawala. Anwani ya tamthilia hii inaelezea vile wafanyakazi wamejitolea kupambana na dhuluma na unyonyaji unaosababishwa na ukoloni. Utawala huu hata hauzingatii haki na sheria bali unalinda masilahi ya wakoloni.

Ndiposa Dewe anasema,

Hiyo ndiyo sheria ya kibeberu. Haikuwekwa kulinda au kutekeleza haki. La! Imewekwa kuwalinda wanyonyaji. Kulinda rasilimali yao...Sheria ya mwenye nguvu mpishe. uk 3

Katika mapambano hayo wafanyakazi waongozwa na mwanamke jasiri (Lanina) aliyejikomboa kimawazo. Lanina anafaulu katika kuwazindua wafanyakazi wenzake wapambane na udhalimu na watetee haki zao. Mapambano haya yanaleta mwamko wa kisiasa ambao ndio mwanzo wa matayarisho ya vita vilivyopelekea kuuawa kwa Delamon na vibaraka wake na baadaye kuikomboa nchi nzima kutokana na dhuluma na unyonyaji wa kikoloni. Huu wote ni uhalisia wa kihistoria na kisiasa na unaonyesha kuwa ukoloni haungeangamizwa na kitu kingine ila kutumia nguvu kwa njia ya vita.

Katika kitabu hiki cha *Mbali na Nyumbani*, maudhui ya ukoloni yanajitokeza kwanza wakati Shafi yuko katika harakati za kuitafuta viza ya kuingia Sudan. Ni wakati huu anapoelekezwa kwa ofisi ya mzungu mmoja Mwingereza. Afikapo ofisini humu, anaambiwa na mzungu huyo akae chini. Shafi anapojaribu kukaa, anaanguka kwa kushindwa kujizuia kwani mzungu akivuta kiti kwa nyuma Shafi akiwa katika hali ya kukaa. Hiki ni kitendo kimojawapo cha vitendo vya dharau ambavyo waafrika walikuwa wakitendewa na wakoloni.

Kisa kingine kinachodhihirisha mambo ya ukoloni ni kile cha Shafi kuulizwa kabila lake. Anapojibu kwamba yeye ni Mzanzibari, mzungu anasisitiza kwamba Shafi ni Mkikuyu. Anamwambia,

Wewe ni Kikuyu na tutarejesha wewe Kenya kwenye *Reserve*. uk 212

Mwandishi anaendelea kueleza kuwa,

Ulikuwa wakati wa hali ya hatari nchini Kenya. Wakati huo wakikuyu walikuwa wakiendesha mapambano ya kutumia silaha dhidi ya wakoloni wa Kiingereza, wakiongozwa na umoja wao wa Mau Mau. Walikuwa wakisakwa kama manunda wala watu. Walikuwa hawaruhusiwi kuingia Uganda na Mkikuyu aliyethubutu kufanya hivyo alikamatwa na alirudishwa Kenya. uk 212

Upeo wa dharau ya ukoloni wafika wakati Shafi anaagizwa avue nguo zote hata chupi. Asema,

Mzungu alinitazama vile nilivyokuwa uchi. Alitabasamu na kufurahi kama aliyeona mnyama katika moja ya bustani za wanyama zilizokuwepo kwao. Uchi wangu ulimfurahisha. uk 214

Hiki ni kitendo cha kudhalilisha na kushusha hadhi ya binadamu mwenzako. Kinathibitisha vile wakoloni walivyokuwa wamekosa utu na kitendo cha aina hii humsababishia mhusika mateso ya kisaikolojia. Kudunishwa huku humfanya mhusika ajione kama hana thamani yoyote.

Mambo ya siasa kuhusiana na ukoloni yanaendelea kudhihirika katika ofisi ya Ubalozi wa Ghana nchini Sudan. Mwenyeji wao anawahamasisha kuhusu siasa. Anawaeleza juu ya umuhimu wa waafrika kuungana na kuwa kitu kimoja katika vita vya kujikomboa na kuikata minyororo ya kikoloni. Wanapofika Kairo, hamasa za kisiasa zinaendelea na wanajipata wakihimizwa kushiriki katika siasa ya kupigania uhuru wa nchi zao. Hili ni kinyume na lengo lao la kwenda Misri ambalo lilikuwa kupata elimu. Wanapata kwamba, vyama vya wapigania uhuru wa Afrika kutoka nchi mbalimbali vimejikusanya pamoja ndani ya nyumba moja nambari kumi na tano. Ndani ya nyumba hiyo, kila chama cha kupigania uhuru kilikuwa na ofisi yake. Kadiri wanavyozidi kuhamasishwa kisiasa katika nyumba nambari kumi na tano, ndivyo udugu na upendo miongoni mwao wote unavyojengeka. Wanaenda na kurudi kwenye ofisi ile takriban kila

siku. Hawafanyi lolote isipokuwa kusoma magazeti au kupigwa msasa wa kisiasa ili watambue umuhimu wa waafrika kuwa huru na kujitawala wenyewe.

Huko huko Misri, wanapelekwa kambi ya kijeshi kwa mafunzo na baada ya kuyamaliza, wanarudishwa makwao lakini kwa siri sana. Hii inaonyesha kuwa wakoloni wangepata kuwepo kwa kundi kama hilo la kuwang'oa mamlakani, wangepata cha mtema kuni. Ndipo Shafi anaposema,

Walitupeleka kwenye nyumba moja iliyokuwa eneo la Kariokoo. Humo tulifichwa kama wari mpaka siku ya pili tulipopelekwa melini kwa safari ya Unguja. uk 419

Shafi anazidi kueleza jinsi wanavyorudishwa nchi zao wakiwa wamevaa sura mbili. Sura ya kwanza ni ya abiria wa kawaida. Sura ya pili ni ya mpiganaji aliyehitimu na aliyewasili kuja kuikomboa nchi kutoka mikononi mwa wakoloni. Sura hii ya pili ni ya siri kubwa, siri iliyofichika katika nafsi ya kila mmoja wao. Kila mmoja alitakiwa aifiche siri hiyo, isijulikane na mtu yeyote. Hii ndiyo sababu wapiganiaji uhuru huhitaji hongera kwa sababu ya kujitolea kwao kwa kujitenga na familia zao, kujinyima raha na mambo mengine. Hii ni kinyume na vile mambo huwa kwa kawaida. Yaani, wanajeshi wanapohitimu baada ya mafunzo yao, wao na familia zao hujivunia kufuzu kwao kwa sababu sherehe hizo huhudhuriwa na watu wengi hata rais aliye amiri jeshi. Lakini kwa kina Shafi, kila kitu kimefanywa kwa siri hivyo basi kuwanyima fursa ya kuyaonea fahari mafunzo yao. Haya yote ni kwa sababu ya ukoloni.

Mambo ya siasa yanaibuka tena wakati Shafi anaenda Ujerumani kwa masomo zaidi. Wakati huo Ujerumani ilikuwa imegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu moja ilikuwa ikiitwa Ujerumani Magharibi na nyingine Ujerumani Mashariki. Hata mji mkuu wa Berlin ulikuwa vivyo hivyo. Katika ukumbi mmoja wa mikutano, Shafi asema kuwa anaona bango kubwa lililotundikwa

mbele yao. Lilikuwa limeandikwa kwa maandishi makubwa kwa lugha za Kijerumani, Kiingereza na Kifaransa. Lilisema hivi,

Atakayeitembelea Berlin ya Magharibi ni adui. uk 471

Maandishi haya yanatukumbusha miaka ya themanini, wakati wa vita vilivyokuwa vikiitwa *Cold War* au vita baridi. Hii ni kwa sababu havikuwa vita vya silaha bali ni vita vilivyoshirikisha sana sana majibizano na *propaganda*. Hii ilikuwa sawa na uvumi wa kundi fulani kujipendelea na wakati huo huo wakiukashifu upande huo mwingine. Ulimwengu ulikuwa umegawanyika katika pande mbili. Upande mmoja ulijumuisha nchi zilizounga mkono ubepari na mwingine ulijumuisha nchi zilizounga mkono ukomunisti. Upande uliounga mkono ubepari uliongozwa na Marekani ilhali ule uliounga mkono ukomunisti uliongozwa na iliyokuwa ikiitwa U.S.S.R. au nchi ya usosiolisti ya Urusi. Mazungumzo ya mkuu wa chuo hicho yaonyesha wazi kwamba, nchi hiyo haikupendelea ukoloni. Kwa mfano, tunaambiwa,

Aliisifu nchi hiyo kwa kuwa mstari wa mbele katika kupinga ubeberu na ubepari, iliyokuwa ikiunga mkono mapambano ya kupigania uhuru wa watu wa Afrika na Asia na iliyopenda sana amani ya dunia. uk 472

Kwa hivyo, kwa kumalizia tunaweza kusema kuwa, juhudi za nchi kama hizi, misimamo na kampeni za makundi mbalimbali kama vile wafilanthropisti, wamisionari na mapigano ya wazalendo ndivyo vilivyoangamiza ukoloni. Hata hivyo, hatuwezi kusahau nafasi ya Shafi na wenzake wanapojiunga na jeshi ili kushiriki katika mapigano ya kuzikomboa nchi zao.

## **2.7 MAAMUZI MABAYA**

Haya ni maamuzi yasiyofaa na hutokea wakati mtu anakata kauli haraka kuhusu jambo fulani bila kuwa mwangalifu. Wakati mwingine hutokana na ushauri mbaya wa watu wengine.

Matokeo ya maamuzi kama hayo mara nyingi hayapendezi. Katika kitabu hiki, kuna mifano kadhaa inayoonyesha maamuzi mabaya ya Shafi na wenzake. Mfano mmoja ni wakati Shafi na mwenzake Shabaan wanapoamua kurudi Nakuru kutoka Bungoma ili wakutane na mwenzao Abdalla. Wakikutana ndipo wataweza kupanga jinsi ya kuendelea na safari yao mpaka Misri. Badala ya watu wawili kurudi Nakuru, wangemngoja Abdalla atoke Nakuru ajiunge nao huko Bungoma ili waweze kupanga juu ya safari yao ya kuenda Misri. Hii ni kwa sababu, ni rahisi kifedha kwa mtu mmoja kusafiri kutoka Nakuru mpaka Bungoma kuliko wawili kutoka Bungoma na kurudi Nakuru. Kumbuka pia kwamba, wanapotoka Bungoma wakienda Nakuru wanarudi nyuma kwa sababu ni lazima wapitie Bungoma tena wakiendelea na safari yao.

Maamuzi mabaya yanafanyika tena wakati Shafi na wenzake wanne: Abdalla, Shabaan, Elly na Amos wanapewa pesa na Ubalizi wa Ghana huko Sudan. Huu ni msaada wa kuwawezesha kujikimu wakiwa ugenini. Badala ya kwenda kula katika hoteli ya kawaida inayolingana na uwezo wao wa kifedha, wanaamua kula katika hoteli ghali ya kifahari. Shafi anasema,

Tulikwisha zoea kula katika mikahawa ya malofa... Siku ile tulikuwa katika mkahawa wa malodi. Tulijitandaza juu ya viti husemi kwamba mkahawa ule ulikuwa ni mali yetu. uk 327

Uamuzi huu si wa busara kwa sababu umewafanya watumie pesa zaidi ya zile wangetumia wangekula katika mkahawa wao wa kawaida. Ikikumbukwa kwamba wana shida ya kifedha na kwa hivyo, pesa hizo wangezitemia kwa mahitaji mengine.

Kule kwa Shafi kwenda kujihusisha na kahaba wanapomaliza kula na wenzake pia ni maamuzi mabaya. Maamuzi ya kutumia vibaya pesa wanazopewa na Ubalizi wa Ghana kwa kwenda kujifurahisha na kahaba.

Anasema,

Pesa hizo zilikuwa bado zikiniwasha. Kwa hivyo magharibi ilipoingia na wenzangu kuamua kurudi nyumbani, niliwambia nimechoka kuwa kama kuku, kulala baada ya jua kutua tu... Nilitaka kuiona Khartoum baada ya jua kuchwa ili nijue ikiwa mchana ulikuwa na watu, usiku ulikuwa na nani? uk 328

Maamuzi mengine mabaya na ambayo yanaathiri maisha yake Shafi ni kule kuacha mafunzo yake ya ualimu. Huko Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa, alikuwa katika mwaka wake wa mwisho alipoamua kutoroka kwa ajili ya kwende Ulaya. Ingelikuwa vizuri kama angelikamilisha mafunzo yake ya ualimu ili kuweza kupata cheti cha mafunzo hayo. Kwa kukatiza mafunzo hayo, aishia kupoteza muda huo wote na pesa bure. Licha ya kutoroka shule, anatoroka nyumbani kwani anaenda bila kuwaarifu au kuwaaga wazazi na jamaa zake. Maelezo yafuatayo yanathibitisha hivi anaporejea nyumbani kutoka Misri.

Walionijua walishangazwa na kuniona mimi. Kila mtu alijua kuwa nilikuwa nimepotea au niliangamia kusikojulikana. uk 422

Kutoroka kwake nyumbani kunathibitishwa zaidi na maneno anayoyasema kuhusu kwenda kwake Ujerumani baadaye kwa ufadhili wa kisiasa.

Niliondoka tena Zanzibar mwezi Agosti 1961. Mara hii haikuwa kwa utoro kama ilivyokuwa mara ya kwanza nilipotoroka nyumbani nikawaacha wazazi wangu tafrani wakiwa na majonzi na wasiwasi. uk 438

Dondoo hii inaweka mambo mawili wazi. Kuondoka kwa Shafi kwao Zanzibar mara mbili. Mara ya kwanza alikuwa ametoroka nyumbani lakini mara ya pili alikuwa amewaarifu watu. Haja yetu ni hiyo sehemu inayoongea juu ya kutoroka kwake nyumbani kwani inaonyesha kuwa alienda

bila hata kuwajulisha wazazi wake. Haya ni maamuzi mabaya kwa sababu, hata ikiwa mtu ana kiu ya elimu ni vizuri kufuata utaratibu ufaao. Hii ni pamoja na kujua ni chuo gani unachoenda kusomea na ni masomo gani utafanya.

Jambo jingine linalochangia maamuzi mabaya ya Shafi ni kutokuwa na mipango mahususi kuhusu safari yake. Kwa mfano, mwanzo kabisa ana mpango wa kupitia Kuwait kama vile mwenzake Mohammed Nura ambaye aliweza kufika Uingereza. Shafi naye badala ya kushikilia mpango huo, anabadili nia yake na kukubali kuandamana na wenzake kina Abdalla na Shabaan mpaka Misri. Safari hii yao imejaa mikosi na hasa ukosefu wa pesa za kusafiria na za matumizi mengine. Shafi anafanya makosa anapoamua kuendelea na safari ndefu na mara tu wanapofika Nairobi kutoka Mombasa, wafadhili wake wanaanza kulalamikia upungufu wa pesa. Yeye mwenyewe hana pesa zozote na ni mtu anayenuia kufika Misri. Kwenda Misri kwenyewe hakukuwa katika mpango wake wa awali bali anafuata wenzake tu.

Wakiwa Sudan kuelekea Misri, anapoulizwa na mafisa wa Uhamiaji anaenda Misri kufanya nini, anasema kuwa anaenda kusoma.

Mimi kilichonileta huku ni kutafuta elimu. Nimetoka nyumbani na nia yangu ni kutafuta masomo. uk 386

Kule kubadili mpango wake aliokuwa nao akitoka nyumbani wa kwenda Uingereza na baadaye kuamua kwenda Misri kusoma ni maamuzi mabaya. Hii ndiyo sababu anakuja kujuta baada ya kurudi kwao Zanzibar kutoka Misri wanapopata mafunzo ya kijeshi badala ya elimu. Watokapo Misri, mambo hayaendi vile walivyotarajia. Walitarajia kuwa, wangepata Uhuru kwa njia ya kupigana lakini badala yake wakoloni waamua kuwe na uchaguzi. Yaani, wapatiwe uhuru kwa njia ya amani.

Ndipo Shafi anasema,

Tuliposikia mambo ya uchaguzi, sisi tuliopata mafunzo ya kijeshi tuliwauliza wakubwa zetu. Vipi tena? Mambo si yalikuwa yawe kwa mtutu wa bunduki? Tulijibiwa, la!...Sasa mambo yatakuwa kwa karatasi ya kura... Nilihisi kuwa mambo yalikuwa yamevurugika. Nilijuta nafsi yangu, nilijilaumu, nikasema, Ala! Nimesamehe kwenda kusoma nikajitolea kurudi kwetu nikadhani kuwa nimerudi kuja kuwa mpigania uhuru shujaa, sasa ninashikishwa adabu na kuambiwa nisilete ushuyui? uk 424

Anajuta lakini kama methali isemavyo, Majuto ni mjukuu huja baadaye. Anajuta kwa kukubali kujiingiza katika siasa badala ya kuendelea na mipango yake ya kupata elimu. Hakujali siasa ambayo ingemwezesha kukomboa nchi yake. Lakini sasa anapoambiwa kuwa hawapigani na tayari wamepewa mafunzo ya kijeshi, anaona kama amepoteza wakati wake bure.

## **2.8 AZMA**

Azma ni maazimio ambayo mtu huwa nayo kuhusu jambo fulani. Hii ndiyo humsukuma mtu ili kuendelea na mwishowe kuweza kutimiza malengo yake kuhusu jambo hilo. Maudhui ya azma yamejitokeza hapa na pale. Kwa mfano, Shafi anapoabiri chombo kilichonuiwa kumrudisha kwao Zanzibar lakini anagundua kuwa hakiendi Zanzibar bali ni Mombasa, anafurahi sana.

Hii inatokana na azma aliyonayo kuhusu safari yake. Anasema,

Mimi mwenyewe nilifurahi sana kuwa chombo hicho kisingelifika Zanzibar. Nilistahabu kwenda Mombasa nikakabiliane na maisha kwa namna yoyote ile kuliko kurudi Zanzibar, amabako kurudi kwangu kungelikuwa ni kitendo cha kushindwa. uk 23

Azma ambayo Shafi yuko nayo ya kuendelea na safari yake ndiyo inayomfanya avumilie shida nyingi. Akiwa Mombasa anakorudishwa, anakumbana na matatizo mengi kama vile ukosefu wa chakula na malazi lakini hafi moyo. Anasema,

Maisha yangu Mombasa kwa hivyo yalikuwa ya shida na udhia... Shida hizo, pamoja na dhiki iliyonizunguka, haikutokea hata siku moja kujiwa na mawazo ya kutaka kurudi nyumbani kwa baba na mama. uk 33

Shafi anaendelea kuonyesha azma yake kuhusu safari yake. Anapopatiwa shilingi mia tatu na rafikiye babake huko Entebe, anawaza na kuwazua kuhusu jinsi watakavyozitumia ili zivasukume katika safari yao. Anasema,

Muda wote nilikuwa katika safari yangu ya kutoka Entebe kurudi Kampala nilikuwa nikiwaza tu, njia nzima. Nilipanga na kupangua juu ya namna gani nitazisarifu shilingi mia tatu zile ili ziweze kutusongeza anagalau mpaka Khartoum. Sikuwa na mawazo ya kurudi nyuma hata kidogo ijapokuwa baba yangu na Bwana Beja walidhani nimeemewa na shida na mashaka ya ugenini na mshipa wa kurudi nyumbani umenipiga. uk 65

Wakiwa Nimule, wanapata changamoto za usafiri kwani huko huwa na ukosefu mkubwa wa magari ya kuingia Sudan. Hata hivyo, hawajali na ndiyo sababu maudhui ya azma yanajitokeza tena ambapo Shafi anasema,

... ukiwepo usafiri, usiwepo, sisi maji tulikwisha yavulia nguo, lazima tuyakoge. Kwa hivyo hata kama ungelikosekana usafiri, tungeliutwanga hata kwa miguu. Tuliamua hivyo. uk 80

Mpakani mwa Uganda na Sudan, wanashauriwa warudi hadi Kampala ili wapewe viza ya kwenda Uganda. Badala ya kufanya hivyo, Abdalla anapendekeza warudi Bungoma kwa sababu huko wanaweza kufanya maarifa ya kupata pesa. Jambo hili la kushauriwa kurudi Kampala tena

limewavunja moyo mpaka Shafi anaingiwa na wasiwasi akiona kama kwamba Abdalla ameshindwa kuendelea na safari. Katika kuongea kwao, Shafi anagundua kuwa Abdalla bado hajafa moyo. Maelezo haya yanaonyesha kuwa, wangali na azma ya kuendelea na safari yao.

Anasema,

Nilipata moyo nilipobaini kwamba Abdalla alikuwa hakuchoka wala hakuwa na mawazo ya kurudi nyumbani. Kumbe uzi ulikuwa ni ule ule. Ni kuendelea na safari tu bila ya kujali shida na mashaka yaliyo mbele yetu. uk 101

Kama wanavyosema, safari yao imejaa ukorofi na kisirani tele kwa sababu imekumbwa na shida nyingi sana. Shida hizi ni kama vile, ukosefu wa pesa, malazi, chakula na kurudishwa walipotoka miongoni mwa nyingine. Hii ndiyo sababu Shafi anasema,

Mawazo kila namna yalikuwa yakiniduru kichwani. Lakini yote hayo hayakuiteteresha imani yangu na azma yangu thabiti ya kuendelea na safari. Hivyohivyo na ukorofi wake wa kwenda hatua mbili mbele hatua moja nyuma. Niliamini kwamba siku moja nitafika tu. Penye nia pana njia... Njia yenyewe ilikuwa haipitiki kwa urahisi na aliyetaka kuipita ilimlazimu awe na moyo. uk 105

Maelezo haya yanathibitisha kuwa, Shafi na wenzake wana nyoyo za uvumilivu na azimio la kuangalia mbele tu. Hivi ndivyo vinavyowasukuma mbele na kuwafanya wasiangalie nyuma au kufa moyo.

## 2.9 HITIMISHO

Katika sura hii, tumeshughulikia maudhui mbalimbali ambayo yanahusiana na suala la uhamaji na uhamiaji. Hii ni kwa sababu, suala la uhamaji na uhamiaji ni mojawapo ya maudhui yanayojitokeza katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Maudhui hayo tuliyojadili ni pamoja na: ukarimu, watu kuwa na roho mbaya, ufnisadi, tamaa ya pesa, maamuzi mabaya, azma, ukoloni na siasa. Tumejadili maudhui haya kwa sababu yanachangia katika kuboresha au kufanya maisha ya wahusika kuwa magumu wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji.

## **SURA YA TATU**

### **AINA ZA UHAMAJI NA UHAMIAJI, SABABU NA MANUFAA YAKE**

#### **3.0 UTANGULIZI**

Aina za uhamaji na uhamiaji, sababu na manufaa yake, vyote vinarejerea mambo halisi yanayotendeka katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Uhalisia huu wa mambo ndio unaosisitizwa na nadharia tunayoitumia ya uhalisia. Tumegawa sura hii katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza, tumeangalia aina za uhamaji na uhamiaji na sababu zake. Katika sehemu ya pili, tumejaribu kutathmini manufaa yanayotokana na uhamaji na uhamiaji huo kama yanavyojitokeza katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Manufaa yenyewe yametokana na masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa.

#### **3.1.0 AINA ZA UHAMAJI NA UHAMIAJI**

Uhamaji na uhamiaji ni wa aina nyingi. Wa kwanza ni wa hiari, wa pili ni wa kulazimishwa na vile hali ya mambo ilivyo na wa tatu ni wa lazima. Katika ule wa hiari, mtu hujiamulia mwenyewe lakini wa aina ya pili, mtu hulazimika kuchukua uamuzi huo kulingana na hali ya mambo ilivyo huko anakohamia isipokuwa halazimishwi na mtu yeyote. Lakini ule wa tatu unatokea kwa lazima na ndio Cernea (1993) anaouita uhamaji na uhamishwaji wa ghafla.

Tukirejelea riwaya hii ya kitawasifu, tunaona kwamba uhamaji unaohusika sana ni ule wa hiari. Hii ni kwa sababu mwandishi (Shafi) anapoenda safari yake ndefu, anafanya hivyo kwa hiari yake mwenyewe. Ni safari ndefu kwa sababu inamchukua zaidi ya mwaka mmoja kinyume na matarajio yake.

Anasema,

Safari ambayo kwa kawaida isingelichukua zaidi ya mwezi mmoja kwa meli. Lakini safari yangu ilichukua mwaka mzima nikienda na kurudi kama mtu aliyepotea njia. uk.v

Urefu wa safari ndio unaoyafanya maisha yake na wenzake safarini kuwa ya kuhamahama. Ingawa Shafi amepanga safari ya kwenda Uingereza kupata elimu, safari yake haiwi ya moja kwa moja. Hii ni kwa sababu ya shida za pesa na sheria za mambo ya uhamiaji katika nchi mbalimbali anazoenda.

Ingawa uhamaji na uhamiaji unaodhihirika waziwazi ni wa hiari ambapo Shafi anatoka kwao Zanzibar kwa kupenda kwake, uhamaji na uhamiaji wa pili unajitokeza pia. Uhamaji huu wa pili si ule Malwyn (1960:4) anazungumzia wa mtu kuwa mkimbizi kwa kufukuzwa na kulazimishwa na majanga ya kiasili. Huu wa Shafi na wenzake ni wa kulazimishwa na hali ya mambo wanayoikuta huko waendako. Kwa hivyo wanajipata wakihamia mahali huko bila kupenda kwao.

Tumejaribu kuonyesha aina za uhamaji na uhamiaji na mahali unapotokea. Uhamaji na uhamiaji wa hiari tumeuita wa aina ya kwanza na ule wa kulazimishwa na vile hali ya mambo ilivyo tumeuita wa aina ya pili.

### **3.1.1 UHAMAJI NA UHAMIAJI WA HIARI**

Huu ni uhamaji na uhamiaji anaotokana na uamuzi wa mtu mwenyewe bila ya kushurutishwa na yeyote. Hali hii ndiyo iliyojitokeza kwa wingi katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Vilevile humpa mhusika nafasi ya kufikiria kuhusu uhamaji na uhamiaji huo. Pia tumeonyesha ni wapi uhamaji na uhamiaji huo umetokea.

### **3.1.1.1 UHAMAJI ZANZIBAR**

Mfano wa uhamaji wa hiari unapatikana mwanzoni mwa riwaya ambapo Shafi anatoka kwao nyumbani akiwa na matumaini ya kwenda ng'ambo kwa masomo zaidi. Ni dhahiri shahiri kwamba, uhamaji huu ni wa hiari. Hata juhudi anazofanya za kutafuta pesa zaonyesha kweli kuwa amehiari kutekeleza azimio lake. Kwa mfano anajitolea kufanya kazi ya dobi chuoni mwao ili aweke akiba ya kumwezesha kufaulisha hiyo safari yake. Licha ya hayo, anaacha mafunzo yake ya ualimu katika Chuo cha Seyyid Khalifa. Kule kutoiarifu hata familia yake kwaonyesha azma aliyonayo. Labda aogopa kupata pingamizi kutoka kwa wazazi wake. Anafanya haya yote kwa sababu hili ni jambo ambalo amelifikiria kwa muda mrefu na mwishowe anaamua kulitekeleza.

### **3.1.1.2 UHAMAJI MOMBASA**

Uhamaji wa hiari unashuhudiwa tena kupitia kwa Shafi. Shafi akutana na marafikize wawili huko Maskani, Mombasa. Hawa ni, Abdalla Juma Bulushi na Abdalla Juma Maharuki. Vijana hawa wawili wanapokutana naye Mombasa, wanashangaa kumwona kwa vile walifikiri alienda Uingereza kitambo. Wanapogundua kwamba hana mipango yoyote, wanamwambia ajiunge nao katika safari yao ya kwenda Misri. Wanamwambia,

Sisi, hivi unavyotuona tumetokea Unguja tumo safarini, safari ya Kairo. uk 37

Wanapomuuliza ikiwa angejiunga nao na anawambia kuwa, yeye hana pesa za safari kama hiyo, wanamwambia,

Pesa sisi tunazo wewe kama uko tayari sema tu. uk 37

Shafi anafurahia mwaliko huo unaopelekea kuhama kwake Mombasa kwa hiari.

### **3.1.1.3 UHAMIAJI BUNGOMA NA NAKURU**

Huu ni uhamaji wa hiari pia. Kuja kwao Bungoma kumetokana na ushauri waliopewa huko Nimule kwamba, warudi mpaka Kampala ambako wataweza kupata viza ya kuwawezesha kuingia Sudan. Wanapofika Bungoma, Abdalla Bulushi anaamua kwenda Nakuru kwani waonelea kuwa ingekuwa vizuri kujigawa hivyo. Wanataka kila mmoja ajaribu bahati yake mahali tofauti kwani hawataki kuandamana pamoja. Kwenda pamoja kungewafanya kukosa kazi wote kama huko waendako hakuna ajira. Wanakubaliana kwamba Abdalla Bulushi angeenda Nakuru apate mambo yakiwa mazuri, angemwita Shafi waende wakafanye kazi huko.

### **3.1.1.4 UHAMIAJI MISRI**

Baada ya kupata viza ya kuingi Misri, Shafi na wenzake wanafunga safari ya kwenda huko. Uhamiaji huu ni wa hiari kwa sababu wana lengo la kupata elimu huko. Wafikapo Misri, waelekea kwenye eneo linaloitwa Zamalek. Hili ndilo eneo lililokuwa na ofisi mbalimbali. Zamelek ni kisiwa kilichozungukwa na Mto Nile. Majina kama haya yanaleta uhalisia wa mambo kwa sababu, Mto Nile kwa mfano tumeusoma juu yake katika somo la historia na hata jiografia. Mto Nile una uhalisia wa kihistoria kwa sababu ndio uliosababisha kutawaliwa kwa nchi ya Uganda na Waingereza. Kwa vile Misri pia ilikuwa imetawaliwa na Waingereza wawa hawa, hawakutaka Uganda itawaliwe na nchi nyingine kwani ingedhibiti mto huo ulio na chanzo chake Uganda. Hili lingethiri maendeleo ya Misri kiuchumi kwa sababu Mto Nile ndio uti wa mgongo wa Misri.

### **3.1.1.5 UHAMIAJI UJERUMANI**

Uhamiaji huu vilevile ni wa hiari. Unatokea wakati Shafi atoka kwao Zanzibar kwa mara ya pili ili aende Ujerumani kwa masomo aliyokuwa na kiu nayo lakini hakuyapata. Hakuyapata kwa sababu wanapoenda Misri kwa madhumuni ya kupata elimu, wanakuta kukiwa na mwamko wa kisiasa. Kutokana na mwamko huu, wanahamasishwa kisiasa mpaka wanakubali kujiunga na mafunzo ya kijeshi. Mafunzo haya yamenuiwa kuwatayarisha kurudi nchi zao ili kushiriki katika vita vya kuzikomboa nchi hizo kutoka minyororo ya ukoloni. Huu tena ni uhalisia wa mambo kwani wakati huu nchi nyingi hasa barani Afrika zilikuwa zikipigania uhuru wao kiasi cha kumwaga damu nyingi sana na Kenya ikiwa mojawapo. Mapigano haya yanasisitizwa na Ndalu na Kitula (1989:11) katika methali isemayo, “ Amani haiji ila kwa ncha ya upanga.”

### **3.1.1.6 UHAMIAJI ZANZIBAR**

Uhamiaji huu pia ni wa hiari na unashuhudiwa baada ya Shafi kumaliza masomo yake huko Ujerumani. Ni uhamiaji wa hiari kwa sababu anarudi kwao Zanzibar akiwa amehitimu na kwa hivyo anajivunia masomo yake. Ni uamuzi mzuri kwa sababu si watu wote ambao huenda nchi za ng'ambo kusoma hurudi nchi zao tena. Wengine wakipata kazi, hutafuta uraia wa nchi hizo na kuamua kuhamia huko kabisa na hawafikirii kurejea nchi zao tena. Kinyume na hao, Shafi anarejea kwao na anafanya wajibu wake kama anavyotarajiwa na jamii na nchi yake. Uhamiaji huu kweli ameufurahia kwani anaporudi, anatulia na mwishowe anaanza kazi yake ya uandishi wa vitabu vya fasihi ya Kiswahili. Hivyo basi jamii yake inapata manufaa ya elimu yake iliyosababisha uhamaji wake kwao Zanzibar.

### **3.1.1.7 UHAMAJI NA UHAMIAJI WA ABDALLA BULUSHI NA SHAABAN SALIM**

Abdalla na Salim pia waliishi maisha ya kuhamahama kama mwenzao Shafi. Tunaambiwa kwamba walihama kwao tena baada ya kutoka Misri. Tunaarifiwa kuwa muda mfupi baada ya kutoka Kairo, walienda Cuba, Urusi na hatimaye walirejea kwao Zanzibar walikoendelea kufanya kazi ya jeshi. Uhamaji na uhamiaji wao wote baada ya kutoka Misri ni wa hiari kwani ni wao wenyewe waliojipangia na kujiamulia mambo yao. Si kama vile wanavyohamishwa kutoka Misri bila kuhusishwa katika mipango hiyo. Uhamaji na uhamiaji wao katika nchi tulizotajiwa wameuhiari wenyewe kwa vile umenuiwa kuwaendeleza kimaisha.

### **3.1.1.8 UHAMAJI NA UHAMIAJI WA NDUGUYE SHAFI**

Si Shafi na wenzake tu waliopitia maisha ya uhamaji na uhamiaji bali hata nduguye Shafi. Huyu pia anatoka kwao Zanzibar na kwenda Uingereza kusoma. Uhamaji wake vilevile ni wa hiari. Labda amefanya hivyo kwa kuvutiwa na elimu ambayo ndugu yake Shafi amepata Ulaya naye akataka kufanya vivyo hivyo. Hatujaambiwa sababu ya kuamua kwenda Uingereza kusoma lakini ni wazi hajashurutishwa na mtu yeyote. Ujumbe huo kuhusu nduguye Shafi kwenda Uingereza kusoma tunaupata Shafi anapotueleza kuhusu suti aliyoishona kwa kitambaa alichopewa na babake. Anasema,

Nilipomaliza masomo yangu na kurudi Zanzibar, suti hiyo nilimpa ndugu Saad wakati naye alipoondoka kwenda Uingereza kusoma. Nilimpa suti hiyo ili naye apate baraka za baba yetu. uk

483

### **3.1.2.0 UHAMAJI NA UHAMIAJI WA KULAZIMISHWA NA HALI YA MAMBO**

Huu ni uhamaji na uhamiaji unaosababishwa na hali ya mambo ilivyo huko mhusika anakoenda. Hakuna mtu anayemshurutisha kuhama au kuhamia huko bali hujipata akifanya hivyo bila

kupenda kwake. Kwa hivyo si uhamaji na uhamiaji wa hiari na si wa lazima ambapo mtu huhamishwa kwa sababu ya majanga ya asili na mengine. Haya yakitokea hulazimu watu kuhamishwa ili kuepukana na hatari ambayo huwa imeyakabili maisha yao. Tumetoa mifano kama ifuatavyo:

### **3.1.2.1 UHAMIAJI MOMBASA NA ELDORET**

Tumeanza na uhamiaji Mombasa. Ingawa uhamaji unaomtoa Shafi kwao Zanzibar ni wa hiari, tunamwona akihamia Mombasa kwa kulazimishwa na vile hali ya mambo ilivyo huko. Hii inatokea baada ya Shafi kukatazwa kuingia Aden na badala yake kulazimishwa kurudi kwao kwa kukosa dhamana ya shilingi mia sita. Hii ni kulingana na sheria za uhamiaji kama tulivyosema hapo mbeleni. Kwa sababu chombo kinachomrejesha hakiendi kwao Zanzibar bali kinaenda Mombasa, analazimika kuhamia Mombasa.

Uhamiaji wa kulazimishwa na jinsi mambo yalivyo unadhihirika tena vijana hawa watatu wanapofika Eldoret. Kwa kukosa pesa za kuendeleza safari yao, wamejipata wakiishi Eldoret kwa muda wa mwezi mmoja bila kutarajia. Wanakaa huko mpaka wanapopata pesa zinazohitajika katika safari yao. Hii inaonyesha wazi kwamba uhamiaji huo si wa hiari bali ni wa kulazimishwa na hali hiyo.

### **3.1.2.2 UHAMIAJI KAMPALA NA KHARTOUM**

Tukiangalia hali ya maisha Shafi na wenzake wanayopitia, tunaona jinsi wanavyotaabika. Kwa mfano, wanapoenda Kampala, wanakaa huko kwa muda kwa ukosefu wa pesa za kuwawezesha kuendelea na safari yao. Huu ni uhamiaji wa kulazimishwa na jinsi hali ya mambo ilivyo huko. Wanapofika Nimule iliyo mpakani mwa Uganda na Sudan, shida zao zaongezeka. Hii ni baada

ya polisi kuwapokonya pasi zao za kusafiria wanapogundua kuwa wanataka kwenda Sudan na hawana viza ya kuingia huko.

Uhamiaji Khartoum pia ni wa kulazimishwa na hali ya mambo ilivyo. Huku, kina Shafi wakutana na vijana wengine kutoka nchi nyingine hasa Kenya na wote wasimulia juu ya uhamiaji wao Khartoum. Wote wamekwama Khartoum kwa kuwa, kupata viza za kwenda nchi wanazotaka ni vigumu. Hii ni kwa sababu ni lazima maombi waliotuma yakubaliwe ili wapewe hiyo viza.

### **3.1.2.3 UHAMIAJI KATIKA KAMBI YA KIJESHI NA ZANZIBAR**

Uhamiaji wao Misri waishia kuwa wa kulazimishwa na hali ya mambo ilivyo wanapohamia katika kambi ya kijeshi kwa kushawishiwa. Malengo yao ya kwenda Misri ni tofauti na mawazo ya wanasiasa wanaokutana nao katika chumba wanachoambiwa ndicho kinachoshughulikia masilahi yao. Wanasiasa hawa wanawahamasisha hadi akina Shafi wanalazimika kuweka kando mipango yao ya masomo ili washughulikie uhuru wa nchi zao kwanza. Hivyo ndivyo wanavyojipata wakihamia kambi ya kijeshi kwa lengo la kupata mafunzo ya kuwaandaa kupigania uhuru wa nchi zao.

Uhamiaji mwingine unashuhudiwa tena baada ya wao kumaliza mafunzo ya kijeshi Misri. Uhamiaji huu pia si wa hiari bali ni wa kulazimishwa kwani umepangwa. Shafi anaeleza,

Tulihitimu mafunzo yetu vizuri na sasa wakati wa kurudi Zanzibar ulikuwa umefika. Ilikuwa nirudi kule kule nilikotoka. Kule nilikokukimbia nikajiingiza katika maisha ya bahati nasibu yaliyonipeleka huku na kule...Nilikwenda omo, nilikwenda tezi mwisho ilinibidi nirejee ngamani. uk 413

Kwa vile kuwa kwao wanajeshi kumetokana na hamasa za kisiasa, hata kuhama kwao Misri si kwa hiari bali kumepangwa.

### **3.2.0 SABABU ZA UHAMAJI NA UHAMIAJI**

Kuna sababu mbalimbali za uhamaji na uhamiaji kama zinavyodhihirika katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Sababu hizi ndizo zinazowasukuma wahusika kuhama mahali na kuhamia mahali kwingine. Hizi ni kama vile: kupata elimu, viza, ajira, ukosefu wa pesa, mafunzo ya kijeshi na ukombozi wa nchi zao. Sababu hizi ambazo mwandishi wa riwaya hii anazozungumzia ni zile zile zinazowakabili wahamaji na wahamiaji wengine wowote. Kwa hivyo hali halisi ya maisha inaonekana kama inavyotakiwa kuwa kulingana na nadharia ya uhalisia. Zifuatazo ni baadhi ya sababu za uhamaji na uhamiaji katika riwaya hii.

### **3.2.1 KUPATA ELIMU**

Elimu ni nguzo ya maisha. Ingawa elimu sio kila kitu, kuna mambo mengi huwezi kufanya bila elimu katika nchi nyingi. Kwa mfano nchini Kenya, katiba inakuhitaji uwe na shahada ili ukubaliwe kuwania nafasi ya urais, ugavana na nyingine nyingi. Hii imewafanya hata watu wale hawakuwa wakithamini elimu waanze kuona umuhimu wake. Labda ndiyo sababu Shafi akajitolea kwa hali na mali ili aipate. Uhamaji wa kwanza unapatikana mwanzoni mwa riwaya ambapo Shafi anatoka kwao nyumbani akiwa na matumaini ya kwenda ng'ambo kwa masomo zaidi. Ni dhahiri shahiri kwamba uhamaji huu umesababishwa na kiu ya kupata elimu. Elimu nayo huingiliana na masuala ya kijamii. Ikumbukwe kwamba elimu ni ufunguo wa maisha mazuri na licha ya kumfaidi mhusika, pia huifaidi jamii. Anasema,

Wakati huo nilikuwa safarini kwenda kuisaka elimu. uk 3

Kutokana na maneno hayo ya Shafi, tunapata kuelewa chanzo cha safari yake ndefu. Anasema kuwa alikuwa na mazoea ya kutembelea ufukwe uliokuwa karibu sana na chuo chao.

Kwa muda wa miaka mitatu niliishi katika hali hiyo na hapo ndipo ibilisi wa safari alipoanza kuniingia kidogo kidogo na mimi nikatamani kuwa abiria katika vyombo vile nilivyoviona vikiingia na kutoka. Katika hilo nilipata mshabiki mwenzangu, Mohammed Masoud Seif. uk 6

Anaendelea kusema kuwa yeye na Mohammed walikuwa maskauti katika kikosi kimoja chuoni mwao. Kwa bahati nzuri, Mohammed alikuwa amekwisha kwenda Uingereza akiwa mmoja wa maskauti hao. Anasema, kwa hivyo,

Alikuwa heshi kunisimulia juu ya maisha mazuri wanayoishi watu wa Zanzibar huko Portsmouth na fursa nyingi za masomo zinazopatikana huko Uingereza. Mimi akili yangu haikuwa katika starehe na maisha mazuri. Nilikuwa nikipenda kusoma na kila siku nilikuwa nikiwaza lini nitaingia katika chuo huko Ulaya. Basi mimi na Mohammed tulikaa na kupanga. uk 7

Aelezea jinsi walipanga kusafiri kwa jahazi mpaka Kuwait. Wakiwa Kuwait, wangepanya kazi kwa muda na wakishakusanya pesa za kutosha wangeendelea na safari yao mpaka Uingereza. Kwa kifupi, Shafi ametufahamisha asili ya safari yake. Uhamaji wake kutoka kwao Zanzibar ni wa hiari na ametujulisha umetokana na sababu gani.

Uhamaji na uhamiaji unaweza kuchochewa na mambo mengi. Kwa mfano, wakati Mohammed Masoud, rafiki yake Shafi anaugua ghafla na kuaga dunia, Shafi anabahatika kupata rafiki mwingine pia mwenye mawazo yayo hayo ya kutaka kwenda Ulaya. Huyu pia akiitwa Mohammed lakini ni Mohammed Khamisi Nura. Mohammed Khamisi vilevile alikuwa mwanafunzi mwenzake huko Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa lakini alifika Ulaya kwanza.

Kama Shafi anavyosema,

Khamisi alifanikiwa kumfanyia baba yake kiinimacho akamdanganya akazitia pesa mkononi, akaondoka kwa jahazi mpaka Kuwait akaniacha mimi na safari yangu ya hadithi. uk 9

Shafi anaiita safari yake ya hadithi kwa sababu ilikuwa imekumbwa na ukosefu wa pesa. Kinyume na babake Khamisi ambaye hata kama hakuwa tajiri, alikuwa na pesa kiasi, babake Shafi hakuwa nazo kabisa. Hii inadhihirika Shafi anaposema,

Nilimweleza baba yangu kwamba nilitaka kwenda Ulaya kusoma. Aliniuliza bei ya nauli kwa meli mpaka huko Uaya... Nilipomtajia bei hiyo baba yangu, alinywea kama aliyemwagiwa maji ya baridi. Hata mimi mwenyewe nilimwonea huruma. Angelipenda sana kunipeleka mimi mwanawe wa kwanza kwenda kusoma Ulaya lakini uwezo huo hakuwa nao. uk 7

Hii inatudhihirikia ni kwa nini Shafi akapanga safari yake ndefu kisiri ambapo anasema kuwa alitoroka nyumbani. Tunakisia kuwa, yawezekana hakutaka kuiarifu familia yake ambayo haikuwa na uwezo wa kumsaidia na kwa hivyo wangeathirika kimawazo bure. Si hilo tu bali yawezekana kuwa wangemshauri asiende safari ndefu hivyo bila pesa za kutosha. Pia kwa vile Shafi angekawia Aden kwa muda akijaribu kufanya vibarua vya kumwezesha kupata pesa za kugharamia safari yake mpaka Uingereza, labda wazazi wake wangemshauri aweke akiba kwanza.

Tukirejelea tena sababu za uhamaji, tunaona kwamba uhamaji wa Shafi kwao Zanzibar pia umechochewa sana na rafiki yake Mohammed Khamisi Nura ambaye tayari yuko Uingereza.

Shafi asema,

Kila siku zilivyokwenda ndivyo mori wa safari ulivyoziidi kunipanda. Aliyezidi kuupandisha mori huo alikuwa Mohammed Khamisi. Yeye alikuwa akiniandikia barua takriban kila mwezi... Aliniarifu juu ya kufika kwake London na kunieleza kuhusu maisha ya huko Uingereza. Nilimhusudu nikamwona kama aliyefika mwezini. uk 103

Licha ya Shafi kuhama kwao Zanzibar kwa madhumuni ya kupata elimu, tunamwona tena akihama Mombasa kwa lengo lilo hilo. Wakati huu ajiunga na wenzake wanaokwenda Misri kwa sababu hiyo hiyo. Uhamaji wa Shafi Mombasa watokana na mwaliko wa marafiki zake wawili, Abdalla Juma Bulushi na Abdalla Juma Mahatuki. Wanapokutana na Shafi Maskani, Mombasa na kugundua kuwa Shafi hakufanikiwa kwenda Ulaya kama walivyofikiria, na wanamweleza juu ya mipango waliyo nayo ya kwenda Misri. Kisha wanamwuliza ikiwa angependa kuandamana nao na Shafi anakubali. Uhamaji huu unasababisha kuhama kwake Mombasa. Kwa Shafi, uhamaji huu utamwezesha kupiga hatua mbele katika safari yake kwani alikuwa amekwama Mombasa kwa ajili ya ukosefu wa pesa. Uhamaji huu basi umetokana na uamuzi unaoingiliana na mambo ya kijamii kwa sababu safari yenyewe imenuiwa kumwezesha kupata elimu. Maelezo yafuatayo yanaonyesha wazi matarajio yao wafikapo Misri. Shafi anasema,

Katika ofisi ya chama cha wapigania uhuru wa Zanzibar ndimo mambo yetu yalikuwa yakishughulikiwa. Mambo yenyewe yalikuwa ni ya kutafutiwa masomo. Nchi yoyote ile. Ilitubidi tuende hapo kila siku ili kuulizia mambo yetu yote. uk 374

Shafi anaendelea kutufahamisha nia yao ya kwenda Misri anaposema,

Mimi kilichonileta huku ni kutafuta elimu. Nimetoka nyumbani nia yangu ni kutafuta masomo.  
uk 386

Anatoa kauli hii anapoulizwa na mtu anayeitwa Ali sababu yake ya kwenda Misri. Ali ndiye anayesimamia mambo ya kuwahamasisha vijana kisiasa ili wakubali kujiunga na kikosi cha kuuangamiza ukoloni. Shafi anazidi kutueleza vile mambo yameenda mpaka wakajipata wamebadili mawazo yao ya kuendelea na masomo na badala yake wajiunga na mafunzo ya kijeshi. Anasema,

Miezi ilikuwa inakatika mmoja mmoja lakini hakuna jibu nililolipata... Tulikwenda na kurudi kwenye ofisi ile takriban kila siku. Kazi yetu kubwa ilikuwa ama ni kusoma magazeti au kupigwa msasa wa kisiasa ili tutambue umuhimu wa waafrika kuwa huru na kujitawala wenyewe... Siku ambayo Ali alitukusanya katika ofisi yake akatushauri kujiunga na mafunzo ya kijeshi ili baadaye tukaikomboa nchi yetu, sote tulisema, Hewalla! Kwanza ukombozi na masomo baadaye. uk 387

Uhamiaji mwingine unaosababishwa na haja ya elimu unatokea wakati Shafi ahama kwao Zanzibar tena ili aende Ujerumani kwa masomo aliyokuwa na kiu nayo. Masomo haya yametokana na ufadhili wa kisiasa na kwa hivyo uhamiaji huu umesababishwa na masuala ya kisiasa. Ingawa Shafi hajiungi na vyama vya kisiasa bali anajiunga na vyama vya wafanyakazi, anaendelea kutangamana na wanasiasa. Hii ndiyo sababu wanafadhili masomo yake. Ukweli huu unadhihirika anapoambiwa na wanasiasa,

Tumeamua tukupeleke Ulaya ukasome. Tutakupeleka Ujerumani ukasomee mambo ya uchumi katika Chuo Kikuu cha Wafanya Kazi kwa muda wa miaka miwili. uk 434

Uhamaji mwingine unaosababishwa na kiu ya kupata elimu ni wa nduguye Shafi. Huyu pia anatoka kwao Zanzibar na kwenda Uingereza kusoma. Uhamaji huu pia unatokana na masuala ya kijamii kwani unahusu elimu. Baada ya kumaliza masomo yake, alirudi na kuhamia kwao tena. Shafi hata anatueleza jinsi alivyompa nduguye suti aliyoshona na kitambaa alichopewa na babake.

Anasema,

Nilipomaliza masomo yangu na kurudi Zanzibar, suti hiyo nilimpa ndugu yangu Saad wakati naye alipoondoka kwenda Uingereza kusoma. Nilimpa suti hiyo ili naye apate baraka za baba yetu. uk 483

Shafi kumpa ndugu yake suti iliyoshonwa na kitambaa alichokuwa amepewa na babake ili hata nduguye apate baraka za baba yao kunaleta uhalisia wa kitamaduni. Hii ni kwa sababu Wafrika wanaamini kwamba, mtoto akipewa baraka na wazazi wake, maisha yake huenda vizuri. Vivyo hivyo, mtoto akikosa baraka za wazazi wake mambo yake huharibika. Imani hii ya kitamaduni basi ina misingi yake katika uhalisia wa kitamaduni. Kama tulivyosema, nadharia hii husisitiza umuhimu wa wasanii wa kifasihi kujishughulisha na mambo yanayoihusu jamii yenyewe. Kwa hivyo, Shafi anapoongea juu ya kupata baraka za wazazi wake, uhalisia wa mambo yanayotendeka katika jamii unadhihirika waziwazi.

### **3.2.2. UKOSEFU WA PESA**

Hata kama kuna msemo kuwa pesa ndizo kiini cha maovu yote, pesa ni kitu muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku. Ni mambo mengi sana huwezi kufanya bila pesa. Hili linadhihirika hata katika safari hii ya Shafi. Kwa kutokuwa na pesa zinazohitajika kulingana na sheria za uhamiaji, Shafi akataliwa kushuka Aden. Kwa sababu hii, maafisa wa uhamiaji wanaamuru arudishwe kwao Zanzibar lakini haifanyiki hivyo kwa vile chombo anachoabiri hakiendi huko, bali kinaenda Mombasa. Hata hivyo, Shafi hajali. Hii ni kwa kuwa aona aibu kuonekana kwao tena na watu wao wanaojua kwamba alikwisha enda Ulaya kitambo. Kutokana na haya Shafi ajipata akiamia Mombasa.

Anasema,

Mimi mwenyewe nilifurahi sana kuwa chombo hicho kisingelifika Zanzibar... Kurudi kwangu kungelikuwa ni kitendo cha kushindwa. uk 23

Kwa hivyo uhamiaji huu si wa hiari kama ule wa kwanza bali ni wa kulazimishwa na hali ya mambo ilivyo kama tulivyosema hapo juu. Anajikuta katika hali hiyo kwa sababu amekosa pesa za kulipa nauli ya safari ya kurudishwa kutoka Aden hadi Mombasa. Kwa kukosa malipo hayo, afisa wa uhamiaji ampokonya pasi yake ya kusafiria. Shafi asema,

Pasi ya kusafiria nimenyang'anywa, sikuwa na hata senti moja mfukoni. Nilijiona kama niliyefungwa ndani ya jiji la Mombasa. uk 27

Hivyo basi Shafi ajipata akiwa mhamiaji Mombasa bila kupenda kwake. Atakaa huko mpaka apate pesa za kuikomboa pasi yake ya kusafiria na nyingine za kumwezesha kuendelea na safari yake. Uhamiaji huu umechangiwa na mambo mawili. Sababu ya kwanza imetokana na sheria za uhamiaji ambazo zinaingiliana na masuala ya kisiasa. Sababu ya pili imetokana na ukosefu wa pesa ambao unaingiliana na mambo ya kiuchumi.

Uhamiaji mwingine unaotokana na shida za pesa unadhihirika tena vijana hawa watatu wanapofika Eldoret. Huu umesababishwa na suala la kiuchumi. Kutokana na upungufu wa pesa, kina Shafi wanajipata wakiishi Eldoret kwa muda wa mwezi mmoja bila kutarajia. Kinachowasaidia kimetokana na uwenyeji wa Abdalla Juma Bulushi katika mji ule na uhodari wake wa kuingiliana na watu. Shafi anaeleza,

Sote hatukuwa na pesa lakini Abdalla Juma Bulushi... alipata pesa kidogo tukaondoka Eldoret baada ya kuishi hapo kwa kiasi cha mwezi mmoja. uk 58

Kutoka Eldoret, wanaingia Kampala wanakokaa kwa muda kwa ukosefu wa pesa ulio na misingi yake katika masuala ya kiuchumi. Shafi anaeleza vile kwa kuwa, wote hawakuwa na pesa wala mpango wowote wa kuwawezesha kupata pesa, basi walikuwa hawajui mpaka lini wangelielelea kuishi pale Kampala.

### **3.2.3 UHITAJI WA KAZI**

Ni wajibu wa kila mwanadamu kufanya kazi ili kujikimu kimaisha. Hata Mwenyezi Mungu Mwenyewe katika Biblia Takatifu Ameongea juu ya umuhimu wa kazi katika maisha ya binadamu. Kitabu cha pili cha *Thessalonians*, mlango wa 3 mstari wa 10, inasema kuwa, ikiwa mtu hafanyi kazi, basi hasile. Inaendelea kuwahimiza watu wavivu kufanyia kazi kile wanachokula. Kutafuta kazi ndiko kunakomfanya Shafi na mwenzake Abdalla Bulushi kuchukua uamuzi tunaoelezewa. Kwamba, wakiwa Nimule iliyo mpakani mwa Uganda na Sudan, washauriwa kurudi Kampala ili wakachukue viza ya kuwawezesha kuingia Sudan. Badala ya kurudi Kampala wanashauriana na kuafikiana waende Bungoma ambako wanaamini ingekuwa rahisi kupata vibarua vya kuwawezesha kupata pesa za kuwakimu kimaisha na kuendelea na safari yao. Kwenda kwao Bungoma na Nakuru ni uamuzi unaotokana na masuala ya kiuchumi ya kutafuta kazi ili wajiendeleze kimaisha. Kwa hivyo, Abdalla Bulushi ahamia Nakuru na Shafi naye ahamia Bungoma. Shafi anasema,

Nilikwisha ishi hapo kwa muda wa miezi sita na niliona Bungoma na udogo wake, kweli ni mahali pa kumtia mtu mshawasha... Siyo kwa uzuri wake...Ni kwa sababu ya bashasha na uchangamfu wa watu na rehema ya vyakula iliyokuwa imebarikiwa mji huo.uk.155

Baada ya kina Shafi kutoka Misri, Abdalla Juma Bulushi pia aishi maisha ya kuhamahama. Uhamaji huu watokana na mambo ya uhitaji wa kazi.

Mwandishi aeleza,

Baada ya kufika Kairo, mimi na Abdalla tulirudi sote Zanzibar. Baada ya muda mfupi alikwenda Cuba ambako alipata mafunzo ya kijeshi kuongezea yake aliyoyapata Kairo... Baada ya kupata mafunzo yake ya kijeshi huko Cuba, alirudi Zanzibar na kujiunga na harakati za kisiasa. uk 480

Hayo hayakuishia hapo bali Abdalla alihama tena kutoka Zanzibar na kwenda Urusi. Asema,

Abdalla alikwenda Urusi kwa mafunzo zaidi ya kijeshi. Aliporudi alifanya kazi Nachingwea, Morduli na Dar es Salaam. Wakati huo alikuwa na cheo cha Luteni. uk 480

Kama ule wa Abdalla Bulushi baada ya kutoka Misri, hata uhamaji wa Shaaban ulisababishwa na uhitaji wa kazi. Hii ni kwa sababu kote kule anakoenda anafanya hivyo kwa ajili ya kazi.

Twaambiwa,

Mtiririko wa maisha yake ulikuwa kama ule wa Abdalla. Alipata mafunzo ya kijeshi Misri, Cuba na Urusi na kujiunga na jeshi la wananchi wa Tanzania. Kama Abdalla alifanya kazi Nachingwea, Morduli na Dar es Salaam akiwa na cheo cha Luteni. uk 481

Maelezo hayo yanatufahamisha kuwa, wote watatu waliishi maisha ya kuhamahama. Baada ya kutoka Misri, uhamaji na uhamiaji wao wote ulikuwa ni wa hiari bali si wa kulazimishwa. Kwa hivyo wanaufurahia na kazi zote wanazozifanya wanazifanya kwa moyo mkunjufu.

### **3.2.4 KUTAFUTA VIZA**

Viza ni cheti mtu apewacho ili kumwezesha kuingia nchi ngeni. Kutokuwa nacho huwahangaisha watu sana. Mambo ya viza huingiliana na uhalisia wa kisiasa. Hii ni kwa sababu, cheti hiki huhalalisha kuweko kwako katika nchi ngeni na ni mojawapo ya sheria za uhamiaji. Sheria nazo huhusiana na uhalisia wa kisiasa. Uhamiaji wa kina Shafi Khartoum na Sudan

wasababishwa na uhitaji wa viza ya kwenda Misri. Huko Khartoum, kina Shafi wakutana na vijana wengine wa kutoka nchi nyingine na katika mazungumzo yao, ni wazi kwamba wote wamekwama huko kwa ajili ya viza. Wasimulia vile wamekaa huko kwa zaidi ya mwezi mmoja wakingojea kupata viza ya kuingia Misri na kwa hivyo ni uhamiaji unaotokana na masuala ya kisiasa. Vijana wengine kama vile Oluoch walikuwa wamekwisha ishi sana Khartoum. Hata aeleza vile alikuwa mwenyeji aliyekijua kila kipenyo na kichocho cha jiji hilo. Ofisi zote za ubalozi za jiji lile alikwisha zitembelea akiwa katika juhudi za kutafuta masomo. Wake ni uhamiaji unaotokana na masuala ya kijamii kwani anatafuta elimu.

### **3.2.5 KUPATA MAFUNZO YA KIJESHI**

Kila nchi huhitaji wanajeshi kwani ndio hukinga nchi dhidi ya uvamizi kutoka nchi nyingine. Nchi ya Kenya kwa mfano ilikuja kutambua umuhimu wa kuwa na wanajeshi waliohitimu na kuwa na ujuzi wa kupigana na maadui zake wakati walipigana na kundi la Al-Shabaab. KDF walipigana nao mpaka huko kwao Somalia na kutoka wakati huo, KDF imekuja kutambulika hata na mataifa mengine.

Ingawa kina Shafi hawakuwa wamepanga kufanya mafunzo ya kijeshi, wajipata wakiyafanya kwa kushawishiwa. Hivyo basi uhamiaji wao katika kambi ya kijeshi umesukumwa na masuala ya kisiasa yanayoleta uhalisia wa kisiasa na kihistoria. Vipengele hivi vya nadharia ya uhalisia huingiliana vizuri sana na suala la ukoloni. Kihistoria, ukoloni ulihalalisha kutawaliwa kwa nchi moja na nyingine. Mambo ya utawala nayo yanaleta uhalisia wa kisiasa. Kwa hivyo Shafi anapoeleza jinsi hamasa za kisiasa zinavyowashawishi mpaka wanaachana na mipango yao ya elimu, tunawaelewa. Wanaenda Misri wakati nchi nyingi za Afrika ziko katika harakati za kuuangamiza ukoloni.

Shafi aeleza vile watembelea ofisi inayoshughulikia mambo yao mara nyingi bila yeyote kuwambia ukweli wa mambo. Walakini, baada ya kushawishiwa wakubali kwenda kufanya mafunzo ya kijeshi. Anasema,

Tuliyaanza maisha ya kambini hapo kwa kuvua nguo za kiraia na kuvaa sare za kijeshi. uk 396

Mafunzo yenyewe ni magumu na yanahitaji kujitolea kwingi na mtu kuwa tayari kutii amri za wakubwa wake bila kuuliza swali. Anasema vile walionywa na kuambiwa kuwa, yule angethubutu kupinga amri ya mkubwa wake basi dunia angeiona juu chini, chini juu. Anaendelea kueleza vile, kwa muda wa wiki nzima darasa lao lilihamia jangwani wakiripua miripuko ya kutisha. Walichoka, tena wakati mwingine walikuwa na njaa. Hivyo ndivyo mafunzo yao ya kijeshi yalivyokuwa mpaka walipohitimu.

### **3.2.6 KUKOMBOA NCHI ZAO**

Baada ya Shafi na wenzake kutoka nchi mbalimbali kumaliza mafunzo yao ya kijeshi Misri, warudishwa makwao kwenda kuungana na wazalendo wengine ili kukomboa nchi zao kutoka kwa minyororo ya ukoloni. Shafi, Abdalla Bulushi na Shaaban warudishwa nchi yao Zanzibar. Kuhama kwao Misri kumepangwa na wanasiasa wanaosimamia mambo ya ukombozi wa nchi za Afrika. Tunaambiwa kuwa, hawa hukutana katika nyumba nambari Kumi na Tano huko Zamalek, Misri. Wanapohama kutoka Misri, wahamia kwao Zanzibar wanakoanza maisha mapya ya uanajeshi ya kupigania uhuru wa nchi zao. Shafi aeleza vile wanaporudi kwao Zanzibar, wanakuta siasa ikiwa imepamba moto. Yeye hajiingizi katika vyama vya kisiasa bali anajiunga na vyama vinavyotetea masilahi ya wafanyakazi.

### **3.2.7 KUANZA MAISHA MAPYA**

Uhamaji wa Shafi Ujerumani umetokana na haja ya kutaka kurudi kwao Zanzibar ili akaanze maisha mapya. Hii inafanyika baada ya kumaliza masomo yake huko Ujerumani. Uhamaji huu pia umesababishwa na masuala ya kijamii yanayomhitaji mtu kurudi kwao ili akaisaidie jamii na nchi yake. Anarudi kwao Zanzibar akiwa amehitimu na kwa hivyo anajivunia masomo yake. Anasema kuwa ni elimu aliyopata kwa kupitia visa na mikasa, taabu na mashaka yaliyomkumba lakini mwishowe afurahi kuona kwamba amemaliza vizuri. Baada ya Shafi kuishi maisha ya kuhamahama, mwishowe aamua kurejea kwao Zanzibar.

Kurejea kwake kunaafikiana na maoni ya Ndalul na Kitula (1989:136) katika methali isemayo, “Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani.” Shafi arejea kwao nyumbani (ngamani) akiwa amekata kiu aliyokuwa nayo ya elimu. Anasema,

Nilisoma na kuhitimu na nilirudi nyumbani kufungua ukurasa mpya wa maisha yangu. uk 475

### **3.3.0 KUTATHMINI MANUFAA YA UHAMAJI NA UHAMIAJI**

Manufaa ni faida. Jambo lolote tufanyalo huwa na faida au hasara. Watu hupenda kupata faida si hasara. Hii ndiyo sababu tumejaribu kuangalia manufaa ya uhamaji na uhamiaji wa wahusika katika riwaya hii. Manufaa yaweza kugawika kwa njia tatu: kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa kurejelea riwaya ya *Mbali na Nyumbani*, tumeangalia mifano mbalimbali inayohusiana na masuala hayo matatu. Tumeanza na manufaa ya kiuchumi.

### 3.3.1 MANUFAA YA KIUCHUMI

Uhamiaji una manufaa ya kiuchumi kama inavyodhihirika kupitia kwa kijana anayeitwa Abdo. Shafi anakutana na kijana huyu huko Bungoma. Anasema,

Abdo alikuwa ni kijana wa kishihiri mwenye asili ya Yemen. Na yeye alikuwa nd’o katika wale waliofika Bungoma wakaselelea hapo hapo. Alikuwa akimiliki basi moja kubwa aina ya Volvo domo refu lililokuwa likisafirisha abiria kati ya Bungoma, Kakamega na Kisumu. Aliliita basi lake Mawingo Bus. uk 116

Basi la Mawingo ni basi lililokuwa maarufu sana miaka iliyopita na kutajika kwake kunatuletea uhalisia wa mambo. Kutokana na maelezo hayo, tunagundua kuwa, Abdo ni mgeni ambaye amehamia Bungoma na ameweza kuwa na biashara nzuri ya mabasi ya usafiri. Jambo hili linathibitisha ukweli kuwa uhamiaji una manufaa. Uhamiaji wake Bungoma umemletea faida na ndiyo sababu biashara yake imenawiri mpaka ameweza kununua mabasi mawili na kuajiri wafanyakazi.

Shafi pia ni mwingine anayethibitisha kwamba, uhamiaji una manufaa. Anapohamia Bungoma anabahatika kuajiriwa na Abdo kuwa kondakta wa mojawapo ya mabasi yake mawili. Anasema kuwa Abdo anapomwuliza ikiwa kazi ya ukondakta ataiweza, anamjibu,

Naam, ... Na nifikiri nini hasa na mimi kazi naisaka kama lulu. Kazi yoyote ile, kwangu ilikuwa ni kazi... Hapo hapo Abdo aliniajiri kuwa kondakta wa basi lake la pili aliloliita Kuiva. uk 135

Uhamiaji wa Abdalla Bulushi huko Nakuru umemletea manufaa pia. Kazi ambayo Abdalla amepata huko Nakuru ndiyo inayomwezesha kuweka akiba ambayo pamoja na ya Shafi wanatumia kupanga na kufufua safari yao ya kwenda Misri. Kama si kazi hizo walizopata,

safari yao ingebakia kuwa ndoto. Kwa hivyo uhamiaji wao Bungoma na Nakuru mtawalia umewaletea manufaa ya kiuchumi.

Kujifunza mambo ya uandishi wa magazeti ni manufaa mengine ya uhamiaji wa Shafi Zanzibar. Anaporudi kutoka Misri, ndipo anapoanza kujihusisha na vyama vya wafanyakazi na kisha kuwa mwandishi wa magazeti. Ingawaje hatujaambiwa, tunakisia kuwa elimu aliyoipata huko Ujerumani inaweza kuwa inahusiana na kuwa kwake mwandishi wa vitabu vya fasihi. Ni kazi anayoifanya hadi sasa. Kazi yenyewe imemwezesha kujikimu kimaisha na kwa hivyo uhamiaji huo umempa manufaa ya kiuchumi.

### **3.3.2 MANUFAA YA KISIASA**

Manufaa ya kisiasa yamehusiana sanasana na uhamiaji Sudan na huko Misri ambako hamasa za kisiasa zinaendelezwa. Shafi na wenzake wamehamia Sudan kwa kuwa wanangojea kupata viza ya kuingia Misri. Viza hiyo haipatikani kwa urahisi na ndiposa wanafaa kuwa na subira na mwishowe wanafanikiwa kuipata. Kwa hivyo, kuhamia kwao Khartoum kwa madhumuni ya kupata viza kunazaa matunda. Viza hiyo ndiyo matunda au manufaa ya uhamiaji huko. Hii ni kwa sababu bila hiyo viza hawawezi kwenda Sudan na baadaye Misri.

Ujumbe tunaopata kuhusiana na Misri kuwa kitovu cha siasa ya kuzikomboa nchi za Afrika kutoka minyororo ya ukolono ni muhimu. Tunaelezwa,

Wakati huo Kairo ilikuwa ni chungu cha siasa ya Afrika. Chungu hichi kilikuwa kimeinjikwa jikoni, siasa ilikuwa ikitokota sawasawa. Wananchi wa Afrika walikuwa wakidai uhuru. Vyama vya wapigania uhuru wa Afrika kutoka nchi mbalimbali vilijikusanya pamoja ndani ya nyumba nambari Kumi na Tano... Mtaa wa Zamalek. Ndani ya nyumba hiyo kila chama cha kupigania uhuru kilikuwa na ofisi yake. uk 374

Tunapoendelea mbele, tunafahamishwa haya,

Waliokuwemo wote walikuwa wanaharakati wa kupigania uhuru wa nchi zao. Humo ilizungumzwa lugha moja tu, lugha ya ukombozi wa Afrika. Lugha zote zilizungumzwa zikiwemo Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kiarabu au hata Kiswahili, lakini ujumbe wake ulikuwa ni ukombozi wa Afrika. uk 382

Kule kuwa na lugha mbalimbali lakini ujumbe ulikuwa mmoja kunaashiria kitu kimoja. Kwamba nchi hizi za kifarika zilikuwa zikitawaliwa na wakoloni mbalimbali lakini wafrika walikuwa na umoja. Maelezo hayo yanatupa mwangaza kwamba, kuna wanaharakati waliojitolea kuhamia Misri ili kufaulisha shughuli hizo za kuwahamasisha waafrika juu ya ukombozi wa Afrika. Kwa sababu juhudi zao pamoja na za wengine zilipelekea kukombolewa kwa bara la Afrika, tunaweza kusema kwamba uhamiaji huo ulileta manufaa kwa waafrika.

Kina Shafi wanapofika Misri na kukutana na waliyeelekezwa kwake, wanakaribishwa vizuri na wanafurahia maisha ya huko. Inakuwa kinyume na maisha ya shida waliyokuwa wamezoea walipokuwa Uganda na Sudan. Shafi Anasema,

Maisha yetu mjini Kairo hayakuwa kama yale ya Khartoum. Ya Kairo yalikuwa na afadhali sana. Katika nyumba yetu ya Munira hatukulala chini kama wafiwa waliokuwa wakilala matanga kama ilivyokuwa katika kile kijumba cha udongo kilichokuwa maskani yetu kule Khartoum. Tulilalia vitanda vizuri vya spiringi tukipumzika kwenye ukumbi uliokuwa na makochi ya vitambaa vya mahameli. Hatukuwa na wasiwasi wa kisabehi wala chajio. uk 387

Hii inatokana na makaribisho wanayopewa huko Misri. Kwanza wanakaribishwa na mwenyeji wao waliyekutanishwa naye kutoka Bungoma. Baadaye wanajulishwa kwa Ali anayewaunganisha na wafrika wengine wanaoshughulikia ukombozi wa Afrika. Kukaribishwa

kwao hapa kunatokana na umoja unaohimizwa na hamasa za siasa ya kuikomboa Afrika. Haya yanaonyesha kuwa uhamiaji huu una manufaa. Kadiri Shafi na wenzake wanavyozidi kuhamasishwa kisiasa, ndivyo wanavyozidi kuona umuhimu wa kujiunga na wengine katika matayarisho ya kupigania nchi zao. Hii inajitokeza anaposema,

Wakati ule, upepo wa mabadiliko ukivuma katika Bara la Afrika, uwanasiasa ulikuwa ndio mtindo wa maisha. Watu walihisi kuwa hadhi na uluwa vilikuwa katika kuwa mwanasiasa. Kuwa mwasi wa mfumo wa kikoloni na mpinzani wa utawala wa kigeni. uk 398

Ushawishi huu unawafanya wakubali kupewa mafunzo ya kijeshi na baadaye wanahitimu kama anavyosema,

Wiki ya mwisho ya mafunzo yetu ilipomalizika tulikuwa askari jeshi waliotimia, tayari kwa mapambano. uk 412

Kwetu, mafunzo haya ya kijeshi ni manufaa ya uhamiaji wao Misri. Hii ni wazi kulingana na maelezo hapo juu kwamba hadhi na uluwa vilikuwa katika uwanasiasa wa kuangamiza ukoloni. Anaendelea kutujuza jinsi alivyokwenda kujitosa katika maisha ya kujitolea. Haya ni maisha ya kujitolea kwa ajili ya nchi yake. Ni maisha ya kutojijali yeye bali kuujali umma. Anasema,

Niliweka kiu yangu ya kutafuta elimu nyuma yangu na maslahi ya nchi yangu nikayaweka mbele. Nilijitosa kufa au kupona. uk 413

Kujitolea kwao hakukuwa kwa bure kwa sababu baadaye wanajipata wakiheshimiwa sana popote wanapoenda. Kwa mfano, anatuambia vile wanalishwa vizuri na kuchukuliwa kwa taadhima kubwa.

Anasema,

Nilifungua mlango na kabla sijasema chochote yule mwenyeji wetu aliniambia, *Breakfast Sir*. Sikumbuki lini mara ya mwisho niliyoitwa *Sir*. Pale pale nilibaini kuwa kumbe pale tulipokelewa tukiwa watu wakubwa waliostahili kuitwa *Sir*... Tultengewa meza yetu peke yetu... Tulikula kwa nyuma na visu... Tulikuwa kama tuliotoka kwenye dhiki, ghafla tukaingia kwenye faraja. uk 415

Shafi na wengine wote waliohamia Misri na kwingine kwa ajili ya kuzikomboa nchi zao walinufaika nchi hizo zilipopata uhuru. Mifano zaidi ya wanaharakati wa kupigania uhuru waliohama makwao ili kuendeleza mambo hayo ni wana-MauMau nchini Kenya waliotorokea misituni. Waliishi misituni kwa miaka kadhaa na juhudi zao ziliza matunda kwa sababu mwishowe nchi zao zilipata uhuru waliokuwa wakiupigania. Wengine waliohama kwao katika juhudi za kuikomboa nchi yao ni baadhi ya wanachama wa ANC ya Afrika Kusini. Kuna wakati baadhi ya wanachama hao waliamia nchi ya Tanzania ili wapate mafunzo ya kuwawezesha kupigana dhidi ya mfumo wa siasa ya ubaguzi wa rangi. Mifano hiyo inaonyesha kuwa uhamiaji una manufaa kwani hata juhudi hizo za ANC ziliifanya Afrika Kusini kujinyakulia uhuru wake katika mwaka wa 1994. Hatuwezi kuzisahau juhudi za shujaa Nelson Mandela (marehemu) aliyejitolea kuikomboa nchi yake kiasi cha kukubali kuishi gereza kwa karibu miaka thelathini alipohamishiwa Kisiwa cha Robin.

Shafi pia anatufahamisha vile hamasa za kisiasa wanazopata huko Misri zinavyoyaathiri maisha yake anapofika Zanzibar. Anasema,

Kwa hivyo nilipofika Zanzibar nilijiingiza katika kuicheza ngoma hiyo ili niujue vizuri uhondo wake. Nilijiingiza katika ngoma hiyo kwa kipitia katika vyama vya wafanyakazi ambako nilikutana na waandishi kadha walionifunza namna ya kuandika magazeti. uk 423 – 424

Kule kuingizwa katika mambo ya siasa akiwa Misri ndiko pia kunakomfanya ahusiane na wanasiasa. Hata kama haingii katika chama chochote cha kisiasa anakuwa upande wa vyama vya kupigania haki za wafanyakazi. Vyama vya kisiasa wakati huu vilikuwa vikihusiana sana. Hii ni kwa sababu, wakati vyama vya kisiasa vilipopigwa marufuku katika nchi mbalimbali Afrika, vyama vya wafanyakazi ndivyo vilivyoachwa vikiendelea na mapambano dhidi ya ukoloni. Wakati huu ndipo Shafi anakutana na wanasiasa wanaopanga kumpeleka Ujerumani kusoma kupitia ufadhili wa kisiasa. Ufadhili huu wa masomo yake ni manufaa ya uhamiaji wake Zanzibar unaotokana na uhamiaji wake Misri. Wanamwambia,

Tutakupeleka Ujerumani ukasomee mambo ya uchumi katika Chuo kikuu cha Wafanyakazi. uk  
434

Manufaa mengine ya uhamiaji yanadhihirika tukirejelea maisha ya Abdalla Juma Bulushi na Shabaan, wenzake Shafi. Hawa nao wanapotoka Misri, wanajiunga na vikosi vya majeshi katika nchi mbalimbali kama vile Cuba, Urusi na Tanzania ili kuimarisha mafunzo yao ya kijeshi. Mwishowe wanaajiriwa kama maafisa katika jeshi la nchi yao. Nchi yao ilikuja kuitwa Tanzania baada ya Zanzibar kuungana na Tanganyika.

### **3.3.3 MANUFAA YA KIJAMII**

Haya hutokana na mambo kama vile elimu ambayo ndiyo chanzo cha safari hii ndefu ya Shafi. Elimu anayoisaka na inayosababisha maisha yake ya kuhamahama mwishowe anaipata huko Ujerumani. Mifano mingine ya manufaa ya kijamii inayojitokeza katika riwaya hii ni pamoja na kufurahia uzuri wa Bungoma na ufufuzi wa mahusiano yao ya zamani.

Manufaa ya kijamii ya uhamiaji yapatikana huko huko Bungoma ambako Shafi akueleza kuwa mahali kuzuri. Anakuelezea hivi,

... Bungoma... Kweli ni mahali pa kumtia mtu mshawasha... Ni kwa sababu ya bashasha na uchangamfu wa watu wake na rehema ya vyakula iliyokuwa imebarikiwa mji huo... Katika mji huo... Watu husalimiana na kujuliana hali kwa kuitana *mukhwaas* ikiwa na maana ya shemeji... Ni watu waliokuwa hawana makuu... Kila mmoja alikuwa ametosheka na vile alivyokuwa na hakuna aliyekuwa na matamania yasiyo kadiri yake. Kwa hali kama hiyo ilikuwa rahisi kwa mgeni kama mimi kukubalika kwa urahisi katika jamii ya watu wa hapo. Kwa muda mfupi nilioishi Bungoma nilijihisi kama niliyekuwa nyumbani. uk 155

Maelezo hayo yanaonyesha kuwa, mahali pazuri panaweza kumletea mhamiaji manufaa. Hii ni kutokana na amani, umoja na jinsi mtu anavyoweza kufurahia kama anavyofanya Shafi.

Kuhamia kwa Abdalla Nakuru nako kunamwezesha kukutana na Mohammed Saleh mmoja wa marafiki zao waliokuwa wakisoma nao Chuo cha Ualimu. Huyu anawakaribisha na kuwashauri kuhusu jinsi watakavyoendelea na safari yao. Hata anawaelekeza kwa rafiki yake anayeitwa Maalim Idi ambaye anawambia kuwa angewasaidia kupata viza ya kuingia Sudan. Anawashauri,

Msiende Kampala moja kwa moja. Mtasafiri mpaka Njinja... Mtachukua tekisi na mtamwambia dereva akupelekeni Bugembe. Hapo Bugembe ninaye sahibu wangu anaitwa Maalim Idi. Mtafuteni na mkimpata mwelezeni juu ya shida yenu ya visa, yeye atakusaidieni kuipata. uk 174

Uhamaji wa kina Shafi kutoka Misri na uhamiaji wao tena nchi zao unarejesha mahusiano yao ya kifamilia na kijamii. Shafi anapofika nyumbani kwao, wanafurahiana wote. Anasema kuwa, mama yake anapomwona anashtuka na kumtumbulia macho. Halafu anamzungumzia kwa sauti ya hisia za mama aliyepotelewa na mwanawe akakata tamaa ya kumwona tena. Anaendelea kusema kuwa baba yake anapomwona, anamtazama kwa mshangao na kisha akaitanua mikono yake akamwita. Shafi naye alimkimbilia, akamkumbatia na kujilaza juu ya bega lake. Kurejea kwake nyumbani kunamwezesha kuhudhuria mazishi ya babake mdogo, Maalim Said Omar. Hii

pia inampa nafasi ya kutangamana na wanajamii wanapohudhuria mazishi haya na hata baadaye waendelea kuonana. Haya yametokana na kurejea kwake nyumbani Zanzibar.

Mawasiliano ya Shafi na Daniel, rafikiye baada ya muda wa miaka arobaini na saba yamefufua ushuba uliojengwa zamani. Hii ni baada ya Daniel kupewa anwani ya Shafi na Profesa Taban Liyong kutoka Sudan wanapokutana katika kikao cha waandishi huko Uganda. Daniel anatumia anwani hiyo kumwandikia Shafi barua ya kumjulia hali na kutoka hapo wanaendelea kuwasiliana. Haya ni matokeo ya ufufuzi wa mahusiano yaliyotokea zamani wakati Shafi na wenzake walipokutana na Daniel Khartoum. Huu ni wakati walipokuwa wakitafuta viza ya kuingia Misri. Kwa hivyo mahusiano haya ni manufaa ya uhamiaji wao Sudan.

Shafi anaendelea kutukumbusha mahusiano yao ya zamani na Shabaan. Huyu alikuwa mwenzake safarini na walikutana alipokuwa amehamia Bungoma akitafuta pesa za kuiendeleza safari yake. Waliandamana pamoja katika safari hiyo ndefu mpaka Misri. Waliachana baada ya kurudishwa kwao Zanzibar walipokamilisha mafunzo yao ya kijeshi huko Misri. Kwa bahati nzuri, wanakuja kukutana katika uzee wao wakati Shabaan hata amestaafu kutoka jeshini. Shafi anatuambia vile huwa wakikutana mahali panapoitwa Mkunazini. Anasema,

Hapo ndipo anapokuwa kila mara, akinywa kahawa... Mimi pia hupenda kunywa kahawa hapo na tunapokutana na Shabaan basi lazima tutakumbushana tukio lolote lile lililotukuta tukiwa mbali na nyumbani. uk 481

Kukutana kwao ni manufaa ya uhamiaji uliotokea huko Bungoma na unatokea tena wakiwa kwao Tanzania. Hii ni kwa sababu wanapokutana, wanafurahiana, wanahimizana na kukumbashana ya zamani na hiyo inawapunguzia upweke ambao huandamana na uzee.

### **3.4.0 HITIMISHO**

Katika sura hii, tumeonyesha kuwa kuna aina mbili za uhamaji na uhamiaji katika riwaya hii. Aina hizo ni, uhamaji na uhamiaji wa hiari na wa pili ni wa lazima. Huu wa pili unatokana na kulazimishwa na vile hali ya mambo ilivyo wanakoenda. Pia tumechunguza sababu za uhamaji na uhamiaji huu na tumeona kuwa, vyote vinaandamana. Hii ni kusema kuwa, aina ya uhamaji na uhamiaji hufuatana na sababu zake. Vilevile tumejaribu kutathmini manufaa yanayotokana na uhamaji na uhamiaji. Tumeonyesha kuwa uhamaji na uhamiaji una manufaa ya aina mbalimbali kama vile: manufaa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

## **SURA YA NNE**

### **MATATIZO YANAYOWAKUMBA WAHAMAJI NA WAHAMIAJI**

### **KATIKA RIWAYA YA *MBALI NA NYUMBANI* NA JINSI**

### **WANAVYOJARIBU KUYASULUHISHA**

#### **4.0 UTANGULIZI**

Katika sura hii tumejishughulisha na mambo mawili. Jambo la kwanza linahusu matatizo yanayowakumba wahamaji na wahamiaji katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. La pili linaangalia jinsi wahusika wanavyojaribu kusuluhisha matatizo hayo. Tumejaribu kuyachanganua kwa kina matatizo yanayowakumba wahusika hao na jinsi wanavyojaribu kuyatatua. Matatizo hayo hutokana na masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Matatizo ya uhamaji na uhamiaji kijamii ni kama vile: shida za usafiri, chakula, malazi, shida za mawasiliano zinazotokana na ukosefu wa lugha moja ya kuelewana kati ya wahamiaji na wenyeji wao na mengineyo. Matatizo ya kiuchumi ni kama vile: ukosefi wa pesa za mahitaji ya kila siku na changamoto za kazi. Matatizo ya kisiasa sanasana yametokana na sheria za uhamiaji na changamoto za mafunzo ya kijeshi. Katika sehemu ya mwisho tumeangalia jinsi wahusika wanavyojaribu kutatua matatizo yanayowakumba. Kwa kifupi, matatizo ambayo yamejitokeza katika sehemu hii ni sawa na yale wanayopitia wahamaji na wahamiaji wengine popote pale. Hivyo basi yanaleta picha halisi ya hali ya uhamaji na uhamiaji katika maisha ya waathiriwa ulimwenguni. Haya yanaoana vyema na nadharia ya uhalisia. Hii ni kwa vile, nadharia hii huhimiza kuweco kwa ukweli wa mambo katika kazi yoyote ya kifasihi iliyoandikwa kwa misingi ya nadharia ya uhalisia.

#### **4.1.0 MATATIZO YA UHAMAJI NA UHAMIAJI**

Katika sehemu hii, tumeshughulikia matatizo ya uhamaji na uhamiaji kama vile: matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Haya ni matatizo yanayowakumba wahusika wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji katika nchi mbalimbali. Matatizo haya hayawaathiri wahusika tu bali pia wenyeji wao na waliowaacha nyuma. McNeill na Adams (1978:426) wanasema kwamba, faida na hasara za uhamaji kwa wahamaji, wenyeji wao na nchi walizohama na kwa binadamu, aliye hai na ambaye hajazaliwa haviwezi kuhesabika. Tunakubaliana nao kwa sababu pengo wanaloacha nyuma halizibiki na athari yao wanakoenda ni kubwa. Athari hii yaweza kuwa nzuri au mbaya.

Huu ni uhalisia wa kihistoria ambao unatukumbusha jinsi uhamaji na uhamiaji wa Wafrika Marekani wakati wa biashara ya watumwa ilivyozinufaisha nchi za Ulaya. Wakati huu Marekani ilikuwa koloni ya Uingereza. Uingereza ilikuwa ikiendeleza kilimo cha mazao ya aina mbalimbali ikiwemo miwa na pamba. Mazao hayo yalikuwa yakipelekwa Ulaya kama malighafi ya kutengeneza bidhaa katika viwanda vyao. Walipata faida nyingi kutokana na uhuzaji wa bidhaa hizo Ulaya, Afrika Asia na kwingineko. Huu ukiwa wakati wa mapinduzi ya kiviwanda, nchi nyingi za Ulaya zilikuwa zikishindania maendeleo ya viwanda. Ni wakati huu nchi nyingi za Afrika ziliposhuhudia uhamaji wa watu wao waliopelekwa Marekani kuendeleza kilimo hicho kama watumwa. Walikuwa wakichagua vijana na watu wenye nguvu ambao wangehimili safari ndefu melini na ambao wangeweza kufanya kazi wafikapo huko. Wengine walitumika majumbani mwa Wazungu hawa huko Ulaya. Kwa kifupi, biashara hiyo ya watumwa imechangia sana kubakia nyuma kwa Bara la Afrika na kuendelea kwa nchi za Ulaya. Si biashara ya watumwa tu iliyohusika bali kuna mengine.

#### **4.1.1 MATATIZO YA KIJAMII**

Uhamaji na uhamiaji huzusha matatizo mengi ya kijamii. Haya ni pamoja na, shida za usafiri, chakula, malazi, ajira, ukosefu wa lugha ya mawasiliano na mengineyo. Shida hizi ambazo kina Shafi wanapitia ni zilezile ambazo wahamaji na wahamiaji wengine hupitia. Hizi huwaathiri na kuyafanya maisha yao kuwa magumu sana. Mengi ya matatizo haya ni ya kimsingi na mahitaji kama vile, chakula, malazi na lugha ya kumwezesha mtu kuwasiliana ni muhimu sana na kila mwanadamu huvihitaji. Hii ndiyo sababu Umoja wa Mataifa kupitia kwa shirika lake, UNHCR hushughulikia wakimbizi sana kuhusiana na mambo ya chakula, malazi na matibabu. Tumeanza na matatizo ya usafiri.

##### **4.1.1.1 SHIDA ZA SAFARI**

Kulingana na Ndal, Babusa na Mirikau (2014:549), safari ni kitendo cha kutoka pahali pamoja na kwenda pengine ambapo ni mbali. Matatizo ya safari ni yale wanayokabiliana nayo wakiwa safarini kuelekea mahali mbalimbali. Ikumbukwe kwamba, safari hii ndefu ya Shafi ndiyo imesababisha maisha ya uhamaji na uhamiaji kwa sababu imekumbwa na matatizo mengi. Kwa mfano, wakati Shafi anaabiri mashua ya kumfikisha ilikokuwa meli ya kumsafirisha mpaka Aden, mashua inakumbana na mawimbi makali ya kuogofya sana. Anasema,

Yule mpiga kesia alikuwa... akibishana na mawimbi na upepo mkali. Mara nyingine maji yalikuwa yakiruka mpaka ndani ya chombo pale mashua ilipopigwa kofi kubwa la wimbi ikayumba huku na huku ukadhani itazama sasa hivi. uk 12

Shida nyingine ni kwamba, Shafi pia hana uwezo wa kutumia usafiri wa meli ya abiria bali anatumia meli ya mizigo.

Hii inadhahirika anaposema,

M.V. Ubena haikuwa meli ya kuchukua abiria. Ilikuwa meli ya kuchukua mizigo. Abiria waliosafiri kwa meli hiyo nao walionekana kama mizigo tu. Melini humo hamkuwa na fursa zozote kwa ajili ya abiria... uk 13

Safari yenyewe ni ndefu, ya kuchosha na kuvunja moyo kama Shafi anavyotuarifu.

Safari ilikuwa imeshtadi. Tulikuwa katikati ya bahari kuu hatuoni chochote isipokuwa bahari Kusini, bahari Kaskazini, bahari Mashariki, bahari Magharibi... Mawimbi yakipanda na kushuka. Tulihasabu siku moja moja. Ilipofika usiku, mawazo ya nyumbani yalinijia... uk 16

Shafi anazidi kutueleza kuhusu safari yenye zahama na vishindo vya bahari iliyokuwa ikivurumisha mawimbi makubwa makubwa. Ilikuwa kiasi cha kuifanya meli kuonekana kama ingelizama wakati wowote. Safari yao ya kwenda Nairobi ilikuwa kwa treni wakiwa wasafiri wa daraja la tatu. Mabehewa ya wasafiri wa daraja hilo, kwa desturi hujaa tele na abiria wengine huning'inia milangoni. Huu ni usafiri usio na starehe zozote na wasafiri hawa huwa hawana lingine. Kwa sababu ya msongamano wa watu ndani huwa na visa vingi vya wizi ambao huwakosesha abiria usingizi wakiogopa kuibiwa pesa na mizigo yao. Tahadhari ya kuweko kwa wizi inatolewa na Abdalla Bulushi. Kulingana na Shafi, Abdalla Bulushi ni mzoefu wa safari za treni na hivyo basi hujua ujanja na ukora wa wasafiri wanaojiingiza katika misafara ya treni ili kuwaibia abiria.

Wanapofika Nairobi, wanakuta hali ya hewa ikiwa tofauti ya huko Mombasa kulikokuwa na jua kali. Shafi anasema kuwa, kwa vile walipotoka Mombasa kulikuwa na jua kali, hawakufikiria kubeba mavazi ya kujikinga na baridi.

Kwa hivyo baridi ambayo hushuhudiwa mwezi wa Julai inawahangaisha sana. Anasema,

Katika majira yale ya kipupwa, hali ya hewa ilikuwa baridi sana... Nilipoondoka Mombasa sikuhitaji nguo yoyote ya kunikinga na baridi kwa hivyo shati tu lilinitosha. uk 48

Maelezo hayo yanasema mengi kuhusu jinsi wasafiri au wahamiaji hukumbana na shida nyingi waendako bila ya kutarajia. Kwa hivyo, hutatizika wasijue la kufanya kwani hawakutarajia kukabiliana na hali ngumu kama hizo. Hali hizo hata huweza kuwasababishia magonjwa.

Wakiwa huko huko Nairobi, kwa bahati mbaya wanapata mizigo yao imeibiwa na kijana mmoja anayeitwa Odwor. Wamekutana naye katika treni anapojificha kati yao akiwakimbia wahudumu wa treni ili asilipe nauli ya usafiri. Kutoka hapo wanakuwa marafiki na wanasafiri pamoja mpaka Nairobi. Wanapoenda kuchukua mizigo yao pale walipoiacha, wanapata Odwor amewatangulia akaenda nayo yote. Wamwitishapo aliyewawekea mizigo, anawaambia,

Mizigo si mlimtuma Odwor kuja kuichukua? ...Mizigo yote ameichukua Odwor na aliniambia kwamba mlimtuma kuja kuichukua... Wema wetu na imani yetu ilitupoanza. Kumbe Odwor alikuwa mwizi na pale niliposema si haki kumhukumu mtu kwa wasifu wa sura yake, kwa Odwor nilikuwa nimekosea sana. uk 50

Tukio hili linaonyesha shida zile watu hupitia wakiwa safarini. Hizi ni pamoja na kutojua mahali pa salama pa kuiacha mizigo yenu, wakati mwingine mwaweza kumwachia mtu asiyeaminika. Katika tukio jingine, mnaweza kupata mtu anayeaminika lakini mwingine kama Odwor aje amdanganye. Wengine huamua kujibeeba mizigo yao popote waendapo lakini nayo huwasumbua sana. Njia zozote zile huwa na changamoto zake. Inasikitisha sana kuona msafiri kaibiwa mizigo yake.

Hii ni kwa sababu hiyo ni hasara kubwa kwani mtu huwa amepungukiwa na vitu anavyovihitaji aendako na labda hana pesa za kununua vingine. Hata akina Shafi wanapoibiwa mizigo yao, waachwa kutazamana wasijue la kufanya. Lakini kwa bahati njema, waliyemwachia mizigo anawahurumia na kuwapa msaada wa pesa zinazowafaa sana katika safari yao.

Tatizo lingine linatokana na kufika kwao Eldoret usiku wa manane. Hili linawanyima fursa ya kuweza kulala mjini kwani mji wenyewe uko mbali kidogo na stesheni ya reli. Kwa hivyo, walala stesheni mpaka asubuhi. Shafi anasema,

Baridi ilikuwa kali sana na sote watatu tulilitegemea blanketi moja tu alilokuwa nalo Abdalla Juma Bulushi, kwa kulalia na kujifunika. Tulitafuta upenu, ambapo tulihisi tunaweza kujibanza mpaka asubuhi... Baridi ilipenya mpaka ndani ya mifupa... Kila mmoja alilivutia blanketi lile kwake ili limpatie ujoto ujoto na kujinusuru na baridi ile. Tuliligombania lile blanketi kama watoto wadogo... mpaka kulipopambazuka. uk 55

Hayo ni matatizo yanayotokana na safari. Yayo hayo ndiyo wahamiaji wengi hupitia hasa wale wanaoenda safari ndefu na hawajui mtu yeyote waendako.

Safari ya kutoka Kampala kuelekea Sudan imekuwa ndefu na hata hawapati wakati wa kujipumzisha kwani safari ni ya mfululizo. Shafi anaongea juu ya kusafiri kutwa nzima, usiku kucha na baada ya kufika Namasagali, hawakai bali wanaunganisha safari yao kwa meli. Hii inaonyesha kuwa safari hiyo ni ya kuchosha na kwa hivyo inahitaji uvumilivu mwingi.

Shida za safari zaendelea kujitokeza. Wakati huu, wanapofika bandari ya Butiaba, pembezoni mwa Ziwa Albert, wajipata wakilala ndani ya kibanda kidogo kilichokuwa karibu na ufukwe. Hapa wapata kero la mbu waliokuwa wakitokea kwenye nyasi zilizojaa katika tope za maeneo tepetepe yaliyo kandokando ya ziwa.

Shafi anasema,

Haikuwa rahisi kuupata usingizi kwa adha ya mbu hao waliokuwa wakishambulia mfululizo na kusababisha udhia mkubwa wa watu kujizaba makofi ili kuwafukuza. uk 73

Tatizo lingine linaloshuhudiwa mara nyingi katika safari hii ya akina Shafi ni watu kusukumana wakati wa kuabiri au kushuka kutoka vyombo vya usafiri wa abiria. Mifano ni mingi na jambo hili linajitokeza katika usafiri wa magari ya umma, treni na hata meli. Huu ni mfano mmoja tu tumetoa. Shafi anasema,

Abiria walikuwa wamejikusanya kwenye ngazi ya kuingilia melini wakibinyana na kusokotana ... Na wale walinzi nao waliwasukuma kwa kuwavurumisha mateke na kuwapopoa makofi. uk 77

Kutokana na maneno hayo, mtu anaachwa kuwahurumia wahusika wanapopitia misukumano kama hiyo mara nyingi kwa vile safari yenyewe ni ndefu sana.

Wafikapo Nimule, ukali wa hali ya anga unashuhudiwa tena. Wakati huu jua limewatesa sana kama tunavyoambiwa.

Ilikuwa kiasi cha saa saba mchana... miale ya jua ilitapakaa kila mahali, ikiunguza kama moto. Joto lilikuwa likichemka, si juani si kivulini. Juani jua likiunguza, kivulini upepo ukiunguza. uk 83

Shida ya ukosefu wa magari ya usafiri yajitokeza tena wanapoamrisha kurudi Kampala tena wakachukue viza ya kuingia Sudan. Katika Safari ya kurudi kutoka Gulu mpaka Mbale, waabiri lori la mizigo ambalo Shafi asema linamfanya ahisi maumivu na kufusika mwili wake wote. Ukosefu wa magari ya usafiri waendelea kushuhudiwa kati ya Nimule na Juba kulikokuwa na shida kubwa. Kwa kuwa hapakuwa na chombo maalum kwa kuhudumia njia hiyo, usafiri uliotegemewa ni wa malori ya kubeba bidhaa. Hata hivyo ilikuwa shida kupata lolote lililotaka

kuwabeba. Hii ndiyo sababu wanapopata moja, wanafurahi sana kiasi cha kuwafanya kucheka na kuimba njia nzima mpaka wanapofika walipokuwa wakienda.

Safari yao ya kuingia Sudan nayo imekumbwa na tatizo la vumbi nyingi. Shafi anasema kuwa mwendo wa kasi wa treni ulilitimua vumbi lililotimka likajaa hewani na kumiminika ndani ya mabehewa. Anasema kuwa wote walikuwa tafrani kwani kulikuwa na vumbi nje, ndani na kila mahali. Hii yatokana na jangwa la Sahara. Wanapofika Khartoum, wanakaribishwa na shida ya jua kali na joto lisilojua kiasi. Shafi anasema,

Mwili wangu ulikuwa ukijikamua jasho utadhani niliyekuwa karibu na tanuri. Michirizi ya jasho ilikuwa ikichirizika uso mzima. Ilichirizikia kifuani na mgongoni. Shati langu liliroa chepe chepe.  
uk 235

Kwa hivyo shida za safari ndefu kama hii ya akina Shafi ni zile ambazo wahamiaji wengine hupitia hasa wakimbizi wanaotorokea kokote. Hawa huwa hata hawana vyombo vyovyote vya usafiri isipokuwa kutembea kwa miguu kilomita nyingi sana. Safari kama hiyo ni hatari kwani licha ya kuishiwa na nguvu, mtu aweza pia kuuawa na wanyama wa mwituni. Wengine hata hupotea njia kwani hupitia kwenye milima na mabonde na hufia huko. Ni mara nyingi shida za safari hasa za maji zimeangaziwa kwenye runinga kuhusu wahamiaji wanaoangamia baharini wakijaribu kutoroka vita na taabu kwao. Wengi huwa wakitaka kuhamia Marekani na nchi za Ulaya. Kwa kukosa nauli ya kusafiria, wengine huchupia meli lakini mwishowe huanguka majini kwa kuishiwa na nguvu au kubebwa na mawimbi makali.

Shida za safari za wahamaji ambazo zimejitokeza kupitia kwa Shafi na wenzake ni kama ifuatavyo. Kuna ukosefu wa magari ya usafiri unaowapelekea kuabiri vyombo vya mizigo, kubadilika kwa hali ya hewa ambapo kunakuwa na joto, jua na baridi kali.

Pia kuna mwendo mrefu unaowabidi kuvumilia usafiri wa usiku na mchana kwa zaidi ya wiki nzima mfululizo hasa safari ya meli na shida nyinginezo.

#### **4.1.1.2 SHIDA ZA CHAKULA**

Chakula ni kitu muhimu sana katika maisha ya mwanadamu na kiumbe yeyote yule. Watu wengi huwa na shida za chakula hasa wale ambao si wakulima. Hata wale ni wakulima wanaweza kukumbwa na shida za chakula ikiwa kilimo chao hutegemea mvua na hawapati mvua ya kutosha. Lakini shida ya chakula inakuwa kubwa kwa wale waliombali na kwao walikokuwa wakipata chakula kwa urahisi. Mambo yanakuwa mabaya zaidi kwa wale hawana namna au pesa za kununua chakula. Hali hii ndiyo Shafi, wahamaji na wahamiaji wengine hujipata.

Katika kitabu hiki Cha *Mbali na Nyumbani*, tumeonyesha jinsi wahusika wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji wamekumbwa na shida za chakula. Tumetoa mifano kadhaa ya kuonyesha hali hiyo. Mfano wa kwanza unajitokeza wakati Shafi anaanza safari hiyo yake. Kwa vile hakuwa amebeba chakula chochote, ajipata matatani. Anasema,

Nilikuwa sikujiandaa kwa chakula nikiwa safarini. Nilitegemea kuomba chakula mumo humo melini. Siku moja nilipokuwa jikoni kuomba mkate, nilimkuta mpishi akitoa jichwa la nguruwe kutoka kwenye oven. uk 16

Anaeleza vile jambo hilo linavyomshtua kwa sababu yeye akiwa Mwislamu, hapaswi kula nyama ya nguruwe. Lakini kulingana na vile mambo yalivyokuwa, hakuwa na lingine la kufanya isipokuwa kuvunja kanuni hizo kama hakukuwa na chakula kingine melini. Hii inaonyesha wazi kwamba Shafi amekabiliwa na shida kubwa ya chakula. Shafi anazidi kutufafanulia vile wananusuliwa na ufadhili wa Waarabu wanaokutana nao melini. Waarabu hawa wanawagawia chochote kile wanachokipika na wanakula wote. Pia anasema kuwa, mara moja moja anaenda

jikoni na wapishi wanamgawia makombo ya mikate wanayoisaza. Akiwa Mombasa baada ya kurudishwa kutoka Aden, Shafi akabiliwa na shida ya chakula tena. Anaeleza vile kwake maisha yalikuwa magumu sana na baaadhi ya siku hata ilikuwa shida kuupata mlo wa siku moja. Anasema,

Nililala na njaa nikaamka na njaa na ilipofika saa sita mchana, njaa ilinizonga sawasawa. uk 29

Anasema kuwa, hali hii inamfanya aombe vipande viwili vya mbata anazozikuta zikiwa zimeanikwa nje ya duka moja. Anasema kuwa vipande hivyo viwili vya mbata na gilasi moja ya maji ndivyo vilivyokuwa chakula chake cha siku mbili. Anasema kuwa maisha yake huko yaliendelea kuwa hivyo kwa muda. Wakiwa melini tena, wanakumbwa na shida ya chakula. Anaeleza,

Akiba ya chakula tuliyokuwa tumbakiwa nayo ilikuwa ni mkate mmoja tu na makopo yetu ya samaki. Nayo yalikuwa yakimalizika. Iitubidi tusiyaendekeze matumbo yetu na kufakamia tukawa waroho kwa chakula kidogo tulichobakiwa nacho. uk 226

Shida ya chakula inajitokeza tena wakiwa Khartoum ambapo wanashindwa kula mara mbili kwa siku kama kawaida. Yaani, chakula cha mchana na chajio na badala yake wanakula mara moja kwa siku. Hiyo ni baadhi ya mifano ya kuthibitisha kuweko kwa shida ya chakula kwa wahamiaji hawa.

#### **4.1.1.3 SHIDA ZA MALAZI**

Malazi ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi ya binadamu. Kwa hivyo, kila mja huhitaji mahali pa kukaa na kujipumzisha baada ya kazi mchana kutwa. Wahamiaji mara nyingi hukumbwa na shida ya malazi hasa wale hawamjui yeyote kule waendako. Hili pia hufanyika ikiwa hawana uwezo wa kukodi chumba cha kulala hotelini. Hii ndiyo hali Shafi na wenzake wanajikuta

wakiwa wahamiaji mahali kwingine. Tumetoa mifano ya kuthibitisha kauli hiyo. Kwa mfano, Shafi anaporudishwa kutoka Aden, anajipata akianza kuishi mahali anapopaita Maskani, kuliyoko Mwembe Tayari huko Mombasa. Kulingana na maelezo yake, wakazi wa Maskani ni watu wa kipato cha chini hasa wanaofanya kazi za vibarua bandarini. Maelezo yafuatayo yanaweka wazi maisha ya wakazi wa Maskani.

... Ilikuwa maskani ya maluuni watupu. Nyumba ya uhuni na ulevi... kilikuwa kijumba kidogo cha udongo kilichokuwa kimebanwa katikati ya vijumba vingine... Ndani ya nyumba hiyo mlikuwa kiza kitupu. Ukiingia utadhani umeingia pangoni. Mwanga mdogo uliothubutu kuingia humo uliingia kwa tabu... uk 28

Anaendelea kusema vile, ndani ya nyumba hiyo, hakuna usiku uliopita salama bila ya walevi kugombana, kupigana na siku nyingine hata kuchomoleana visu wakitaka kuchinjana. Shafi anaeleza jinsi usiku wake wa kwanza hapo ulivyokuwa na mashaka matupu. Anasema kuwa, alipoingia humo, alipata kitanda kilichokuwa kimekunjwa akakikunjua akalala. Usiku wa manane ulipofika, mwenyewe alikuja akaanza kulaani na kutukanana. Alianza kumkemea kwa kuchukua kitanda chake na kumtisha kuwa angemkojolea mara moja. Shafi anasema,

Alikuwa amekwishafungua vifungo vya suruali yake na ninafikiri ningelichelewa kidogo tu kuamka angelinijaza mkojo uso mzima... Nilimpisha, nikaenda kulala nje ambako wengi walikuwa wametandikwa mikeka, wamelala sesa utadhani walikuwa matangani... Maisha ya Maskani hivyo ndivyo yalivyokuwa na ukorofi wake wote, ilinibidi niyazowee kidogo kidogo. uk 29

Maelezo hayo yanatufahamisha kuwa, wahamiaji hupata shida nyingi za malazi. Hii ni kwa sababu ya kutomjua mtu yeyote na kutojimudu kifedha ili wakodi vyumba vya kulala.

Wanapofika Eldoret, shida ya malazi inajitokeza tena lakini wakati huu, mambo si mabaya kama yalivyokuwa Mombasa. Eldoret wanabahatika kupata chumba cha kulala kutoka kwa marafikize Abdalla Juma Bulushi. Marafiki zake ni vijana wawili wa Kisomalia ambao wanawaonyesha pa kulala ila tu chumba hakina kitanda chochote. Wote wanalala sesa juu ya mablanketi yaliyotandikwa chumbani humo. Chumba chenyewe ni kikubwa na kwao, mambo ni mazuri kwa sababu kuna usalama na amani si kama maskani kulikojaa ukorofi na aina zote za uhuni.

Akiwa Bungoma, maisha ya uhamiaji yamsukuma mpaka anaanza kuishi msikitini. Anakubaliwa kulala katika chumba kimoja msikitini. Hayo ndiyo yanayokuwa makazi yake wakati wote anapokuwa Bungoma. Anasema,

Hicho chumba nilichoruhusiwa kuishi kilikuwa chumba kidogo sana kisichokuwa na chochote ndani. Si cha kulalia si cha kukalia. uk 123

Kuishi msikitini si jambo ambalo mtu yeyote angefurahia. Hii ni kwa sababu msikiti ni mahali pa kumwabudu Mwenyezi Mungu na si mahali pa kuishi. Hii ndiyo sababu Shafi anaona haya msichana anayelitwa Mariana anapomwambia ampeleke kwake, Shafi anamzungusha. Hataki kumwambia sababu ya kukataa kwake. Sababu ni kwamba hataki Mariana ajue hana kwake. Jambo hili linamnyima ile hali mtu hasa mwanamume huwa nayo ya kujiamini akijua kuwa ana mahali anapoweza kupaita pake. Haijalishi ikuwa ni chumba cha kukodi au ni nyumba yako mwenyewe.

Mambo yazidi kuwa mabaya Shafi na vijana wenzake wanne, wawili kutoka Zanzibar na wengine wawili kutoka Kenya wanapoanza kulala nje ya stesheni kuu ya reli jijini Khartoum. Waifanya nje ya stesheni ya reli makazi yao mapya wakingoja kupata viza ya kuwawezesha kuingia Misri.

Anasema,

Sisi hatukuwa wanaowasili wala wanaosafiri ila tukitafuta pa kujisitiri tu... Hapo tulipaona ndipo... Tulitafuta maboksi matupu tukayafumuafumua tukayatandika chini vizuri... uk 252

Anaendelea kusema kuwa taabu, dhiki na mashaka yote alikwishayazoea. Kwa hivyo kulalia maboksi na tofali kuwa mto wake wa kuwekea kichwa halikuwa jambo la kumletea tafara na kumnyang'anya raha ya usingizi wa usiku. Wakiwa wamelala huko nje ya stesheni ya reli, usingizi wao wakatizwa na funza waliokuwa wametapakaa kila mahali wakitoka kwenye kinyesi. Yalikuwa maisha ya shida. Anasema kuwa maisha mjini Khartoum aliyaona yakiwa mzigo mzito kwa vile yalikuwa maisha yasiyokuwa na mahali pa kuyaishi. Anasema kuwa maisha yalikuwa magumu lakini hawakuwa na la kufanya. Hili linathibitika anaposema,

Kwa muda wa wiki mbili hapo ndipo palipokuwa maskani yetu. Hapo ndipo palipokuwa stara ya haja zetu zote za kibinaadamu. Hapo ndipo palipokuwa nyumbani na hapo ndio msalani. uk 267

Kutoka nje ya stesheni ya reli, wahamia mahali wanapotafutiwa na rafiki yao Daniel wa kutoka Sudan. Ingawa chumba chenyewe ni cha udongo, usingekilinganisha na kulala kwao nje ya stesheni. Chumba hiki kimewapumzisha kubeba virago vyao kila asubuhi na kuhangaika navyo barabarani kwa kukosa pa kuviacha. Tunaambiwa kuwa ilikuwa nyumba ya udongo mtupu, tokea msingi mpaka dari. Dari yenyewe haikuwa na paa. Shafi anasema kuwa alimwomba Mungu isinyeshe mvua kwani kungenyesha nyumba hiyo ingelimung'unyuka yote ikageuka rojo. Anasema kuwa, chumbani humo hamkuwemo kitu chochote zaidi ya mbacha uliokuwa umekunjwa na kuegemezwa pembeni. Sakafu ya chumba hicho pia ilikuwa ni vumbi tupu. Mwanga wa mchana vilevile uliingia kwa shida kubwa kupitia kwenye kidirisha kidogo.

Anasema kuwa hata hivyo, palikuwa ni afadhali mara elfu kuliko makazi yao nje ya stesheni yaliyokuwa makazi ya kila mpita njia.

#### **4.1.1.4 SHIDA ZA LUGHA**

Lugha ni chombo cha mawasiliano baina ya watu. Ili mawasiliano yafaulu, ni lazima wazungumzaji watumie lugha inayoeleweka na wote wanaohusika. Katika kitabu hiki, kuna nyakati mbalimbali ambapo Shafi na wenzake wamepata shida ya lugha ya kuwawezesha kuwasiliana na watu kule wanakopitia na pia kuhamia. Tumetoa mifano kama ifuatavyo.

Mfano wa kwanza unajitokeza wakati Shafi na mwenzake Ame wako safarini kwenda Aden. Wakiwa katika safari hiyo, wakutana na abiria wengine wawili. Anasema kuwa hawakuwa na mengi ya kuzungumza na abiria wenzake. Wawili hao walikuwa kila wakati wakiongea kwa Kiarabu kwa hivyo hawakuwa na muda wa kuongea nao. Kutokana na maneno hayo, tunaweza kuchukulia kuwa hali hiyo inasabababishwa na kutoelewana kilugha. Yaweza kuwa hawa abiria wengine wawili hawaelewi lugha ambayo Shafi wa mwenzake Ame wanaongea. Vivyo hivyo, akina Shafi nao hawakielewi Kiarabu na ni kweli kwa maana Shafi amesema mara nyingi kuwa hajui Kiarabu. Anajua maneno machache sana ya Kiarabu.

Tukio la pili linalohibitisha kuweko kwa tatizo la lugha ladhihirika Shafi na mwenzake wanapofika Aden. Hili linatokea wakati wanapohojiwa na afisa wa uhamiaji huko Aden.

Anasema,

Ame alikuwa hajui Kiingereza naye Afisa wa uhamiaji hajui Kiswahili. Ulizuka mtafaruku wote hawakuelewana. Kelele alizozipiga Ame, vurugu aliyoifanya, yote hayo hayakumsaidia kitu chochote. Hatima yake ilikuwa kama yangu nayo ni kurudishwa Zanzibar. uk 20

Yaweza kuwa Ame arudishwa Zanzibar kwa sababu ya kukosa lugha ya mawasiliano. Ikiwa kweli hiyo ndiyo sababu iliyomfanya Ame arudishwe Zanzibar, basi afisi hiyo ya uhamiaji ina shida inayohitaji kushughulikiwa mara moja. Hii ni kwa ajili ya gharama na wakati anaopotezewa Ame anaporudishwa Zanzibar. Jinsi ya kutatua shida hiyo tumetaja katika sehemu ya kutoa suluhisho la matatizo yanayowakumba wahamiaji.

Mara nyingine shida ya lugha inapojitokeza ni wakati wanapokuwa melini. Shafi akutana na msichana mmoja wa Kisudan ambaye amvutia sana lakini ashindwa kujieleza kwake. Msichana huyu anaitwa Nisreen na tunavyoona ni kana kwamba Shafi anataka mazungumzo naye lakini Nisreen hataki kwani anaona haya. Shafi naye anataka kuyaendeleza mazungumzo na Nisreen lakini lugha inaleta shida. Shafi anasema,

Hakugeuka nyuma labda alikuwa na wasiwasi kuwa ningeliyaendeleza mazungumzo. Laiti angelijua kwamba na Kiarabu changu nacho kilikuwa kimeishia pale kwa hivyo hata ningelitaka, nisingeliweza kuendelea na mazungumzo. uk 230

Tunajua na tumesema kwamba lugha ni muhimu katika maisha ya binadamu. Inaweza kutumiwa katika shughuli rasmi na shughuli za kawaida. Hii inadhihirika vizuri wakati akina Shafi wakiwa katika harakati zao za kuitafuta viza ya kuingia Misri, wanazoeana na kujenga ushuba wa kufanyiana masihara na bawabu wa Ubalozzi wa Misri ulioko Khartoum. Hili limetokana na kwenda kwao huko mara nyingi. Shafi anatufahamisha kuwa mazungumzo yao ya kufanyiana mzaha yalikuwa hayana lugha maalum kwa sababu bawabu huyo hakuwa mjuzi wa Kiingereza na wao hawakuwa wajuzi wa Kiarabu. Kwa hivyo, mzaha wao uliishia kwenye mazungumzo kuhusu viza tu. Hapa, umuhimu wa lugha ya mawasiliano unaibuka kwani ushuba waliojenga ungewawezesha kufahamiana zaidi na kuongea juu ya mambo mengine yaliyo nje ya shughuli za viza. Haya yangewapunguzia huzuni walio nao kwa kungojea viza hiyo kwa muda mrefu.

Pia ingewafanya wafurahie kwenda kwao kwenye Ubalazi huo hivyo basi kufupisha urefu wa siku hiyo.

Wakati mwingine shida ya lugha inaposhuhudiwa ni pale Shafi anapoenda kujihusisha na kahaba wa Kisudan. Mwishowe wanajiona wakitumia lugha ya ishara hasa wakati ulipofika wa kuitishana pesa. Mazungumzo yao yamekumbwa na tatizo la kuelewana mpaka wakabaki kutazamana. Hali hii imewawezesha kuelewana kama Shafi anavyotueleza,

Aliniuliza kwa lugha niliyoshindwa kuelewa... Alizungumza kwa lugha ya wenyeji wa Sudan ya Kusini ambayo masikioni ilisikika kama Kiarabu koko. Nilibaki kumtazama tu na yeye akinitazama. Nadhani aliiona waziwazi hamu iliyokuwa imenijaa kwa kunitazama machoni tu.  
uk 331

Shida ya lugha inapatikana tena katika afisi ya balazi wa Misri jijini Khartoum. Shafi anatuambia vile mazungumzo marefu yalivyoendelea kati ya balazi na afisa wake. Anasema kuwa mazungumzo hayo yalimpita hivyo hivyo bila ya kuelewa chochote. Kiarabu chake alichokiokotaokota Khartoum hakikutosha kumfanya aelewe kilichozungumzwa. Baada ya mazungumzo yao, balazi amzungumzia Shafi kwa Kiarabu lakini haelewi anamwambia nini. Hivyo basi, Shafi abaki kumtazama tu. Anasema,

Alibaini kuwa sikuelewa aliyoniambia kwa hivyo aliamua kuzungumza na mimi kwa lugha ya kibubu. Alipekechapekecha vidole vyake kama mwenye kuhesabu pesa. uk 338

Wakati huu Shafi ana bahati kwa sababu afisa wa balazi aliye mle chumbani amweleza kwa Kiingereza yale balazi aliyokuwa akimwuliza. Amwambia kuwa balazi alitaka kujua ikiwa Shafi alikuwa na pesa za kugharamia safari yake.

Shida za lugha zaendelea kujitokeza. Wakati huu inahusiana na fomu wanazohitajika kujaza wakiwa mpakani mwa Sudan na Misri wakitaka kuingia Misri. Fomu zenyewe zinawashangaza wote kwani zimeandikwa kwa Kiarabu kitupu. Hili linazua mabishano kati yao na mwenye kuwajazia zile fomu kwa sababu wanalazimishwa kutoa pesa ili wajaziwe. Tatizo ni kwamba hawana pesa. Anasema kuwa walikazana ili wapunguziwe bei hiyo lakini mwishowe iliwabidi kila mmoja wao atoe pauni moja ya Kimisri kwa shughuli hiyo.

Matatizo ya lugha yanatokea tena wakati huu wakiwa Misri. Usiku mmoja wakiwa katika kambi ya kijeshi huko jangwani, Shafi akabiliana na mauti. Anapotoka nje ya banda lao kwenda kujisaidia, apatana na mlinzi ambaye hawaelewani kilugha. Askari yuko katika harakati zake za kuilinda kambi hiyo. Anaposikia nyayo za Shafi nje anainua bunduki tayari kuifyatua wakati wowote lakini kwa bahati nzuri, Shafi aokolewa na mwenzake kambini anayeitwa Mohammed. Shafi aeleza,

Wakati nikiwa nimeelekezwa bunduki kifua, mikono nimeinyanyua juu, nimesimama kama mateka wa kivita, nilimsikia mwenzangu mmoja, Mohammed, akisema, *Amaan! Amaan!* uk 400

Mohammed anayejua Kiarabu ndiye anayemweleza askari huyo wao ni akina nani na wanafanya nini kambini mle. Ni baada ya maelezo hayo askari huyu anapomwachilia mateka wake na kuiondoa bunduki mbele ya kifua cha Shafi. Shida hii ya lugha ya kuwasiliana humpa mtu changamoto hasa mhamiaji kwani humnyima uhuru na uwezo wa kutangamana na watu ipasavyo. Hii ni kwa sababu inambidi mhamiaji kutafsiriwa mazungumzo kule haelewani na wenyeji wake. Wakati mtu anahitaji mkalimani na hayuko karibu, mtu hutaabika sana.

Shida ya mwisho kuhusiana na lugha inajitokeza Shafi anapoenda Ujerumani kwa masomo zaidi. Huko, badala ya kuanza masomo yaliyompeleka huko moja kwa moja, inampasa kujifunza

Kijerumani kwanza. Kwa hivyo arudi darasani tena lakini kama anavyosema, darasa hili la sasa si kama lile alilolikumbuka katika Chuo cha Ualimu. Hilo lilikuwa la kufunzwa taaluma na maarifa. Hili lilikuwa darasa la kufundishwa *a b che* lakini *a b che* zenyewe zilikuwa ni za Kijerumani. Anasema kuwa Kijerumani alichokijua kilikuwa ni maneno machache ya matusi aliyokuwa akimsikia mzee wake marehemu Bwana Mahmoud akimwita mpinzani wake. Huu ulikuwa wakati wa mchezo wa dhuluma pale Baraste, Zanzibar. Alimwita, “*Du schsein*” Anaendelea kusema kuwa, ingawa hakujua maana yake, alikuwa na hakika kwamba yalikuwa matusi. Anasema kuwa, alidhani Bwana Mahmoud aliyapata maneno hayo kutoka kwa watawala wa Kijerumani walioitawala Tanzania wakati mmoja. Kwa kifupi, jambo hili la kulazimishwa kujifunza Kijerumani lampotezea wakati mwingi sana. Anasema,

Ilitubidi tujifunze lugha ya Kijerumani, lugha ambayo sikujua kabisa. uk 473

#### **4.1.1.5 MATESO YA KISAIKOLOJIA**

Mateso ya kisaikolojia ni mawazo yanayoingia akilini mwa mtu na kuanza kumsumbua akili. Hali hii haijaitokeza sana. Mfano ni pale Shafi anatueleza vile wanapokwama Khartoum, anaanza kuona safari ikiwa ndefu na yenye misukosuko mingi. Mwingine hata haiwi kadiri yake. Anasema,

Mambo ya nyumbani nayo yalikuwa yakinidhihirikia mbele ya macho yangu. Baba na mama na ndugu. Nilikuwa na hakika kwamba mama na baba yangu walikuwa na unyonge mkubwa wakihiisi mtoto wao labda nimeangamia kule ambako wao hawakujui. Ndugu zangu walikuwa bado wadogo na mimi nilikuwa ndio tegemeo pekee la wazazi wangu la kuwasaidia kuwalea. uk 263

#### **4.1.2.0 MATATIZO YA KIUCHUMI**

Matatizo ya kiuchumi ni yale yanayotokana na mawazo ya kisaikolojia kuhusiana na fedha, shida za pesa, ukosefu wa ajira, changamoto za kikazi na mengineyo. Matatizo ya kiuchumi hasa ukosefu wa pesa ndiyo yaliyoifanya safari ya Shafi kuwa ndefu kama anavyotueleza. Anasema kuwa safari ambayo ingemchukua mwezi mmoja kwa meli, mwishowe yamchukua mwaka mzima. Ni safari isiyoeleweka kwa sababu, kawaida mtu anayekwenda Ulaya kama anavyosema, hupanda ndege na kwenda lakini safari ya Shafi si ya moja kwa moja. Kwa kujadili matatizo ya kiuchumi yanayowakumba wahusika wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji, tumeanza na mawazo ya kisaikolojia kuhusiana na uhaba wa pesa.

#### **4.1.2.1 MAWAZO YA KISAIKOLOJIA YANAYOHUSIANA NA UKOSEFU WA PESA**

Haya ni mawazo yanayowakumba wahamiaji kutokana na ukosefu wa pesa. Hili hutokea kwa sababu, wahusika wana wasiwasi ya kutojua vile watakavyopata chakula na mahali pa kulala. Kwa mfano, Shafi anapoanza safari yake kutoka kwao Zanzibar, anaeleza jinsi anavyowaza kuhusu safari inayompeleka mahali hamjui mtu yeyote. Anasema,

Niliangalia mbele tu kule ninakoenda. Niliwaza kwamba ninakwenda Aden, nchi ya ugenini. Nilikuwa simjui mtu, sikuwa na mwenyeji wa kufikia, sikujua ningeishi vipi. Mimi nilikuwa ninakwenda tu. Nilikuwa nina shilingi chache sana mfukoni. uk 15

Mawazo ya aina hii humtia mtu wasiwasi sana na kuendelea kumsumbua. Haya ni mambo yanayotokea kwa watu wengi wakiwa katika hali kama hiyo. Kwa hivyo ni mambo ya kweli na yanaleta uhalisia wa mambo. Tatizo la Shafi kuingiwa na mawazo kuhusu maisha ya uhamiaji afikapo Mombasa yanamsumbua kama yalivyomsumbua alipoelekea Aden.

Anasema,

Baadhi ya wakati... huwaza mustakbali wa safari yangu na maisha yangu... Ningelifanya nini Mombasa? Ningeliishi vipi Mombasa? Sikuwa na ndugu, sikuwa na jamaa, sikuwa na yeyote niliyemjua. uk 24 - 25

Shafi anapohamia Bungoma kabla ya kupata kibarua kwa Abdo, alemewa na mzigo wa maisha kwa jumla. Hili linajitokeza katika kauli ifuatayo.

Kuanzia hapo ilinibidi niyabebe maisha kichwani peke yangu. Yalikuwa mazito na jinsi yalivyokuwa mazito nilijihisi kama niliyeubeba Mlima Elgon. Niliogopa usije ukanitopea. Nilijisikia kama ninausemesha mlima ule nikiuomba usinigeukie ukawa mzigo mzito kwangu badala ya kuwa mwanga wa kuiangaza njia ya safari yangu. uk 122

Shafi anasema maneno haya baada ya kuhama kwa Bwana Bakari aliyekuwa mwenyeji wake tangu aingie Bungoma. Alikuwa anakula na kulala kwake. Sasa anaenda kuanzisha maisha mapya msikitini ambako hana chochote. Kuteseka kwao kisaikolojia kwatokana na shida ya pesa. Hayo mawazo ya mhusika kujisikia hana yeyote wa kutegemea akiwa mahali pageni yanaibuka tena Shafi anaposema,

Kwetu Khartoum palikuwa ni ughaibuni, mbali na nyumbani. Hatukuwa na ndugu, hatukuwa na jamaa, hatukuwa na rafiki, hatukuwa na mwenyeji. Katika hali kama hiyo, tusingelithubutu kuzitumia pesa chache tulizokuwanazo kwa anasa ya kuishi hotelini au kwenye nyumba ya kulala wageni. uk 251

#### 4.1.2.2 SHIDA ZA PESA

Pesa ni kitu muhimu sana katika maisha yetu. Bila pesa, huwezi kufanya mambo mengi sana. Tumetoa mifani mingi katika riwaya hii kuthibitisha kuweco kwa shida za pesa kwa Shafi na wenzake. Kwa mfano, Shafi anatuambia vile uhaba wa pesa unamkabili mapema anapoanza safari yake. Anasema kuwa vishilingi vyake vichache alivyokuwa navyo alivimaliza kwa chakula wakati akiwa Tanga na Mombasa na walipoondoka Mombasa, alikuwa hana hata senti moja. Unaposikia hivyo unabaki tu kumhurumia na kushangaa vile ataweza kukamilisha safari ndefu namna hiyo bila pesa.

Tukio lingine ambalo linadhihirisha kuweco kwa shida ya pesa ni kule kurudishwa kwa Shafi kwao. Hii ni kwa sababu ya kukosa shilingi mia sita zilizohitajika kuwekwa dhamana ili aruhusiwe kushuka Aden. Kurudishwa kwake kunakopelekea kuhamia kwake Mombasa ni thibitisho wazi kwamba Shafi ana shida ya pesa.

Wakati mwingine shida ya pesa inavyojitokeza ni pale Shafi anapokonywa pasi ya kusafiria kwa kukosa kulipa nauli anayodaiwa ya kutolewa Aden mpaka Mombasa. Anasema,

Mimi pesa sina. Labda nitafute kazi hapa Mombasa na nitakapozipata hizo pesa nikulipe...

Alichukua pasi yangu ya kusafiria na nilishuka Mombasa bila ya pasi yangu ya kusafiria. uk 26

Si Shafi tu ambaye anadhihirisha kuweco kwa shida ya pesa. Marafiki zake Abdalla Juma Bulushi na Abdalla Juma Maharuki pia ni vivyo hivyo. Hii inajitokeza wakati wanapofika Nairobi kutoka Mombasa.

Shafi anasema hivi,

Kwa mshangao mkubwa niliwasikia wenzangu wakilalamika kuwa wameishiwa na pesa. Mimi nilibakia nimepigwa na bumbuwazi, najiuliza, vipi? Watu hawa walisema wana pesa za kutosha za kugharamia safari ya kutoka Mombasa mpaka Kairo, pesa nyingi za kutosha kujilipia wao pamoja na mimi, leo ghafla, wanasema wameishiwa na pesa ilhali bado hatukufika popote. uk 49

Pia wanapofika Jinja wanaona njia rahisi ya kufika waendako na kumpata mwenyeji wao ni kukodi tekisi. Lakini baada ya kushauriana, wanaona kuwa hiyo ingekuwa na anasa ambayo katika hali waliyokuwa isingekuwa na maslahi kwao. Kwa hivyo, waamua kwenda kwa miguu. Umuzi huo wa kutembea ingawa wanakoenda ni mbali na wana mizigo waonyesha kweli wana shida ya pesa. Kadiri wanavyozidi kukaa Khartoum, ndivyo uhitaji wao wa pesa unavyozidi.

Shafi anasema,

... hali yetu katika mji wa Khartoum na ulitima ulitunyemelea taratibu... kila *gurshi* niliyokuwa nayo mfukoni niliipigia hesabu... katika hali hiyo, hali ya kupangua bajeti ndivyo siku ilivyonipambazukia. Njiani tukitembea mimi nilikuwa nikipanga na kupangua. uk 301

Maneno hayo yaonyesha jinsi shida ya pesa inavyomsumbua kiakili. Shida ya pesa za usafiri ndiyo vilevile inayomfanya kuingiwa na fikira za kutaka kuchupia meli kutoka *Port Sudan* mpaka Ulaya ingawa ni safari ndefu na ngumu.

Shafi akiwa safarini kwenda Ujerumani kwa masomo zaidi, ajipta tena akikabiliwa na shida ya kulipa kodi ya uwanja wa ndege wa Zurich. Si yeye peke yake bali kuna abiria wengine. Anasema kuwa kulipa kodi hiyo ilikuwa ni kadhia kubwa kwao wote. Wote hawakuwa na pesa na hapo ndipo mmoja wao, Suleiman alipozikumbuka zile dola ishirini alizotumia kwa njia isiyofaa. Huyu anajuta kwani wangetumia dola hizo wakati huo kutoa malipo hayo.

Hiyo ni baadhi ya mifano inayothibitisha kuwoko kwa shida ya pesa katika maisha ya uhamaji na uhamiaji kwenye kitabu hiki.

#### **4.1.2.3 UKOSEFU WA AJIRA**

Tunaweza kusema kuwa, ajira ni kazi ambayo mtu hufanya halafu analipwa. Siku hizi kuna ukosefu mwingi wa ajira ulimwenguni hasa katika nchi zinazoendelea. Inasemekana kwamba maovu mengi yanayotendeka miongoni mwa vijana wetu hutokana na ukosefu wa ajira. Uovu huo ni kama vile: biashara na matumizi ya dawa za kulevya, wizi wa mabavu, utekaji nyara na mafunzo yanayoingiliana na ugaidi. Mafunzo haya hulenga kuwafanya vijana wa Kiislamu kuchukua msimamo mkali wa kidini usiovumilia dini nyingine.

Tukirejelea mifano ya ukosefu wa ajira katika kitabu hiki, tunapata mfano wa kwanza kupitia kwa Shafi anaporudishwa Mombasa. Baada ya kupokonywa pasi yake ya kusafiria, hana budi ila kuanza kutafuta kazi ya kumwezesha kuikomboa pasi yake. Anasema,

Sikuwa na kazi wala bazi. Niliranda katika mji huo mashariki na magharibi... Nikitafuta kibarua chochote kile. Lakini kila nilipotaka kutia mguu wangu nilikabiliwa na bango lililotundikwa mlangoni likiniambia, Hakuna kazi. uk 31

Jambo kama hilo hufisha moyo sana. Shafi anasema kuwa akiwa katika harakati za kuhangaikia kazi katika bandari ya Kilindini, anazidi kukabiliana na vibao vilivyotundikwa milangoni vikimjulisha kwamba hakuna kazi. Anasema kuwa vibao hivyo havikumkatisha tamaa kwani anaamini kuwa mhitaji hachoki. Anategemea kazi ya kuhesabu mizigo iliyokuwa ikiteremshwa kutoka melini lakini angundua kuwa kazi hizo mara nyingi hupewa walio na ujuzi wa hesabu na yeye hakuwa nao.

Ukosefu wa kazi wazidi kushuhudiwa lakini wakati huu, kinachomshangaza Shafi ni kitu tofauti. Anapoamua kwenda kuchukua pasi yake ya kusafiria, anakuta mwanamke wa kizuzugu ofisini. Kinachomshangaza ni kwamba, mwanamke huyu anapomwona Shafi ofisini mwake tu, anamwambia “Hakuna kazi!” inasikitisha kusikia mtu akikwambia kuwa hakuna kazi hata kabla ya kungoja umwambie kile unachotaka. Hii inaonyesha wazi kwamba kuna shida kubwa ya kazi.

Ukosefu wa ajira wajitokeza tena Shafi na wenzake wanapoenda Uganda. Anasema,

Tuliranda kila pembe ya mji wa Kampala kutafuta kibarua chochote kile cha kutuwezesha kupata angalau pesa kidogo ili tuendelee na safari yetu. Lakini hatukufanikiwa. uk 62

Shafi na mwenzake Abdalla Juma Bulushi wanapolazimishwa kurudi Kampala wakachukulie viza ya kuingia Sudan huko, badala yake wanaamua kwenda Bungoma. Wakiwa Bungoma, ndipo wanazunguka wakitafuta kibarua chochote lakini wanakosa. Shafi anasema kuwa, kutwa yeye na Abdalla walikuwa wakiranda pale mjini. Walikuwa wakitoka duka la mtu mmoja wanaingia duka la mwingine. Anasema kuwa kazi yao ilikuwa kupiga gumzo tu kutwa nzima. Anasema kwamba, jitihada zao za kutafuta kibarua chochote kile ili kuwapatia angalau pesa kidogo hazikufanikiwa na ndiyo sababu Abdalla akaamua kujiendea Nakuru kujaribu bahati yake huko.

#### **4.1.2.4 CHANGAMOTO ZA KIKAZI**

Hizi ni shida ambazo watu hupitia katika shughuli zao za kikazi. Hapa tunamaanisha kazi za kuajiriwa hasa wahamiaji. Changamoto hizi zinadhihirika wazi Shafi anapotueleza jinsi kazi ya ukondakta anayoajiriwa na Abdo inavyokuwa ngumu kwake.

Hii inafanyika mwanzoni mwa kazi hiyo kiasi cha kumfanya kujuta kwa nini aikubali. Ugumu wa kazi hiyo unajitokeza anaposema,

Ilinibidi niamke alfajiri kuliko kawaida yangu, niingie katika baridi ya umande ulionyonyota usiku kucha kutika Mlima Elgon. Abiria nao walikuwa wengi na mizigo yao mingi kadhalika. Kuna wale waliokuwa na magunia ya mahindi... kuna waliosafiri na baiskeli zao na mimi nilikuwa ndiye wa kuzinyanyua na kuzipandisha juu ya kipaa cha gari ili Wilson azifunge huko juu. Hayo yote yalihitaji nguvu, ujuzi na uzoefu. Vyote hivyo mimi sikuwa navyo. uk 137

Changamoto nyingine inatokana na mwajiri wake, Abdo kutomwamini. Abdo anaona kama Shafi anamdanganya kwa kutompatia pesa zote zinazotokana na biashara yake ya usafiri wa umma. Wakati Shafi hampatii pesa nyingi, anaona kama anamwibia na ndiposa anamkaripia anapomwuliza,

Vipi biashara siku hizi?...juzi ulileta shilingi hamsini, jana hamsini, kwa nini siku zote huleti nyingi kama leo?...Wacha maneno yako! ...Wewe lazima unaniibia! uk 150

Walakini Shafi anajitetea kwa kumwambia kuwa haiwezekani biashara ikawa nzuri kila siku. Abdo anapoona vile Shafi amekuja juu na wakati huo huo amemkazia macho, anamwambia waachane na hayo na yanaisha. Changamoto nyingine inadhihirika Abdo anapoanza kumshuku Shafi kuwa na uhusiano na mpenzi wake Mariana. Tukio hili linamfanya Abdo amwonye Shafi anapomwambia,

Tena sitaki kukuona ukichekacheka naye. uk 150

Shafi naye anakubali kwa unyenyekevu akiogopa kibarua chaweza kupotea na anakihitaji sana ili afaulise safari yake. Lakini ukweli ni kwamba si Shafi anayemkosea heshima mwajiri wake bali

mpenzi wake Mariana ndiye anayemtafuta Shafi. Hii ni wazi wakati Mariana anamsihi Shafi ampeleke kwake.

#### **4.1.3.0 MATATIZO YA KISIASA**

Haya ni matatizo yanayotokana na mambo ya kisiasa kama vile, sheria za uhamiaji, changamoto za mafunzo na kazi ya kijeshi. Sheria hizo humhitaji mhamiaji kuwa na pasi ya kusafiria, viza ya kumwezesha kwenda nchi anayotaka kwenda na nyinginezo. Matatizo mengine yanahusu changamoto za mafunzo ya kijeshi ambayo hawakuwa wamekusudia kufanya. Hata kazi ya kijeshi yenyewe ina changamoto zake. Tuanze na sheria za uhamiaji.

#### **4.1.3.1 SHERIA ZA UHAMIAJI**

Hizi ni sheria zinazoongoza mambo ya uhamiaji ili wahamiaji wajue jinsi ya kuendeleza mambo yao katika nchi ngeni bila kuvunja sheria za nchi hiyo. Vivyo hivyo, sheria hizo huziongoza nchi husika kuelewa vile watakavyoweza kuzuia na kukabiliana na matatizo ya uhamiaji. Baadhi ya sheria za uhamiaji ni sawa katika nchi nyingi na ndiyo sababu wahusika katika riwaya hii wanaitishwa vitu sawa kote wanakoenda. Kutilia mkazo hoja kwamba baadhi ya sheria za uhamiaji ni sawa katika nchi nyingi, tumepata maelezo ya mhusika Bob katika riwaya ya *Vipanya vya Maabarara* (2007). Bob anaeleza juu ya kuitishwa pasi ya kusafiria wanapokuwa safarini wakienda Tanzania na mwajiri wake Vera. Pasi ndiyo hati muhimu inayohitajika mtu anaposafiri kokote katika eneo la Afrika Mashariki. Asema,

“Tukafika Namanga, mji wa mpakani. Tulishuka, tukaingia kwenye vyumba vya shughuli za uhamiaji. Pasi zetu zilipigwa muhuri upande wa Kenya, kisha polisi wakaja kukagua gari. Kuhakikisha kwamba hatukubeba chochote haramu. Basi tukaelekea upande wa Tanzania – mita ishirini hivi kutoka hapo. Utaratibu ule ule ulirudiwa, mara hii na maofisa wa uhamiaji na polisi

wa Tanzania. Tulipewa vikaratasi vya kujaza. Kueleza ulikotoka, mahali hasa ulikokuwa unaelekea Tanzania na jumla ya siku ambazo ungekaa huko.” uk 124

Mfano wa kwanza katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani* kuhusiana na sheria za uhamiaji unajitokeza mara tu Shafi afikapo Aden. Hapa, anazuiliwa kuingia Aden kwa kutoweza kutimiza sheria moja ya uhamiaji. Anasema kwamba hakudhani kuwa kumkatalia kwake kulikuwa ni kwa ajili ya utovu wa huruma. Alikuwa lazima akubaliane na kanuni na sheria za nchi ile. Sheria ilimlazimu afisa wa uhamiaji awatafutie chombo chochote kile kilichokuwa kikielekea Zanzibar, wapakiwa ndani ya chombo hicho waondoke Aden. Hawakutakiwa kuonekana ndani ya nchi ile.

Sheria yenyewe inaeleweka kupitia kwa kauli hii,

Huwezi kushuka Aden mpaka uweke dhamana ya shilingi mia sita. uk 19

Shafi anaporudishwa Mombasa kutoka Aden na hatimaye kupokonywa pasi yake ya kusafiria, ni sehemu ya sheria hizo. Hii ni kwa sababu ya kushindwa kulipa gharama ya safari yake ya kurudishwa kutoka Aden hadi Mombasa. Sheria nyingine ni mtu kubeba kitambulisho au pasi ya kusafiria kila wakati. Kwa mtu aliyepokonywa pasi yake ya kusafiria maisha yanakuwa magumu sana na ndipo anaposema,

Hapo, ili mtu aweze kuishi kwa utulivu ilimbidi awe na kitambulisho... Kitambulisho pekee ambacho kingeliweza kuninusuru na mtafaruku wa askari ilikuwa ni ile pasi yangu ya kusafiria.

Nayo ilikuwa kule kwa wakala wa meli, asingeliitoa mpaka nimlipe pesa zake. uk 32

Kanuni nyingine inamhitaji mtu kubadilisha pesa za nchi husika mapema au mpakani. Bila hizo, mtu hutaabika sana. Kwa mfano, wanapofika mpakani mwa Sudan, wanashauriwa wawe na pesa za Sudan waingiapo Sudan. Wanaposema kuwa wangetumia pesa za Afrika Mashariki, wanaambiwa kuwa pesa hizo hazitumiwi Sudan. Mwishowe inawabidi wafuate maagizo hayo.

Pia kuna kanuni ya mtu kuwa na viza ya kuingia nchi husika ili aruhusiwe kuingia humo. Ukweli huu unadhihirika wanapofika kwenye mpaka wa Sudan ambapo wanaitishwa viza ya kuingia Sudan na wanasema kuwa hawakujua kama wanahitaji viza ya kuingia Sudan. Wanaambiwa,

Kama hamna viza ya kuingia Sudan hamwezi kuvuka mpaka. Kuanzia sasa hivi mpo chini ya ulinzi wa polisi. uk 85

Baada ya kuingia tu ndani ya kituo cha polisi, hawaulizwi la heri wala la shari. Wapelekwa moja kwa moja kwenye chumba cha mahabusu na wacomewa humo. Kutoka wakati huo, wapokonywa pasi za kusafiria zilizowapa uhuru wa kutembea popote nchini humo bila wasiwasi ya kukamatwa na polisi. Wanapoamua kwenda kuomba viza ya kuingia Sudan, wanaelekezwa kwa Ubalozi wa Sudan ulioko Kampala. Ofisini humo, wanaulizwa maswali kama vile; wanaenda Sudan kufanya nini, na wanaposema kuwa wanapita tu, wanaulizwa wanapita wakienda wapi. Wasemapo kuwa wanaenda Misri, wanaulizwa wanaenda kwa nani na mengineyo. Kwa kifupi, maafisa wa uhamiaji wanataka kuhakikisha kwamba unajua unakoenda ili usije kuwa mzururaji wa kwenda kusababisha uhalifu katika nchi za wenyewe.

Shafi anapokuwa mgonjwa wakiwa Gulu, hali yake inamhitaji kulazwa hospitalini lakini haifanyiki hivyo kwa vile yumo mikononi mwa polisi. Kwetu kitendo kama hicho ni ukiukaji wa haki za kibinadamu.

Pia viza ya kuingia Misri inawalazimu kukaa Khartoum kwa muda mrefu sana. Wanapokonywa pasi za kusafiria mpaka wapate viza ya kuingia Misri. Wanaambiwa,

Kwanza leteni pasi zenu za kusafiria...Itabidi mziwache hapa mpaka hapo mtakapopata viza ya kuingia Misri. uk 239

Elly na Amos nao wazuiliwa na polisi kwa kutokuwa na pasi za kusafiria.

Wanaambiwa,

Wenzenu hawawezi kuondoka hapa. Tutawaweka chini ya ulinzi mpaka tutakapopata maelekezo kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani. uk 240

Elly na Amos hawakushughulika kutafuta pasi za kusafiria kwani walipitia njia za magendo. Huu ni udhaifu unaotokana na Wizara ya Uhamiaji inayoshughulikia mambo ya pasi za kusafiria na mengineyo. Udhaifu huu unajitokeza wakati tunapata maelezo yafuatayo kutoka kwa Elly na Amos.

Walitueleza jinsi walivyoingia Uganda kwa njia ya magendo na kupenya Sudan kwa njia za kujifichaficha wakisaidiwa na wanavijiji wa sehemu walizopitia. uk 231

Maneno haya yanatufahamisha mengi kuhusu shida zinazoikumba Wizara ya Uhamiaji na tumeanza kuelewa asili ya kashifa iliyofichuliwa hivi majuzi nchini Kenya. Kwamba, mhamiaji akiwa na pesa kiasi fulani, anaweza kupewa stakabadhi muhimu kama vile: pasi ya kusafiria, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha kitaifa. Hii inaonyesha vile ufasidi umekithiri katika sekta mbalimbali za nchi nyingi hasa Kenya. Pia inatufahamisha ni kwa nini yule mfanyabiashara maarufu kutoka Nigeria alipatikana tena nchini Kenya hata baada ya kurudishwa Nigeria kwa ndege iliyokodishwa na nchi ya Kenya. Ni jambo la kusikitisha kushuhudia tukio kama hilo ambalo liliaibisha nchi ya Kenya kwani ndege hiyo ilikuwa imetekwa nyara katika uwanja mmoja wa ndege huko Nigeria kwa muda wa wiki mbili. Licha ya aibu hiyo, nchi ya Kenya ilipata hasara ya mamilioni ya pesa kutokana na kuzuiliwa kwa ndege hiyo. La kustaajabisha ni vile huyu Mnigeria alivyorejea Kenya tena siku chache baadaye. Swali ambalo wengi walikuwa wakijiuliza ni vile alivyorudi nchini. Alipitia wapi na maafisa wa polisi walikuwa wapi alipopitia mpakani? Kuna uwezekano wa mambo mawili. Jambo moja ni

kwamba, ufisadi ulitumiwa ama mipaka yetu haina ulinzi na kwa hivyo haina usalama. Labda hii ndiyo sababu kuna ukosefu wa usalama nchini.

Tukiirejelea riwaya yetu tena tunapata kwamba, kutokuwa na pasi za kusafiria kwawalazimu kina Shafi kufanya baraza la wizara ya mambo ya nje kuwa malazi yao. Wanasema,

Usiku ulipoingia hatukuwa na jingine la kufanya ila kupiga kambi palepale barazani. Hatukuwa na wasiwasi wa kupiga kambi hapo. Jengo la Wizara ya Mambo ya Nje lilikuwa na ulinzi shadidi wa askari...Tulitandika mablanketi yetu tukaandaa pa kulala. Kwetu, yote ile ilikuwa ni kheri kwani hatukujua tungelikuwa wageni wa nani usiku ule. uk 241

Ofisi za uhamiaji katika nchi mbalimbali huendesha mambo yao tofauti. Tunasema hivi kwa kuona vile akina Shafi wanavyoachiliwa kulala katika baraza la Wizara ya Mambo ya Nje kwa karibu wiki nzima bila mtu yeyote kujali. Ati kwa sababu baadhi yao hawana pasi za kusafiria na wengine wamepokonywa pasi zao kwa kutokuwa na viza ya kuingia Sudan. Hili linaonyesha kuwa, kuna udhaifu katika ofisi hii ya uhamiaji na unahitaji kurekebisha mara moja.

Akina Shafi wanapowaeleza wenzao jinsi wanavyoshikwa na kusumbuliwa na maafisa wa polisi kwa kuwashuku tu wanapopitia Gulu, wenzao wanauona kama mwiba wa kujichoma ambao hauna kilio. Hii ndiyo sababu Edward na Julius wanawalaumu kwa kupitia Gulu badala ya Moyo ambako watu hawachunguzwi. Haya yanadhihirika Shafi anaposema,

Niliwaeleza Edward na Julius hekaya yetu ya kuwekwa mahabusu Gulu. Walitulaumu kwa nini tulipitia Nimule tusipitie Moyo ambako hakukuweco vizuizi vya mpaka. Niliwaeleza mkasa wa kusumbuliwa nikawekwa uchi na Mzungu Arua. Walicheka. uk 258

Kule kwa Edward na Julius kuwalaumu kina Shafi kwa kupitia Gulu kuliko na vizuizi kwaonyesha vile sheria za uhamiaji huvunjwa kwa kutumia njia za magendo. Hii inaturejesha

kwa hali nchi ya Kenya imejikuta. Inasemekana kwamba, wahamiaji wengine hutorokea mipakani bila ya kugunduliwa na yeyote. Watu kama hawa ndio huja kuwa tishio kubwa kwa nchi. Hii inatufahamisha ni kwa nini baadhi ya sheria zinakuhitaji kueleza mengi kuhusu huko uendako. Kwa mfano, ufikapo nchi hiyo, utakuwa mgeni wa nani? Waenda kufanya shughuli gani? Utakaa huko kwa muda gani? Kama unaenda kusoma ni somo gani ungefanya na masomo yako yangekamilika lini na kadhalika.

Kipindi cha kungojea maombi ya viza ni kirefu kiasi kwamba, wahusika wanataabika sana kwa kuwa hawana mahali pa kukaa wakingojea majibu hayo. Hili linaeleweka kupitia maneno haya,

Kama kawaida yetu, tuliamkia Ubalozi wa Misri ili kwenda kusikiliza jibu letu la “bado”. Hili ndilo tulilolipata tulipofika hapo. Hatukuwa na jingine la kufanya. Kazi ya kuranda mchana kutwa bila ya kuwa na lolote la kufanya ilikwisha tuchosha. Kuranda tu na kuiona siku ikipita hivihivi ni kitu kilichonizidisha uchungu. uk 268

Mwishowe majibu yao yakubaliwa baada ya kungojea kwa muda mrefu na wanalifurahia sana.

#### **4.1.3.2 CHANGAMOTO ZA KIJESHI**

Hizi ni shida wahusika wanazokabiliana nazo wanapojiunga na mafunzo ya kijeshi huko Misri. Maelezo wanayopewa kuhusu amri za kijeshi zaonyesha kuwa mafunzo yenyewe si ya kuchezeza. Hii inadhihirika Shafi anaposema vile wanavyoambiwa kuwa, mtindo wa maisha katika Kambi ile ulikuwa kutoa amri na kutii amri. Wakubwa hutoa amri kwa wadogo na wadogo kutii amri za wakubwa bila ya kuhoji. Wanapoanza mazoezi, wanayaona yakiwa magumu kwani hawakuwa wamezoea.

Anasema,

Tulikimbia masafa marefu. Mimi pumzi zilinipaa juu juu nikihema kama mgonjwa wa pumu. Siku nyingi sikupambana na suluhu kama ile. Adha ya miguu kuzama ndani ya mchanga wa jangwani na adha ya uzito wa viatu, hayo yalitoshwa kuufanya mchakamchaka ule kuwa ni adhabu kwetu. uk 401

Kadiri siku zinavyopita, ndivyo mazoezi yanavyozidi kuwa magumu kwao. Shafi anasema kuwa ulifika wakati alipoanza kujuta.

Nilianza kujiuliza mwenyewe, balaa gani hili nililojitafutia? Zilinjia fikra za kubadili mawazo nijitoe katika shengeshwa ile niliyojiingiza. Lakini nilisema maji nimeshayavulia nguo, wacha niyakoge tu. uk 404

Mafunzo yatolewa kambini na kupelekewa jangwani. Kwa muda wa wiki nzima darasa lao lahamia jangwani ili kuweza kuripua miripuko ya kutisha. Ni mazoezi ya kuchosha na tena huhisi njaa. Mafunzo yachocha wanaporudi jangwani tena kwa wiki nyingine kwa mazoezi ya vitendo, kuripua mabomo yaliyokuwa na nguvu zaidi kuliko waliyoyaripua wiki iliyopita. Wakati huu, karibu mmoja wao aliyekuwa akiitwa Mansour afe. Inasemekana hakutii amri ya kulala na kuinamisha kichwa wakati wa mripuko. Anasema kwamba, mafunzo yao yalizalisha majeruhi wake wa kwanza. Ajali ya Mansour inawaathiri sana mpaka Shafi anaendelea kujuta anaposema,

Hatukujua kama alikuwa hai au alikufa. Hapo ndipo nilipotanabahi kuwa nilikuwa nimejiingiza katika maisha ya hatari, maisha ya roho mkononi. Kila wakati uwe tayari ama kuilinda au kuipoteza. Nilijiuliza tena na tena kama yale ndiyo yaliyokuwa matilaba yangu baada ya kutoroka kwetu nikitangatanga huko na huko. uk 411

Pia tunaambiwa kwamba, baada ya wao kutoka Misri, Abdalla alikwenda Urusi kwa mafunzo zaidi ya kijeshi. Mwishowe anajiunga na jeshi la nchi yao lakini alipouliwa Rais wa Zanzibar, Abeid Karume, Abdalla akamatwa na kuwekwa jela kwa muda mrefu. Baada ya kutoka jela aliachishwa kazi jeshini. Baada ya muda, afya yake ilianza kuwa mbaya. Iliendelea kuwa mbaya huku akisumbuliwa na ugonjwa wa kutetemeka. Ugonjwa huo uliendelea kumsumbua mpaka kufa kwake. Kwa hivyo shida zilizosababisha kifo chake zilitokana na kazi ya kijeshi iliyo na changamoto nyingi.

#### **4.2.0 SULUHISHO LA MATATIZO YA UHAMAJI NA UHAMIAJI**

Tumeangalia jinsi wahusika wanavyojaribu kusuluhisha matatizo yanayowakumba wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji. Kwetu, kusuluhisha ni kutatua. Ni jambo la kawaida kwa binadamu kujaribu kuyatatua matatizo yamkumbapo. Mtu yeyote mwenye akili timamu hawezi kukaa tu bila kufanya chochote anapokabiliwa na tatizo lolote lile. Mtu hujaribu juu chini ili kujiondoa kwa shida hiyo. Hivi ndivyo Shafi na wenzake wanavyojaribu kufanya katika riwaya husika. Ikumbukwe kwamba, si matatizo yote ambayo mtu huweza kujitatia mwenyewe. Kuna mengine ambayo huhitaji msaada wa watu wengine. Hawa waweza kuwa mtu binafsi, shirika au serikali. Kuna utatuzi wa shida za kisiasa, kijamii na kiuchumi. Utatuzi wa baadhi ya shida hizi ndio unaosababisha uhamaji na uhamiaji mwingine

#### **4.2.1 UTATUZI WA MASUALA YA KISIASA**

Utatuzi mwingine si lazima utokane na wahusika wenyewe. Kwa mfano, wakati mwenzake Ame anaporudishwa na afisa wa uhamiaji kutoka Aden, haieleweki amerudishwa kwa sababu gani. Lakini mzozo unaozuka baina yake na afisa wa uhamiaji unaonyesha kwamba, kuna shida ya

kutoelewana. Tatizo kama hilo lisuluhishwe kwa kuweka mkalimani hapo ili awasaidie wale wana shida ya lugha ili jambo kama hilo lizitokee tena.

Shida ya viza nayo zisuluhishwe kwa kuzitafuta na kuzipata kwa wakati unaofaa. Hii itapunguza kutaabika kwa wahusika wakizingoja. Wahamiaji nao wafaa kuwa na stakabadhi muhimu zinazohitajika ugenini kulingana na sheria za uhamiaji. Kwa mfano, Shafi anaposhukiwa kuwa Mkikuyu, kinachomwoko hapa ni cheti cha kuzaliwa. Hiki ndicho kinachothibitisha kuwa yeye si Mkikuyu bali ni mzaliwa wa Zanzibar. Wakikuyu walikuwa wakichukiwa na wazungu sana kwa ajili ya vita vya Mau Mau huko Kenya. Cheti cha kuzaliwa ndicho kinachokuwa suluhisho la tuhuma hiyo.

Subira ni kiti kingine muhimu sana katika maisha yetu na husaidia kutuondolea wasiwasi. Kwa mfano, viza inapochukua muda kupatikana, kina Shafi wajitia moyo wa kuvumilia na kuwa na subira na ndipo anaposema,

Sikuchoka kustahimili tabu na mashaka yote yaliyonifika huko nilikotoka mpaka nikafika hapa nilipo, vipi nishindwe kustahimili hivi sasa, wakati nimekwisha mla ng'ombe mzima, nimebakisha mkia tu? uk 342

Hata katika kambi ya kijeshi, mafunzo yanapokuwa magumu, kinachowasaidia ni uvumilivu na kujitolea kwingi. Anasema,

Lakini nilisema maji nimeshayavulia nguo,wacha niyakoge tu. Nilijikaza hivyo hivyo na kuzidi kuonyesha ukakamavu. Nilijikaza kisabuni, kifua mbele, mguu weka, mguu ondoa, kushoto, kulia, mpaka tulipofika palipodhamiriwa. Palikuwa katikati ya jangwa, mbali kabisa na mabanda ya kambi ile...Hapo, Luteni Sameer alituamuru tusimame, miguu bado tumeikaza. Alipotuamuru turegeze miguu, nilipumua “ofyeeee!” uk 405

#### 4.2.2 UTATUZI WA MASUALA YA KIJAMII

Utatuzi huu unahusu masuala ya kijamii kama vile, shida za safari, chakula, malazi, lugha ya mawasiliano na nyinginezo. Mfano mmoja wakati Shafi anapoingwa na mawazo na wasiwasi kuhusu maisha yake anapohamia mahali asipomjua yeyote. Anasuluhisha hayo kwa kujipa moyo akisema,

Lakini nilikuwa na imani thabiti ndani ya moyo wangu kwamba binadamu asingeliweza kushindwa na namna ya kuishi mahali popote pale. uk 25

Mfano mwingine ni pale Shafi anapokabiliwa na shida ya chakula kwani hakuwa amebeba chakula chochote. Asuluhisha hili kwa kuamua kwenda jikoni kuomba chakula na wapishi wamgawia makombo ya mikate waliyoisaza. Mara nyingine Shafi anapokumbwa na njaa akiwa Mombasa, anatatua tatizo hilo kwa kumkabili mwenye duka na kumwomba vipande viwili vya mbata na anapewa.

Njia nyingine ya kusuluhisha shida ya chakula ni kuamua kuwa na utaratibu wa kula mara moja kwa siku. Ni mlo uliolenga kuzima njaa ya mchana kutwa na kulipa uzito tumbo ili kuziba njaa ya usiku kucha. Mlo huo waula baina ya saa kumi na saa kumi na moja jioni.

Kuhusu shida ya kusumbuliwa na mawazo ya nyumbani ambayo Shafi anayaita maradhi ya kitoto ya kufikiri mambo ya nyumbani, watafuta njia. Wajaribu kujipunguzia hayo kwa kuamua kufanya utalii katika mahali panapoitwa Omduraman huko Khartoum. Anasema kuwa, ziara yao katika mji huo ilikuwa kama maliwazo yaliyomliwaza hayo maradhi ya kitoto.

Kuhamia kwa Shafi msikitini ni suluhisho la tatizo la malazi. Anaamua kumwendea Sheikh Noor baada ya mwenyeji wake, Bwana Bakari kumwambia kuwa chumba alichokuwa akilala kitaanza kutumiwa na wageni wake.

Kutatua shida ya ukosefu wa malazi, waenda kutafuta mahali pa kulala huko Chuo Kikuu cha Khartoum. Ingawa wakosa nafasi hiyo huko, lakini wakutana na kijana ambaye awasaidia sana. Huyu kijana, Daniel, ndiye anayewatafutia nyumba wanayokaa muda wote wanapokuwa Khartoum. Hata kama ni nyumba ya udongo yawasaidia sana.

Kwa kukosa mahali pa kukaa walingoja kupata viza ya kuingia Misri, wageuza mkahawa wanaokula kuwa mahala pao pa mapumziko. Kama si kukaa hapo, basi ingewalazimu wawe wakiranda njiani tu kama anavyosema,

Hatukuwa na pengine popote pa kwenda isipokuwa pale kwenye ule mkahawa tuliokuwa tukila kila siku. Mkahawa huo ulikuwa ndipo kama kijiwe cha wasaka viza waliokuwepo Khartoum.  
uk 302

Hii pia yaonyesha shida ambazo wahamiaji hupitia wakiwa katika shughuli zao mbalimbali. Kwa kukosa mahali pa kwenda au kukaa, hujipata wakirandaranda mijini au kufanya mikahawa ya kula kuwa mahali pao pa kupumzika. Ikumbukwe kwamba si wahamiaji wote huwa na shida hiyo. Wale wana pesa za kukodi vyumba katika hoteli mbalimbali huhamia huko kwa muda wanaotaka. Kuhusu shida za usafiri, wazitatua kwa kuabiri malori na meli za mizigo zinazopatikana na wanabebwa pamoja na mizigo.

Kuhusu tatizo la lugha, tunapendekeza ofisi za serikali zote ziwe na wakalimani wa kutoa tafsiri ya maelezo ya mhamiaji ambaye lugha yake haieleweki mahali hapo. Kulingana na TUKI (1990:57), tafsiri ni habari iliyohamishwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine.

### 4.2.3 UTATUZI WA MASUALA YA KIUCHUMI

Huu ni utatuzi unaohusiana na shida za ajira, changamoto za kikazi, pesa na mengineyo. Kwa mfano, akina Shafi wanapoambiwa warudi Kampala wakachukue viza ya kuingia Sudan, wanashauriana na kuamua waende Bungoma badala ya Kampala. Wanaona kuwa, pesa walizonazo hazitawafikisha popote na huko Kampala nako watahitaji pesa kuipata hiyo viza. Ndipo wanapotoa uamuzi huu.

Tukirudi Bungoma tunaweza kufanya maarifa ya kupata pesa. Uk 101

Shafi anapokabiliwa na ukosefu wa kazi akiwa Bungoma, anajaribu kulisuluhisha kwa kuamua kwenda kutafuta kazi ya kuwa mwalimu wa uchoraji katika shule moja huko Bungoma. Anaeleza vile alikuwa na ujuzi wa uchoraji tangu alipokuwa mwanafunzi katika Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa. Anasema kuwa, alilimudu somo la sanaa vizuri sana na alikuwa miongoni mwa wachoraji wazuri huko. Anasema,

Pale chuoni nilikwishawahi kupata zawadi ya kuwa mchoraji bora mwaka wa 1959. uk 125

Kupata kazi ya kuwa kondakta wa basi moja la Abdo ni suluhisho la shida ya kazi. Hii ndiyo sababu anatia bidii katika kazi hii ingawa ina changamoto nyingi kwani hakuwa amefanya kazi hii tena. Kila shida akabiliana nayo kwa njia inayofaa. Anasema kuwa, Siku zilivyokwenda na kazi ya ukondakta na mbinu zake alizielewa taratibu. Kwa mfano, ilipokuwepo mizigo mizito ya kupakiwa juu ya chanja, alimwomba mwenye mizigo naye amsaidie. Pia ajifunza namna ya kuinyanzua baiskeli ili kuipakia juu ya chanja. Uhuni na uchepe nao auzoea. Anasema,

Yule aliyetaka uchepe, kwangu aliupata... na aliyeutaka uhuni, kwangu aliupata vilevile.

Nilikuwa tayari kwa lolote lile. uk 138

Anatuambia kuwa, kinachohitimisha kazi yake ya ukondakta ni kule kuipokea leseni yake pamoja na beji ya P.S.V. Tatizo la kuogopa kukamatwa na polisi alitua kwa kutafuta na kuvipata vifaa hivyo muhimu. Hivi pia vimemfanya kuwa kondakta aliyetimia.

Kugawiwa *gurshi* mia moja kila mmoja wao ni njia ya kuwapunguzia mzigo wa ukosefu wa pesa. Hii inafanywa na ubalozi wa Ghana ulio Khartoum. Tunaeleza hivi,

Balozi alitia mkono wake ndani ya kibweta, alichota bunda la noti akalishika mkononi. Alituita.

Alianza kutugawia noti zile mmojammoja na kila aliyekabidhiwa noti zake alitoka nje huku akitoa ahsante kubwa. uk 322

#### **4.3.0 HITIMISHO**

Katika sehemu hii, tumeeleza kwa kina matatizo yanayowakumba wahusika katika riwaya hii na jinsi wanavyojaribu kuyatatua. Matatizo hayo ni ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Matatizo ya kijamii yaliyojitokeza ni kama vile: shida za safari au matatizo yanayowakumba wahamiaji wakiwa katika safari zao ndefu kabla ya kufika wanakohamia. Pia tumeangalia shida wanazopata za chakula, malazi, lugha ya mawasiliano na shida nyinginezo. Aidha, tumeshughulikia matatizo ya kiuchumi na miongoni mwao ni: shida za pesa na athari zake kiakili, ukosefu wa ajira na changamoto za kikazi. Vilevile, tumejadili matatizo ya kisiasa yakiwa pamoja na: sheria za uhamiaji na changamoto za mafunzo ya kijeshi. Mwisho, tumejaribu kuonyesha njia za kusuluhisha baadhi ya matatizo hayo.

## **SURA YA TANO**

### **5.0 UTANGULIZI**

Katika sura hii tumetoa muhtasari wa utafiti wetu. Hii ni kulingana na madhumuni ya utafiti kama yalivyodhihirika katika uchunguzi wetu. Lengo la utafiti huu ni kuchunguza suala la uhamaji na uhamiaji katika riwaya ya kitawasifu ya *Mbali na Nyumbani* kwa mtazamo wa nadharia ya uhalisia. Tumeihakiki riwaya hii kwa kuangalia jinsi suala hili la uhamaji na uhamiaji lilivyoendelezwa na mwandishi ambaye ni Adam Shafi.

### **5.1 MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI**

Matokeo ya utafiti wetu yaliongozwa na madhumuni yafuatayo:

- i. Kujadili aina za uhamaji na uhamiaji. Katika kufanya hivyo tumetambua kuwa uhamaji na uhamiaji uliojitokeza katika riwaya hii ni wa aina mbili. Kuna uhamaji na uhamiaji wa hiari na kuna ule wa lazima. Huu wa lazima unatokana na kulazimishwa na hali ya mambo ilivyo kule wahusika waendako. Uhamaji na uhamiaji huu hata hivyo tumeona kuwa si wa lazima kiasi cha kulazimishwa kama vile wakimbizi huhamishwa na serikali zao wakati wa majanga ya kawaida. Uhamaji na uhamiaji wa hiari nao ni ule unaotokana na uamuzi wa mhusika mwenyewe baada ya kufikiria. Walakini, tumepata kwamba Uhamaji na uhamiaji wa hiari ndio unaojitokeza kwa wingi kuliko ule wa lazima.
- ii. Madhumuni yetu ya pili yalikuwa kufafanua sababu za uhamaji na uhamiaji katika riwaya hii. Katika ufafanuzi wetu tumebaini kuwa uhamaji na uhamiaji umechochewa na ari ya wahusika kutaka kujikimu au kujiendeleza kimaisha. Uchunguzi wetu pia ulibaini kwamba uhamaji na uhamiaji mwingine haukunuiwa kuyaendeleza maisha ya wahusika

binafsi kama tulivyofikiria bali ni jamii na nchi kwa jumla. Walakini, tuligundua kuwa sababu kuu ya uhamaji na uhamiaji katika riwaya hii imetokana na kiu ya elimu.

iii. Madhumuni yetu ya tatu yalikuwa kuchunguza manufaa ya uhamaji na uhamiaji. Tulipofanya hivyo, tuligundua kuwa kuna manufaa ya aina tatu. Manufaa haya ni ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Manufaa ya kiuchumi yanatokana na kuajiriwa kwao kazi, kupata mafunzo ya kitaaluma kama vile, uandishi wa vitabu vya fasihi. Pia tumepata kwamba, manufaa ya kisiasa yanahusu wahusika kuweza kupata viza zilizo muhimu ili wakubaliwe kuingia nchi wanazodhamiria kwenda. Vilevile tumegundua kuwa mafunzo ya kijeshi ambayo wahusika wanapata baada ya ushawishi na hamasa za kisiasa yanachangia kuwa wanajeshi kwa baadhi yao hatimaye. Tumetambua pia kuwa, baadhi ya manufaa ya uhamaji na uhamiaji yanatokana na uhusiano wa kisiasa unaopelekea wahusika hao kufadhiliwa kielimu. Juu ya hayo, tumegundua kuwa manufaa ya kijamii ya uhamaji na uhamiaji ni kama vile, kupata elimu na kujenga mahusiano ya kudumu ya kijamii.

iv. Madhumuni ya nne yalikuwa kuelezea kwa kina matatizo yanayowakumba wahusika katika riwaya ya *Mbali na Nyumbani*. Tuligundua kuwa suala la uhamaji na uhamiaji huhusiana sana na shida zinazowakabili wahusika na nchi wanazoenda. Uchunguzi wetu umepata kwamba uhamaji na uhamiaji unaandamana na matatizo mbalimbali. Matatizo haya ni ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Pia tulibaini kwamba tatizo la kiuchumi linachangia sana kuweko kwa baadhi ya matatizo ya kijamii na kisiasa. Kwa mfano, ukosefu wa pesa ndio uliosababisha shida za kijamii kama vile: shida za usafiri, chakula na malazi. Hata kiini cha safari ndefu ya Shafi kimetokana na tatizo la kiuchumi. Pia kubadili mpango wake wa awali wa kwenda Ulaya halafu anajipata Misri ni sababu hiyo.

v. Madhumuni yetu ya tano na ya mwisho yalikuwa kutathmini jinsi wahusika wanavyojaribu kusuluhisha matatizo yanayowakumba. Katika uchunguzi wetu, tulibaini kwamba kuna utatuzi wa masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Tulipata kwamba, kuhusu utatuzi wa masuala ya kisiasa kama upataji wa viza na changamoto za kijeshi, iliwabidi wahusika kuwa na subira, uvumilivu na kuzingatia maagizo. Pia tuligundua kuwa matatizo mengine hawakuwa na uwezo wa kukabiliana nayo kwani yanahitaji suluhu kutoka kwa watu wengine. Kuhusu utatuzi wa masuala ya kijamii tulipata kwamba wahusika walijaribu kutumia njia mbalimbali na walifanikiwa. kwa mfano, shida za safari walizitatua kwa kuabiri malori na meli za mizigo walipokosa vifaa mwafaka vya usafiri. Shida za chakula walitatua kwa kuamua kuanza kula mlo mmoja kwa siku. Shida ya malazi ilitatuliwa kwa kutojali walipolala. Kwa hivyo waliamua kuwa wakilala popote hasa nje ya stesheni ya reli. Utatuzi wa shida ya lugha ya mawasiliano iliwapa changamoto mpaka wakati mwingine walilazimika kunyamaza tu au kutumia lugha ya ishara.

Nadharia zetu tete katika 1.3 zilikuwa tano na baada ya kuzichunguza, tumeona kwamba zote zinathibitika. Kwa hivyo, katika utafiti wetu tumegundua yafuatayo:

- i. Kuna aina mbili za uhamaji na uhamiaji: uhamaji na uhamiaji wa hiari na wa lazima unaotokana na kulazimishwa na hali ya mambo ilivyo huko wahusika wanakoenda.
- ii. Walakini, tumepata kwamba si aina zote za uhamaji na uhamiaji huchochewa na ari ya mhusika kutaka kujiendeleza kimaisha. Tuligundua kuwa aina nyingine zinazochangiwa na mambo mengine hazilengi kuwanufaisha wahusika binafsi bali hunuiwa kufaidi jamii na nchi kwa jumla.

- iii. Uhamaji na uhamiaji una manufaa. Hii imethibitishwa na utafiti wetu uliobaini kuwa uhamaji na uhamiaji una manufaa ambayo ni ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.
- iv. Uhamaji na uhamiaji huandamana na matatizo mbalimbali. Hii pia ilithibitika kwani tuligundua kuwa kuna matatizo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.
- v. Wahusika hujaribu kusuluhisha matatizo yanayowakumba. Utafiti huu umepata kuwa, hili ni kweli ingawa tuligundua kuwa hawawezi kutatua matatizo yote kivyao. Kuna mengine yanayohitaji msaada wa watu wengine.

Kwa sababu kazi tunayohakiki ni ya kitawasifu, uhakiki wetu umehalalishwa na matumizi ya nadharia ya uhalisia. Hii ni kwa sababu nadharia hii husisitiza kwamba, msanii wa kifasihi afaa kuandika juu ya mambo yanayofanyika katika jamii au yanaweza kutendeka katika maisha ya kawaida ya binadamu. Suala la uhamaji na uhamiaji ambalo limejitokeza sana katika riwaya hii ya kitawasifu ndilo limeitawala. Suala lenyewe limejitokeza kupitia kwa mwandishi mwenyewe na kwa hivyo si mambo ya kufikiria bali ni mambo ya kweli. Yote anayoyapitia ni yale yale ambayo watu wengine hupitia wakiwa katika hali ya uhamaji na uhamiaji. Kwa hivyo ni ukweli wa mambo na ni hali halisi ya maisha.

## **5.2 MAPENDEKEZO**

Utafiti huu umejadili suala la uhamaji na uhamiaji kama lilivyojitokeza katika riwaya ya kitawasifu ya *Mbali na Nyumbani* (2013) iliyoandikwa na Adam Shafi. Tumetumia nadharia ya uhalisia inayoafikiana vizuri na mambo ya uhamaji na uhamiaji. Tungependekeza watafiti wengine wafanye uhakiki wa riwaya hii kwa kufanya uchambuzi wa wahusika na matumizi ya lugha kwani hatukuwa na muda wa kufanya hivyo. Vilevile haya yalikuwa nje ya upeo na mipaka yetu.

## MAREJELEO

Amin, S. (1974) *Modern Migrations in Western Africa*. London: Oxford University Press.

Barnum, H.N. & Sabot, R.H. (1976) *Migration, Education & Urban Surplus Labour*. Paris: The Organization for Economic Co-operation & Development(O.E.C.D).

Boyle, N & Swales, M (1986) *Realism in European Literature*. London: Cambridge University Press.

Burhani, Z. (1987) *Mwisho wa Kosa*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Caldwell, J.C. (1969) *The Movement to Ghana's Towns*. New York: Columbia University Press.

Cernea, M.M. (1993) *The Urban Environment & Population Relocation*. Washington D.C: World Bank.

Hance, W.A. ( 1970) *Population, Migration and Urbanization in Africa*. New York: Columbia University Press.

Harris, W.H. & Levey, J.S. (1975) *The New Columbia Encyclopedia*. New York: Columbia University Press.

Hussein, E. (1969) *Kinjeketile*. Nairobi: Oxford University Press.

Kairu, N.C. na Wainaina, W.I. (2006) *Golden Tips*. Nairobi: Moran Publishers.

Kiruthu, F; Kapiyo, J & Kimori, W (2011) *The Evolving World*. Bk.3. Nairobi: Oxford University Press.

Larousse, E. (1968) *Longman English Larousse*. London: Associated Companies, Branches & representatives throughout the world.

Lukács, G. (1972) *Studies in European Realism*. London : The Merlin Press.

Madumulla, J.S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Malywn, J.A. (1960) *American Immigration*. Chicago: The University of Chicago Press.

Margolis, J. (2001) *Selves and other Texts: The Case for Cultural Realism*. Pennsylvania: Penn State University Press.

Mazrui, A (1981) *Kilio Cha Haki*. Nairobi: Longman Kenya Limited

Mbatiah, M. (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Fotoform Limited.

\_\_\_\_\_ (2007) *Vipanya Vya Maabara*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

McNeill, W. H & Adams, R.S. (1978) *Human Migration: Pattern & Policies*. Bloomington. Indiana University Press.

Mkangi, K. (2003) *Walenisi*. Nairobi: East African Publishing House.

Msokile, M. (1992) *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mohammed, S.A. (1980) *Utengano*. Nairobi: Longman Kenya Limited.

Ndalu A.E. na King'ei, G.K (1989) *Kamusi ya Methali za Kiswahili*. Nairobi: East African. Educational Publishers.

Ndalu, A.E., Babusa, H. Na Mirikan, S.A. (2014) *Kamusi Teule ya Kiswahili: Kilele cha Lugha*.  
Nairobi: East African Educational Publishers.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo  
Kenyatta Foundation.

Odhiambo, D.O. (2003) *African Immigration Policies: The Case of Kenya, 1906 – 2000*.  
M.A.(Hakijachapishwa).

Olali, T. (2008) *Mafamba*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

SCOH, F.D. (1972) *The Peopling of America: Perspectives on Immigration*. Virginia: The  
American Historical Association.

Senkoro, F.E.M.K. (1982) *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Shaaban, R. (1951) *Kusadikika*. Nairobi: Thomas Nelson & Sons Limited.

\_\_\_\_\_ (1966) *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*. Nairobi:  
Thomas Nelson & Sons Limited.

Shafi, A. (1978) *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Nairobi: Vide – Muwa Publishers Limited.

\_\_\_\_\_ (1979) *Kuli*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Limited.

\_\_\_\_\_ (2003) *Haini*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Limited.

\_\_\_\_\_ (2013) *Mbali na Nyumbani*. Nairobi: Longhorn Publishers (K)  
Limited.

Skeldon, R. (1997) *Migration and Development: A global perspective*. London: Addison Wesley Longman.

Tuki (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI

\_\_\_\_\_ (2010) *English – Swahili Dictionary 3<sup>rd</sup> Edition*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research University of Dar es Salaam.

Wafula, R.M. na Kimani, N. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (1996) *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Limited.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi. Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

\_\_\_\_\_ (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

\_\_\_\_\_ (2010) *Kanzi ya Fasihi I: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide – Muwa Publishers.

White, P & Woods, R. (1980) *The Geographical Impact of Migration*. London: Longman Group Limited.

*Holy Bible: New International Version* (1984) Nairobi: International Bible Society.

Microsoft Encarta *Online Encyclopedia* (2000)– *Realism art & Literature*).

Josh Rahn *Online Literature* (2011).

Wikipedia the free encyclopedia, Alexander Moseley *Political Philosophy*.